# Nipashe

Jumamosi Septemba 14, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580023

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Mashine ya kisasa uchunguzi saratani ya titi yazinduliwa

UKURASA 3




UKURASA 13

# Serikali yamuonya Musiba

• **Lugola** asema hatumiwi na serikali, aagiza Jeshi la Polisi limchunguze... *Ukurasa 2*



Waziri wa Mambo ya Ndani, Kangi Lugola, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana. **PICHA: WMNN**

## YALIYOMO


UKURASA WA 2

**BUNGE LABAINI UDHAIFU KWENYE UANDISHI SHERIA**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo imelieleza Bunge kuwa imebaini udhaifu katika uandishi wa sheria...

UKURASA WA 11

**SERIKALI YAONYA MAABARA VIPIMO VISIVYO SAHIHI**

NAIBU Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, amesema vituo vingi vya...

UKURASA WA 25

**MAZISHI YA MUGABE HATIMAYE FAMILIA, SERIKALI ZAAFIKIANA**

Hatimaye Serikali, wanafamilia wakubaliana kumzika Uwanja wa Mashujaa...


## Tanzania yasifiwa Mahakama Mafisadi

UKURASA 3

## TCRA yaja na suluhisho utitiri wa ving'amuzi

UKURASA 2


**MICHEZO** **MAJALIWA AZIPA NENO SIMBA, YANGA** UK.31

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Serikali yamuonya Musiba

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi Kangi Lugola, amemuonya mwanaharakati Cyprian Musiba kuacha tabia ya kuuaminisha umma kuwa anatumiwa na serikali.

Pia amemuonya kuwa serikali haitamvumilia kama ataendelea kwa kumchukulia hatua kali za kisheria bila kumwangalia machoni.

Lugola, alitoa onyo hilo jana jijini Dodoma wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake baada ya kumaliza ziara ya kukagua ujenzi wa majengo ya makao makuu ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji pamoja na Idara ya Uhamiaji.

Alisema anamuonya Musiba kuacha tabia ya kuuaminisha umma wa Watanzania kuwa anatumiwa na serikali katika kufanya au kuongea mambo mbalimbali ambayo amekuwa akiyafanya.

"Nitumie fursa hii pia kumuonya mwanaharakati huru Cyprian Musiba kuacha tabia ya kuwaaminisha wananchi kuwa anatumika na serikali, kwani serikali haifanyi kazi na wanaharakati kuna kipindi hadi viongozi wa dini waliandika waraka wakionyesha namna wanavyo aminishwa kuwa Musiba anatumika na serikali kwa yale anayoyafanya," Lugola alionya.

Aliliagiza Jeshi la polisi kuendelea na uchunguzi na pale itakapobainika kuwa Musiba bado anaendelea kueleza vitu ambavyo vinaonyesha kuwa anatumwa na serikali na watachukua hatua kali bila kutamzama machoni.

"Tunamuonya Musiba afanye uanaharakati wake na kuacha kujihusisha na serikali, tupo makini tunafanya uchunguzi wetu na tunapoona kuwa kuna mtu anavuka mipaka tunamuonya," alisema Lugola.

Onyo hilo la Waziri Lugola, limekuja siku chache baada mwanaharakati huyo kudaiwa kuwachafua baadhi ya watu kupitia vyombo vyake vya habari na mitandao ya kijamii

Vile vile, Waziri Lugola aliwaonya watu wanaojihusisha na utapeli kwa kutumia majina ya viongozi wakuu wa serikali pamoja na wizi wa kwenye mitandao kuacha mara moja kwa kuwa Jeshi la Polisi lipo makini na litawabaini.

Aliwatahadharisha watu ambao wanatumia majina ya viongozi kuwatisha watu wengine kwa madai kuwa wametumwa na rais au waziri mkuu.

"Unakuta mtu anawatisha watu kuwa ametumwa na kiongozi au kudai kuwa maagizo hayo yametoka juu kwa Rais na kama watayapinga watakamatwa, hii yote tu ni kutaka kufanya utapeli," Lugola alisisitiza.

Alisema kuwa pamekuwapo na watu wanaofanya utapeli kwa kutumia majengo ya serikali kwa kujifanya Usalama wa Taifa au Takukuru kwa kuwatisha watu hasa wawekezaji.

"Niwaonye matapeli wote wanaotumia njia hii kuacha mara moja, serikali tayari imeshabaini wanachokifanya, lakini pia wananchi wanatakiwa kuwa makini na hawa watu kama wanashida waje katika ofisi zetu na kuacha kuwaamini watu hawa," alitahadharisha.

Awali akikagua ujenzi wa jengo la ghorofa tatu la makao makuu ya Jeshi la Zimamto na Uokoaji alilitaka kubadilika na kuhakikisha kuwa askari wake wanawahi katika maeneo ambayo yanatokea majanga ya moto katika maeneo mbalimbali nchini.

"Niwatake mbadilike katika utendaji wenu kwa namna ambavyo mnakwenda katika matukio ya majanga sio mnakwenda na nyie kushangaa kama ambavyo wanafanya watu wengine lakini pia mtoe elimu kwa wanachi ili waweze kujikinga na majanga haya ya moto"alisema Lugola

Hatahivyo, alilitaka Jeshi hilo kuweka utaratibu wa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara hasa katika Jiji la Dodoma ambalo hivi sasa pamekuwepo na ujenzi wa majengo mengi ya serikali.

INAENDELEA UK.8



Mratibu wa Huduma za Afya na Kinywa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Daisy Majamba (kushoto) na Mkurugenzi wa Masoko wa taasisi ya afya ya wanawake (GE Health care), wakiangalia mashine ya kisasa na ya kwanza katika nchi za Afrika ya kufanya uchunguzi wa saratani, baada ya kuzinduliwa katika hospitali ya Aga Khan, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: ROMANA MALLY**

# TCRA yaja na suluhisho la ving'amuzi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imetangaza utaratibu wa kuwaondolea wananchi adha ya kumiliki visimbuzi (decoder) vingi kwa wakati mmoja kwa kuleta huduma itakayokuwa na kifaa maalum cha kisasa cha teknolojia ya KAM.

Utaratibu utapokamilika vitaanza kutumika Desemba mwaka huu, ili kubadilisha utaratibu wa sasa wa nyumba kuwa na visimbuzi zaidi ya kimoja.

Mkuu wa Kitengo cha Leseni wa TCRA, Andrew Kisaka, alisema kwa mabadiliko hayo kisimbuzi kimoja kinaweza kupokea mawasiliano ya visimbuzi vingi kwa wakati mmoja.

"Tumejikita katika tatizo linalowakumba wananchi wengi kuwa na visimbusi vingi majumbani, kwa kushirikiana na wadau tumekaa tumekubaliana tuingize sokoni visimbuzi ambavyo vitatumia teknolojia ya KAM," alisema.

Kwa mujibu wa Kisaka, vitakuwa na uwezo wa kudaka chaneli zisizo lipia na kwa kutumia kisimbuzi hicho hakutakuwa na haja ya kubadili ili kupata chaneli nyingi.

"Mwananchi atakachotakiwa kufanya ni kununua KAM na kupachika kwenye kisimbuzi uliochonacho nyumbani, kisimbuzi kitakuwa kimoja utakachokuwa unabadilisha ni KAM," alisema na kuongeza:

"Ni kama vile unasimu moja, lakini unabadilisha kadi mbalimbali, tumeshakaa na wadau wote na tumeshakutana na kamati ya bunge inayohusika."

Kisaka alisema, TCRA imeshakutana na wadau wote na sasa utawekwa utaratibu wa jinsi ya kuagiza visimbuzi hivyo kwa nguvu ya soko.

"Visimbuzi vilivyopo vitaendelea kutumika, lakini vilivyo na tekonolojia ya KAM vitaanza kuchukua nafasi ya visimbuzi vilivyopo hadi vilivyopo nyumbani vitakapoisha," alisema.

Vile vile, alisema milango iko wazi kwa mtu yeyote kuingiza visimbuzi vyenye teknolojia ya KAM ilimradi akidhi vigezo na masharti yaliyowekwa.

# Bunge labaini udhaifu wanasheria serikalini

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo imelieleza Bunge kuwa imebaini udhaifu katika uandishi wa sheria na kwamba changamoto hiyo inachagizwa na wanasheria wengi wa serikali kutokuwa na weledi.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Andrew Chenge, aliyasema hayo bungeni jijini Dodoma jana alipohitimisha hoja ya kamati yake kuhusu uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa katika mikutano ya 14 na 15 ya Bunge.

Alisema kamati yake imebaini serikali ina watalaamu wachache wa sheria wenye weledi katika uandishi wa sheria, hivyo kuna haja ya kuchukua hatua ya kuimarisha eneo hilo.

Hoja hiyo iliungwa mkono na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Prof. Adelardus Kilangi, ambaye alikiri kuwapo kwa changamoto hiyo na kueleza kuwa tayari serikali imechukua hatua kwa lengo la kuitatua.

Alisema serikali iko mbioni kuanzisha chuo maalum ambacho wanasheria na mawakili wa serikali watakuwa wanapelekwa kwa ajili ya kuongezwa ujuzi katika masuala ya kisheria na utungaji wa sheria.

**MAKOSA YENYEWE**

Awali, akiwasilisha bungeni jana taarifa kuhusu uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa bungeni katika mikutano hiyo miwili, Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo, William Ngeleja, alisema wamebaini dosari mbalimbali katika sheria ndogo 14 walizozichambua.

Alisema sheria zenye dosari hizo ni pamoja na ya The Medical, Dental and Allied Health Professionals, 2018, ambayo Kanuni yake ya 3(1) inatoa utaratibu kwamba malalamiko dhidi ya daktari yanaweza kuwasilishwa kwa Msajili wa Baraza la Madaktari, lakini neno 'may' lililotumika linaondoa ulazima wa kutumika kwa kifungu hicho.

Alisema kamati pia imebaini baadhi ya kanuni za sheria hiyo zinakinzana na Sheria ya Uhusiano Kazini ya Mwaka 2004 inayotaja muda wa kufanya kazi ni saa tisa kwa siku za kazi, lakini sheria inayolalamikiwa inamtaka daktari aliye mafunzo kwa vitendo kuwapo hospitalini wakati wote.

"Kamati pia imebaini kutofuatwa kwa utaratibu wa uandishi katika Kanuni ya The Civil Aviation, 2018 iliyotungwa chini ya Sheria ya The Civil Aviation, Sura 102," alisema.

Alisema makosa pia yamebainika katika Sheria Ndogo za Uanzishwaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii za Halmashauri za Wilaya ya Madaba, 2018 na The Merchant Shipping Regulations, 2019.

Ngeleja alisema kamati yao inaishauri serikali kuchukua hatua za haraka kuzifanyia marekebisho sheria ndogo zote zenye dosari na baada ya marekebisho hayo kufanyika na kuchapishwa kwenye Gazeti la Serikali, sheria ndogo hizo ziwasilishwe bungeni kwa mujibu wa sheria.

## HABARI KITAIFA




Mkazi wa Jiji la Dar es Salaam, akiwa amesimama mbele ya Kituo cha Polisi Msimbazi, eneo la Kariakoo, jijini humo juzi, licha ya kuwapo kwa onyo la kuzuia kitendo hicho. **PICHA: JOHN BADI**

# Mashine ya kisasa saratani ya titi yazinduliwa

**Na Romana Mallya**

MASHINE ya uchunguzi wa saratani ya matiti yenye uwezo wa kulichunguza titi kwa undani zaidi na kutoa majibu mengi, imezinduliwa jijini Dar es Salaam katika Hospitali ya Aga Khan.

Daktari Bingwa wa Radiologia kutoka Aga Khan, Pili Ally, alisema hayo jana wakati wa uzinduzi wa mashine hiyo iliyonunuliwa kwa gharama ya Dola za Marekani 300,000 (zaidi ya Sh. milioni 700).

Dk. Pili alisema mashine hiyo ina uwezo mkubwa wa kuangalia na kupata vitu vingi zaidi vilivyomo ndani ya titi tofauti na nyingine ambazo zinapiga picha moja na kuona kitu kimoja tu.

Alisema kuwapo kwa mashine hiyo Tanzania kunaifanya kuwa nchi ya pili Bara la Afrika kuwa nayo ikitanguliwa na Afrika Kusini.

Akizungumzia hali ya saratani ya matiti, Dk. Pili alisema tathmini iliyofanyika mwaka 2017, inaonyesha idadi ya wagonjwa wapya inakadiriwa kuongezeka kutoka watu 2,732 mwaka 2012 na kufikia 4,961 mwaka 2030.

"Inakadiriwa kwamba kutakuwa na ongezeko la wagonjwa wa saratani ya matiti wapya kwa asilimia 82 Tanzania ifikapo mwaka 2030 pamoja na ongezeko la asilimia 80 la vifo vitokanavyo na satarani ya titi kwa mwaka huo," alisema.

"Saratani ya matiti ni ya pili Tanzania ikitanguliwa na saratani ya shingo ya kizazi. Kwa kuwa na mashine yenye ubora zaidi itawezesha kugundua tatizo katika hatua za awali na kupata matibabu.

"Umri ambao mtu anatakiwa kuchunguza saratani ya matiti kwa wale ambao katika familia zao hawana historia ya saratani ni kuanzia miaka 40, lakini wenye historia ya saratani ni kuanzia miaka 30, chini ya hapo haifanyiki," alisema.

Daktari Bingwa wa Radiologia, Ahmed Jusabani, alisema uboreshwaji wa huduma hiyo ni kuwasaidia Watanzania kupata matibabu kwa gharama nafuu wakiwa nchini.

Alisema uwezo wa mashine hiyo kwa siku ni kuhudumia wagonjwa 20 wakati ya awali ilikuwa na uwezo wa watano pekee.

"Kuwapo kwa mashine hii hapa nchini ni kama kichocheo, serikali iangalie iwekezekano mikoa mingine, hatuwezi kumaliza matatizo yote, mashine ambayo ilikuwa ikitoa huduma kama hiyo hapa tunaipeleka Mwanza ili ikasaidie ukanda huo," alisema.

Pia, alisema Aga Khan inatoa huduma ya kuangalia saratani ya matiti kwa watu 30 bure ambao imewaomba Ofisi ya Mganga Mkuu Mkoa wa Dar es Salaam kuratibu wanaokwenda kupata huduma hiyo.

Mratibu wa Huduma za Afya Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Daisy Majamba, akizungumza kwa niaba ya Mganga Mkuu Mkoa huo, Dk. Yudas Ndungile, aliipongeza hospitali hiyo kwa ununuzi wa mashine hiyo ya kisasa.

Mkurugenzi wa Masoko wa Taasisi ya Afya ya wanawake (GE Healthcare Africa), Maria Smith, alisema saratani ya matiti ni tatizo kubwa na linawaumiza wengi.

"Kujichunguza mapema bado linabaki kuwa jambo la msingi ambalo litapunguza ukubwa wa tatizo na maumivu kwa wanawake. Tunajivunia kushirikiana na Aga Khan ili kuleta teknolojia muhimu itakayohudumia Watanzania itakayosaidia kugundua na kupata matibabu mapema na kupunguza maumivu ya ugonjwa huu," alisema.

# TZ yasifiwa kuanzisha Mahakama ya Mafisadi

**Na Mary Geofrey**

TANZANIA imetajwa kuwa nchi pekee yenye Mahakama Kuu kitengo cha kushughulika kesi za rushwa kati ya nchi 49 wananchama wa Umoja wa Afrika ya Ushauri wa Masuala yanayohusu Rushwa (AUABC).

Hayo yalibainishwa jana na Mwenyekiti wa Bodi ya AUABC, Begoto Miarom, wakati akizungumza na waandishi wa habari katika mkutano wa wajumbe watano wa bodi hiyo kutoka nchi mbalimbali waliokuja kufanya tathmini ya kupambana na rushwa nchini.

Mkutano huo uliwakutanisha wadau wa sekta binafsi kwa lengo la kufanya tathmini ya mkataba wa kupambana na rushwa unavyotekelezwa nchini.

Alisema katika mahojiano na asasi za umma na vyombo mbalimbali vinavyotekeleza mradi huo, walibaini kuwa mkataba huo unatekelezwa vizuri nchini hasa suala la kuwa na mahakama ya wala rushwa ambayo nchi nyingine hawana.

"Tumekuja Tanzania kwa ajili ya kufanya tathmini ya jinsi nchi hii inavyotekeleza mkataba wa Umoja wa Afrika wa kuzuia na kupambana na rushwa. Katika tathmini ya awamu, yapo mambo ambayo tumeyabaini yanaofanywa na nchi katika kupambana na rushwa na mazuri tuliyoyaona tutayatolea mapendekezo yatumike katika nchi nyingine kwa sababu kila nchi ina mifumo na taratibu zake za kutekeleza mkataba huu," Miarom alisema.

Alisema kabla ya kuja nchini walipokea ripoti za nchi wanachama, kuzipitia na wanatembelea kila nchi kwa ajili ya kufanya tathmini na kwamba ripoti wataiwasilisha katika bodi hiyo.

Alisema kuhusu tathmini waliyofanya wataenda kuifanyia kazi na kutoa ripoti ambayo itawasilishwa Takukuru.

Awali, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Brigedia Jenerali, John Mbungo, alisema ni mara ya kwanza kufanyiwa tathmini ya utekelezaji wa mkataba huo.

Alisema katika tathmini waliyoanza kuifanya nchini kuanzia Septemba 9, mwaka huu, inaonyesha Tanzania imepiga hatua kubwa katika utekelezaji wa mkataba huo wa kupambana na rushwa.

INAENDELEA UK.8

BONITE BOTTLERS LIMITED

**Advertisements of Employment**

**1. Salesman**

**Qualification:**

- Applicant should be a holder of form IV/VI with Diploma in Sales and Marketing / Business Administration or any related field from recognized Institution.

**Key skills & Abilities:**

- Skills and knowledge of customer care and customer services.
- Ability and skills of route sales.
- Ability to forecast sales / load to be taken for each day to the location assigned.
- Able to work independently with minimum supervision.
- Self motivated, flexible person and a good team player.
- Ability to seek out and develop news business and maximize all possible opportunities to increase Sales.

√ **Experience** : Any experience in the same related field will be an added advantage.

**Mode of Application:**

All applications accompanied with cover letter, photocopies of certificates and CVs to be sent to undersigned address, reach him not later than 21/09/2019.

**The Managing Director,
Bonite Bottlers Ltd,
P. O. Box 1352,
MOSHI.**

21541602

# Askofu Mkuu Ruwa'ichi aanza kutembea

**Na Mary Geofrey**

SIKU tatu baada ya Muhashamu Askofu Mkuu wa Jimbo Katoliki la Dar es Salaam, Yuda Thadeus Ruwa'ichi, kufanyiwa upasuaji wa kuondoa damu iliyokuwa imevilia kwenye ubongo, ameanza kutembea na kukaa mwenyewe.

Hayo yalibainishwa na daktari wake ambaye ni Bingwa wa Upasuaji wa Ubongo, Uti wa Mgongo na Mishipa ya Fahamu wa Tasisi ya Tiba ya Mifupa (MOI), Prof. Joseph Kahamba, wakati akizungumza na Nipashe jana.

Alisema Muhashamu Askofu Ruwa'ichi ameendelea kufanya mazoezi ya kutembea mwenyewe bila shida, kusimama na kukaa kwenye kiti.

Alisema ni hali ya kawaida kwa mgonjwa aliyefanyiwa upasuaji kwenye kichwa au ubongo kukaa na kutembea ndani ya siku tatu kama ilivyo kwa Muhashamu Askofu Ruwa'ichi.

"Hali ya Baba Muhashamu Askofu Ruwa'ichi inaendelea vizuri sana, ameanza kukaa mwenyewe na kutembea. Ni hali ya kawaida kwa mgonjwa kama huyu kutembea na kukaa ndani ya siku tatu na ndio matarajio yetu madaktari ingawa kuna baadhi ya wagonjwa wanachelewa," Prof. Kahamba alisema.

Alisema pia jopo la wataalam saba wakiwamo madaktari bingwa wanne wanaendelea kumfanyia uchunguzi wa kina kiongozi huyo wa kanisa ili aweze kurejea katika hali yake ya kawaida.

Jana Ofisa Uhusiano wa MOI, Patrick Mvungi, alisema kila baada ya saa moja madaktari hao wanaingia wodini kwa ajili ya kufuatilia maendeleo ya kiongozi huyo katika kuhakikisha anarejea katika hali yake ya kawaida mapema zaidi.

"Muhashamu Askofu Ruwa'ichi anaendelea vizuri sana jopo la wataalam saba wanaomuangalia, kila asubuhi inafanyika ibada fupi na leo Askofu ameshiriki ibada hiyo akiwa amekaa mwenyewe," Mvungi alisema.

Alieleza kuwa, jopo linalomfanyia uchunguzi kiongozi huyo wa kanisa nchini ni madaktari bingwa watatu wa magonjwa Ubongo, Dawa za Usingizi na Magonjwa ya ndani. "Leo jioni (jana) watakaa kuangalia kama wamuondoe katika chumba cha uangalizi maalum (ICU) na kumuhamishia wodi za kawaida," Mvungi alisema.

**Ghrama za Matibabu**

Prof. Kahamba alisema ugonjwa huo unaofahamika kwa jina la kitaalam la 'Chronic Subdural Haematoma' gharama za kufanyiwa upasuaji nchini ni Sh. milioni nne, lakini kwenda nje ya nchi zinagharimu Sh. milioni 20.

Alisema MOI wanawafanyia upasuaji wagonjwa wawili kila wiki na takribani 100 kwa mwaka na hali zao zinakuwa nzuri.

"Ugonjwa kama huu unatibika MOI bila shida na tunafanya upasuaji kwa wagonjwa wengi hadi 100 kwa mwaka na wagonjwa wote wanapona na gharama zetu zote hadi malazi ni ndogo zinafika Sh. milioni nne, kulinganisha na nje ya nchi ambazo zinafika hadi Sh. milioni 20 kwa kila kitu," Prof. Kahamba alisema.



Watoto wakivua samaki kwa kutumia chandarua katika eneo la Songas, Kinyerezi, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kisena, mkewe wafutiwa mashtaka 4

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imewaondolea mashtaka manne ya kutakatisha fedha Mkurugenzi wa Mradi wa Mabasi yaendayo haraka jijini Dar es Salaam (Udart), Robert Kisena (46), mke wake Frorencia Mshauri maarufu Frolence Membe (43) na wenzao watatu na kubaki na tuhuma za uhujumu uchumi ikiwamo kusababisha hasara ya Sh. bilioni 2.4 kwa kampuni hiyo.

Hata hivyo, washtakiwa hao sasa wanakabiliwa na mashtaka 15 kati ya 19 ikiwamo ya kughushi, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na kuisababishia Udart hasara ya Sh. 2,414,326,260.70.

Jana mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Augustine Rwizile, ilikubali ombi la upande wa Jamhuri la kutaka kuwabadilishia washtakiwa hati ya mashtaka.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa upande wa mashtaka unawasilisha ombi kwa mahakama la kuwabadilishia washtakiwa hati ya mashtaka. Hakimu alikubaliana na ombi hilo.

Wankyo alidai kuwa katika hati mpya washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka 15.

Aliwataja washtakiwa hao mbali na Kisena wengine ni, Kulwa Kisena (33), Charles Newe (47) na Chen Shi (32).

Ilidaiwa kuwa kati ya oktoba 2012 mpaka Mei 31, 2018, washtakiwa wanadaiwa kutenda makosa hayo.

Ilidaiwa kuwa kati ya Januari Mosi, 2011 na Mei 31,2018 katika mahali tofauti wakiwa na watu wengine waliratibu shughuli za kiharifu huku wakijua kufanya hivyo ni kosa la kisheria.

Katika shtaka la pili kati ya Januari Mosi, 2015 na Desemba 31, 2017 katika eneo la Jangwani, washtakiwa hao, akiwamo Mkurugenzi wa Kampuni ya Zenon Oil Gas Limited alijenga kituo cha mafuta kinachoitwa Zenon Oil and Gas katika karakana ya Kampuni ya Udart bila ya kuwa na kibali kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma na Nishati na Maji (Ewura).

Shtaka la tatu kati ya Januari Mosi,2015 na Desemba 31, 2017 katika eneo la Jangwani jijini Dar es Salaam washtakiwa wakiwa wakurugenzi wa kampuni hiyo kwa pamoja walianzisha biashara ya kuuza mafuta ya petroli katika eneo ambalo halijaruhusiwa.

Shtaka la nne ilidaiwa kuwa kati ya Mei 25, 2015 na Desemba 31, 2016 katika Jiji la Dar es Salaam, washtakiwa Robert Charles na Frolencia wakiwa na lengo la kuficha uhalisia, waliiba mafuta yenye thamani ya Sh 1, 216,145,374 kwa kuyauza wakati wakijua ni mali ya UDART.

Katika shtaka jingine, ilidaiwa kati ya Mei 25, 2015 na Desemba 31, 2016 akiwa jijini Dar es Salaam kwa makusudi alisababishia hasara UDART ya Sh.2.414, 326, 260.70

Upande huo wa Jamhuri ulidai shtaka jingine Juni 8, 2016 katika benki ya NMB tawi la Benki House lililopo Ilala, jijini Dar es Salaam Robert na Chen walijipatia Sh. milioni 594.9 mali ya mradi huo.

Pia ilidaiwa washtakiwa wote kati ya Mei 25, 2015 na Desemba 31, 2016 walisababishia hasara ya Sh. bilioni 2.4.

Hakimu alisema washtakiwa hawatakiwi kujibu chochote kwa sababu mahakama yake haina mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi bila kibali cha Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP) au upelelezi utakapokamilika itahamishiwa Mahakama Kuu Divisheni ya Uhujumu Uchumi na Rushwa.

Kesi hiyo itatajwa Septemba 17, mwaka huu na washtakiwa wamepelekwa mahabusu.

# WB kuwezesha Watanzania mil. 5 miradi kiuchumi

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Dunia (WB) imesema zaidi ya Watanzania milioni tano nusu ya idadi hiyo ikiwa wanawake wanatarajia kunufaika na mradi wa kuziwezesha kaya maskini kuboresha maisha yao kupitia miradi na fursa za kiuchumi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na WB, awamu ya pili ya fedha kwa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf), iliyopitishwa na Bodi ya Wakurugenzi wa benki hiyo, utaipa zaidi ya Dola za Marekani milioni 450 (sawa na Sh. bilioni 1).

Fedha hizo zinatolewa ikiwa ni awamu ya pili ya mradi wa Productive Social Safety Net Project (PSSN II) chini ya mradi unaotekelezwa na Tasaf kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa chakula na maisha ya kaya, kuongeza idadi ya watoto wanaokwenda shule za msingi na huduma za afya.

Pia, fedha hizo zitaboresha na kuongeza idadi ya wanafunzi wanaoendelea na masomo ya sekondari.

"Tanzania iko katika hatua za awali za utekelezaji wa mradi wa kaya maskini kuwasaidia wanaufaika kuhifadhi fedha na kupata bidhaa, imesaidia wengi kuwa na akiba ya chakula, kupata elimu na huduma za afya. Msaada huu ni muhimu kwa kuwa umesaidia eneo kubwa la uboreshaji wa maisha ya watu na kuongeza ujuzi na kumudu mazingira ambayo bado iko chini ya asilimia 0.40," alisema Mkurugenzi Mkazi wa WB, Bella Bird.

"Tutaendelea kufanyakazi na serikali kwa kuhusisha wananchi na wadau wengine kwenye masuala ya maendeleo yanayowahusu watu moja kwa moja na nchi kwa ujumla."

Alisema, Tanzania imefanikiwa kutekeleza mradi wa mfano wa kutoa fedha kwenye kaya maskini tangu mwaka 2009 hadi 2012 kwa wilaya tatu nchini.

Mwaka 2012, serikali ilianza kutekeleza mradi huo na kufanikiwa kuzifikia kaya milioni moja hadi Septemba 2015.

Vile vile, awamu ya kwanza ya PSSN ililenga asilimia 10 ya watu wanaokadiriwa kuwa ni 650,000 wanaoishi chini ya mstari wa umaskini huku 350,000 wakiwa kwenye hatari ya kushuka kwenye mstari huo kutokana na mabadiliko ya kiuchumi.

Bird alisema lengo la awamu ya pili ya mradi huo ni kuzisaidia kaya maskini kupata fedha na fursa za huduma za kijamii na kutunza familia zao.

HABARI KITAIFA

# Misri kuwekeza Dola mil. 900

**Na Juster Prudence,** TUDARCo

KAMPUNI 22 kutoka Misri zimewekeza nchini zaidi ya Dola za Kimarekani milioni 900 (sawa na Sh. trilioni 2.068), kwa ajili ya kusaidia ukuaji wa biashara na uchumi.

Hayo yameelezwa na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, wakati wa ufunguzi wa Wiki ya Biashara ya Misri inayomalizika leo.

Alisema biashara kati ya Tanzania na Misri imekuwa kwa asilimia 75 baada ya kuingiza bidhaa mbalimbali zenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 42 (sawa na Sh. bilioni 97) ikilinganishwa na bidhaa za mwanzo zilizokuwa na thamani ya Dola za Marekani milioni 24 mwaka 2017.

Alieleza kuwa serikali itaendelea kuboresha mazingira ya biashara na kuhamasisha kampuni nyingi za Misri kuwekeza nchini kwa lengo la kudumisha uhusiano wa kibiashara baina ya nchi hizo mbili na kusema sekta binafsi zimekuwa na mchango mkubwa katika suala la biashara na uwekezaji na kusaidia kukuza uchumi.

Mwinyi alisema ni fursa kwa wafanyabiashara wa Tanzania kufanya mazungumzo na wafanyabiashara wa Misri ili kuboresha ushirikiano wa kibiashara baina ya nchi hizo mbili.

Naye Rais wa Chemba ya Wafanyabiashara Tanzania (TCCIA), Paul Koyi, alisema watafanya kila wanaloweza ili biashara pamoja na uwekezaji viweze kuongezeka na kufikia Tanzania ya viwanda kwa vitendo.

Alibainisha kuwapo na mazungumzo yanayoendelea baina yao na hivyo makubaliano yatawekwa na yatakapokuwa tayari nyaraka zitasainiwa ili kuanzisha kiwanda cha dawa nchini Tanzania.




Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Vijana la Tanzania Youth Alliance (TAYOA), Balozi Charles Sanga (wa tatu kushoto) na Mkurungezi Peter Masika (wa tatu kulia), wakikata utepe kuzindua mradi wa kuendeleza vipaji vya vijana wa Vijanatz Talent Show Timiza Malengo Yako, jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari nchini. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# JPM aiomba China kiwanda cha kubangua korosho

**Na Rahma Kisilwa,** TUDARCO

RAIS John Magufuli, ameiomba Serikali ya China kujenga kiwanda cha kubangua korosho nchini ambacho kitasimamiwa na majeshi ya Tanzania na nchi hiyo.

Pia, kiwanda hicho kitaongeza thamani ya korosho na kuiwezesha China kupata bidhaa hiyo iliyobanguliwa tayari kwa matumizi.

Rais Magufuli aliyasema hayo juzi katika hafla ya makabidhiano ya magari 40 kutoka Jeshi la Ukombozi la Watu wa China (PLA).

Alisema pamoja na kuwa na uhusiano mzuri kati ya China na Tanzania, angependa uimarishwe zaidi kwa kujenga kiwanda kikubwa cha korosho nchini Tanzania kitakachosimamiwa na Jeshi la Wananchi la Tanzania (JWTZ) pamoja na Jeshi la China (PLA).

"Ni vizuri pajengwe kiwanda kikubwa cha korosho ambacho kitakuwa kinasimamiwa na majeshi haya mawili ili korosho zitakapomalizika kutengenezwa kule Lindi, basi zipelekwe moja kwa moja zikaliwe na wanajeshi wa China, badala ya Wachina kusubiri korosho kutoka nchi nyingine kama India au Vietinam ambao nao wamezifuata kutoka Tanzania," alisema Rais.

Alisema ni vyema kiwanda hicho kijengwe na kuwa na uwezo wa kubangua tani 200,000 za korosho kwa mwaka.

# Rita yatoa upendeleo vyeti wenye ulemavu

**Na Mary Geofrey**

WAKALA wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (Rita), umewataka watu wenye uhitaji maalum, kujitokeza katika ofisi zao kupata huduma muhimu ikiwamo cheti cha kuzaliwa, vizazi na vifo, wosia, udhamini.

Makundi hayo ni pamoja watu wenye ulemavu wa viungo, wakiwamo wasioona, wa miguu, wenye watoto, wajawazito, wazee ambao watatengewa dawati lao kwa ajili ya kuwahudumia.

Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa Rita, Emmy Hudson, aliyasema hayo jijini Dar es Salaam, baada ya kutoa hundi ya Sh. milioni moja, kwa Chama cha Wasiiona cha Mkoa wa Dar es Salaam na kueleza kuwa wanatoa huduma hizo kupitia dirisha maalum walilolianzisha.

"Kwa sasa ofisi yetu imeweka dawati maalum la kuhudumia watu hawa na wito wetu tunawaomba wasijifiche na kukosa huduma badala yake wajitokeze na sisi tupo tayari kuwahudumia," Emmy alisema.

Alisema fedha walizowasaidia ni kwa ajili ya udhamini wa chama hicho kwenda kwenye maonyesho ya siku ya fimbo nyeupe ambayo kimataifa yatafanyika Oktoba 10 mpaka 15, mkoani Kigoma.

"Watu wa makundi maalum nao wanahitaji kupata huduma zetu na tumekuwa tunatoa elimu mbalimbali kwa jamii kwamba hata watu hao wanahitaji cheti cha kuzaliwa, kuandika wosia na hata kuanzisha taasisi zao kwa kufuata sheria mbalimbali za udhamini katika ofisi yetu," Emmy alisema.

Alisema ofisi ya Rita itafika Kigoma kwa ajili ya kutoa elimu hiyo kwa wenye makundi maalum ili waweze kupata huduma kama ambavyo wamekuwa wakipata wananchi wengine.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa chama hicho, Paul Mathias, aliishukuru Rita kusikia kilio cha kuomba udhamini huku akiziomba taasisi nyingine kufanya hivyo ili kufanikisha safari yao ya kwenda Kigoma.

Hata hivyo, alizitaka jamii kutoacha kuficha watoto wenye ulemavu ndani ili waweze kupata huduma mbalimbali za kijamii.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kila la kheri Yanga, Azam michuano ya CAF

**KWANZA** kabisa Nipashe linaanza kutoa pongezi kwa wachezaji na benchi la ufundi la Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), ambalo wiki iliyopita lilifanikiwa kuwafunga wapinzani wao Burundi maarufu Intamba Murugamba.

Taifa Stars iliwaondoa majirani hao na kutinga hatua ya makundi ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia zitakazochezwa mwaka 2022 huko nchini Qatar.

Pia pongezi zingine zinatakiwa kwenda kwa mashabiki waliojitokeza kushuhudia mchezo huo ambao ndani ya dakika 120, timu hizo zilikuwa sare ya mabao 2-2 na kulazimika kwenda kwenye penalti na hapo, Taifa Stars ndipo waliibuka kidedea kwa kupata ushindi wa mabao 3-0.

Tukirudi katika ngazi ya klabu, leo wawakilishi pekee wa Tanzania Bara katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Yanga, wanatarajia kushuka uwanjani kuwakaribisha wapinzani wao, Zesco kutoka Zambia.

Mechi hiyo ni ya kwanza ya raundi ya kwanza ya michuano hiyo na Yanga ambayo ilirejea kwenye michuano hiyo kupitia mafanikio waliyofikia watani zao, Simba msimu uliopita, wanahitaji kupata ushindi ili kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kusonga mbele.

Yanga inatakiwa kucheza kwa nguvu zote na kutowadharau wapinzani wao, kwa sababu nao wamekuja hapa nchini kwa lengo moja la kupata matokeo chanya.

Nipashe linawakumbusha Yanga kupambana ili wapate ushindi katika mechi ya leo, na hapo watakuwa wamejiweka kwenye nafasi nzuri ya kwenda kukamiliza kibarua walichokianza mjini Lusaka katika mchezo wa marudiano.

Hakuna kisichowezekana, na mcheza kwao hutuzwa, wachezaji na viongozi wa Yanga wanatakiwa kuendelea kujiimarisha na kutoruhusu sababu nyingine kuwavuruga katika kipindi hiki cha mapambano walichonacho.

Kufanya vema kwa Yanga katika mchezo wa leo na mingine itakayofuata, kunaweza kuifanya tena Tanzania Bara kutoa wawakilishi wanne kwenye michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), na kuifanya bendera ya nchi kupepea zaidi.

Mbali na Yanga ambayo sasa iko chini ya Mkongomani Mwinyi Zahera, Nipashe pia linawaombea dua njema na yenye mafanikio wawakilishi wengine wa Bara katika mashindano ya kimataifa ni Azam FC.

Matajiri hao wa Chamazi, wao watashusha karata yao kesho Jumapili kuvaana na Triangle United ya Zimbabwe kwenye mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika. Ni mechi muhimu kwa mabingwa hao wa zamani wa Kombe la Kagame.

Endapo Azam itapata ushindi, itakuwa imetanguliza hatua moja mbele na itakapofika ugenini, itatakiwa kukamilisha kibarua ilichokianza hapa nyumbani. Huu ni wakati wa wachezaji wa Tanzania kujitangaza.


Klabu inapofanya vema kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho, inaweka "sokoni" wachezaji wake na hivyo mawakala mbalimbali hujitokeza kuwafuatilia na wale wanaopata bahati ya kusajiliwa, baadaye hurejea nchini wakiwa imara zaidi na kuisaidia Taifa Stars kupata matokeo bora kwenye michuano itakayoshiriki.

Tuache ubaguzi wa kushangilia wageni, huu ni wakati wa kuwa pamoja na Yanga, Azam FC na Malindi ya Zanzibar ambao kesho watakaribisha Al Masry kutoka Misri kwenye mchezo mwingine wa Kombe la Shirikisho.

Nipashe linazitakia mafanikio Yanga, Azam FC na Malindi katika mechi zao za kimataifa. Kila la kheri Tanzania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Yanga, Vodacom nani ana haki?

Na Barnabas Maro

**YANGA** ni klabu ya kandanda iliyoanzishwa mwaka 1935 jijini Dar es Salaam. Ina wanachama na mashabiki mbalimbali wanaoipenda timu hiyo lakini inaishi kwa matumaini ikitegemea misaada!

Tangu tajiri aliyekuwa mfadhili wao kujiondoa, wachezaji wamekuwa wakiishi maisha ya mashaka (matatizo au masahibu yanayompata mtu katika maisha). Kadhia (tukio la kuhuzunisha) hiyo imewafanya baadhi yao waikimbie ili kutafuta maisha kwingine huku wakiendelea kudai fedha za usajili na mishahara yao ya nyuma.

Klabu hiyo yatambulika kwa jezi zao za rangi ya kijani, njano na nyeusi. Haikubali kupewa jezi zenye rangi tofauti, hasa nyekundu inayotumiwa na watani zao, Simba ambao ndio wapinzani wao wakuu katika kabumbu nchini.

Vodacom ni kampuni ya simu za mkononi yenye nembo nyeupe na nyekundu kama ilivyo Simba. Kampuni hiyo imeingia mkataba wa kuidhamini tena Ligi Kuu Tanzania Bara kama ilivyokuwa mwaka 2012 lakini kwa masharti ya kutobadilisha rangi za nembo yake.

Kirumbizi (ngoma inayochezwa na wachezaji inayohusisha kupigana kwa fimbo) kinaanzia hapa. Msimamo wa Yanga ni kama kumwambia Muislamu anayeishika dini yake sawasawa ale nyama ya nguruwe ili umsaidie! Kwake ni haramu na kufuru, kwani ni jambo lisiloruhusiwa kabisa.

Yanga na ufukara wake wa kujitakia, yasema haitaruhusu rangi tofauti katika jezi zake yaani kijani, njano na nyeusi. Kampuni ya Vodacom iliyotia saini (sio 'sahihi') kuidhamini Ligi Kuu Tanzania Bara, nayo inasimamia nembo yake.

Kwa mvutano huu wa Yanga na Vodacom atakayeumia ni nani? Hebu tusome methali zifuatazo:

"Wakati wa hatari kila mtu huililia roho yake." Maana yake hatari inapotokea kila mtu huitapia (kitendo cha kuwania kitu kwa pupa) roho yake au hutamani kujiokoa yeye tu.

**Yanga na ufukara wake wa kujitakia, yasema haitaruhusu rangi tofauti katika jezi zake yaani kijani, njano na nyeusi. Kampuni ya Vodacom iliyotia saini (sio 'sahihi') kuidhamini Ligi Kuu Tanzania Bara, nayo inasimamia nembo yake.**

Tuangalie methali nyingine: "Waja uma kumi usipate hata kimoja." Maana yake utaishia kuviuma vyanda au vidole vyako kumi kwa majuto na uchungu usipate hata kitu kimoja.

Methali hii hutumiwa kwa mtu anayepewa ushauri unaoweza kumfaa kisha akaupuuza na kuishia kufikwa na majuto ya kutoambulia kitu katika jambo alilokuwa akilifanya.

Nembo ya kampuni haimaanishi kutoa rangi za klabu ya Yanga, hasha! (sivyo kabisa). Nembo huwepo sehemu fulani tu ya jezi za wachezaji bila kuathiri rangi za klabu husika.

Yaonyesha kuwa kampuni yenye nembo hiyo ndio inayoidhamini timu husika yaani Young African Sports Club ambayo kwa ufupi yaitwa Yanga na sasa yaitwa 'timu ya wananchi.' Kwani timu zingine si za wananchi?

Yanga yapaswa kuamua moja kati ya mawili: Kukubali nembo ya Vodacom kwenye jezi zake ili ipate msaada wa kampuni hiyo au ikatae na kukosa msaada wa Vodacom.

Ipi yenye ubavu kati ya Yanga na Vodacom? Nionavyo, Vodacom imetulia tuli (bila ya kutikisika) kusubiri jibu la Yanga kupitia Shirikisho la Soka Tanzania (TFF). Vodacom ilivyotulia, ni kama chatu anavyotulia na kupepesa (fanya kope za macho zicheze kwa kuzipeleka juu chini) ili kuvuta windo lake.

Viongozi wa Yanga wanapaswa kutambua kuwa kukataa nembo ya Vodacom hakutaiathiri kampuni hiyo kwani vilabu vyote vinavyoshiriki Ligi Kuu vitaitumia kwenye jezi zao huku vikipata mgao wa fedha za Vodacom. Kati ya Yanga na Vodacom mkosa atakuwa nani?

Ushauri wa mwisho kwa Yanga: "Masikini hapiki kombe (la wali) mpaka mwaka wa mavuno." Maana yake masikini hawezi kuandaa sahani kubwa la wali hadi wakati wa mavuno.

Yanga, "halahala* mti na macho." Ijitunze au ijiangalie isijitie kijiti machoni. Hii ni methali ya kumpigia mfano mtu anayefanya mambo yake bila kuwa na uangalifu.

***marobarnabas@yahoo.com***
***0784 334 096***

## HABARI BUNGE

# Kamati ulinzi zapewa rungu wakiukaji matumizi

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Josephat Kandege, amesema imeziagiza kamati za ulinzi na usalama za mikoa na wilaya kuchukua hatua stahiki pale inapobainika ukiukwaji wa matumizi ya ardhi kwenye eneo la hifadhi.

Akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum(CCM), Martha Umbulla, alisema mwaka 2012 mahakama ilitoa hukumu kuwa wakulima na wafugaji wote kuondoka ndani ya hifadhi ya jamii ya Emborley Murtangos iliyopo kiteto. Hata hivyo, alisema baadhi ya wananchi walipinga amri hiyo na kuendelea kufanya shughuli zao hivyo kuzua mgogoro baina ya wakulima na wafugaji.

Mbunge huyo alihoji serikali imeshughulikia kwa kiasi gani mgogoro huo uliodumu kwa miaka minane, hatua zilizochukuliwa kuwadhibiti na kuwaadhibu waliokiuka amri hiyo na kauli ya serikali juu ya matumizi ya hifadhi hiyo ili kumaliza mgogoro.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri huyo alisema eneo la hifadhi hiyo litabaki kuwa la hifadhi ya jamii kwa kuzingatia mpango wa matumizi ya ardhi kama ulivyoainishwa kwa kuzingatia maamuzi ya Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani.


Alisema hali ya ulinzi na usalama katika eneo hilo itaendelea kuimarishwa ili kuhakikisha panakuwapo amani na utulivu wakati wote.

Hata hivyo, aliagiza kamati za ulinzi na usalama za mikoa na wilaya kuchukua hatua stahiki pale inapobainika ukiukwaji wa matumizi ya ardhi kwenye eneo la hifadhi.

Alifafanua kuwa mwaka 2014/15 serikali iliunda kikosi kazi cha wataalam kutoka Ofisi ya Rais-Tamisemi, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Fedha na Mipango (Ofisi ya Taifa Takwimu), Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Manyara na Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto kwa lengo la kuhakiki mipaka ya hifadhi.

Alisema serikali imeendelea kuwaondoa wananchi na makundi ya wakulima na wafugaji wanaoendelea kuingia kwenye hifadhi.

# Mbunge ahofu kiwango ubanguaji korosho




Habari na Augusta Njoji

MBUNGE wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota, amesema kiwango cha ubanguaji korosho ni kidogo ikilinganishwa na mavuno kwa mwaka husika.

Akiuliza swali la nyongeza jana bungeni, Chikota alisema kiwango cha ubanguaji kwa mwaka ni tani 50,000 ambacho ni kidogo huku kukiwapo na mavuno mengi.

"Kwa mfano mwaka 2017/18 Tanzania tulifikisha mavuno ya korosho tani 312,000, kwa hiyo kiwango kinachobanguliwa ni kidogo sana,"alisema.

Alihoji kwa kuwa Mkoa wa Lindi na Mtwara imetenga maeneo ya uwekezaji kwa ajili ya viwanda vya korosho serikali itatoa kivutio maalum ikiwamo kufuta baadhi ya kodi ili waje mikoa wa Lindi na Mtwara kuwekeza viwanda vipya vya korosho.

Pia alihoji badala ya mkulima wa korosho kudhaminiwa na chama chake cha ushirika, serikali ya kijiji na Mkurugenzi ina mpango gani wa kuondoa mlolongo huo na kuwaacha kudhaminiwa na chama ili kupata pembejeo.

Katika swali lake la msingi, Chikota alihoji viwanda vilivyopo nchini vina uwezo wa kubangua korosho kiasi gani na serikali ina mpango gani wa kuongeza ubanguaji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Stella Manyanya, alisema kwasasa Tanzania ina jumla ya viwanda vikubwa, vya kati na vidogo vya kubangua korosho 34, vikubwa na vya kati ni 18 na vidogo ni 16.

Alisema viwanda 18 vikubwa na vya kati vina uwezo uliosimikwa wa kubangua tani 63,400 kwa mwaka na 13 kati yake vinafanya kazi.

"Viwanda vidogo ni 16 kati ya hivyo tisa vinafanya kazi na vina uwezo wa kubangua tani 9,610 kwa mwaka,"alisema.

Alibainisha kuwa viwanda vyote 34 vya korosho vina jumla ya uwezo uliosimikwa wa kubangua tani tani 73,010 kwa mwaka na uwezo unaotumika kwasasa ni tani zisizozidi 50,000.

Alisema kuwa serikali imehamasisha sekta binafsi kuanzisha viwanda vya kubangua korosho na imefanikiwa kuwabadilisha wafanyabiashara wakubwa watatu wa kuuza korosho ghafi kujenga viwanda vya kubangua korosho.

Aliwataja wafanyabiashara hao kuwa ni Al andalus Company, Mnazi Mmoja Lindi, Mkemi Agrix Company na Fuzzy International Company vyote vya Mkuranga, mkoani Pwani.

Pamoja na jitihada hizo, alisema wamefanikiwa kupata mwekezaji mmoja ambaye kiwanda chake kiliwekwa jiwe la msingi na rais mwezi Aprili 2019.

"Kiwanda hicho kinatarajia kuanza kubangua tani 6,000 na kitaendelea na kuongeza uwezo wake mpaka kufikia tani 10,000 kwa mwaka na kitakuwa chenye teknolojia ya kisasa na kinatarajiwa kutoa ajira 250,"alisema.

Kadhalika, alisema serikali imekuwa ikiweka vivutio kwa wawekezaji hasa kwa viwanda vyote vyenye malighafi zinazozalishwa nchini na hivi karibuni kuna kodi zimeondolewa ili kuhakikisha viwanda hivyo vinaweza kufanya kazi.

Alisema kwa viwanda ambavyo kwasasa havibangui korosho vinaunganishwa na wawekezaji wengine ili viweze kufanya kazi na kuongeza ubanguaji.

"Kuhusu suala lake la pembejeo mawazo yake tunayachukua na tutayafanyia kazi," alisema Manyanya.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akizindua mfumo wa uendeshaji Bunge kidigitali, katika ukumbi wa Msekwa, bungeni jijini Dodoma, juzi. Wanaoshuhudia ni Spika wa Bunge, Job Ndugai (kushoto), Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (wapili kulia), na Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania (TWPG), Margaret Sitta. **PICHA: OWM**

# Uhaba mahabusu kikwazo kutenganisha umri wahalifu

SERIKALI imesema suala la kuwatenganisha wahalifu kwa kuzingatia vigezo vya umri, kosa na kifungo, limekuwa halizingatiwi gerezani kutokana na kuwapo na msongamano wa mahabusi na uhaba wa mabweni.

Kutokana na uhaba huo, mahabusi na wafungwa wamekuwa wakichanganywa.

Kauli hiyo ilitolewa jana bungeni na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Hamad Yusuf Masauni, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Najma Murtaza Giga.

Alihoji utaratibu wa kuweka pamoja watuhumiwa wenye makosa tofauti kama vile wizi wa kuku au mazao, mauaji, ujambazi sugu na ubakaji ni taratibu wa kawaida katika magereza na mahabusu hapa nchini, hali kadhalika kwa wafungwa wenye rika tofauti.

Pia alihoji kuwaweka pamoja wafungwa na watuhumiwa hao ni hali hatarishi kwa mustakabali wa maisha yao ya baadaye.

"Je, serikali haioni inapoteza nguvu kazi ya vijana wetu kwa kuwachanganya pamoja na wale wabakaji hususan vijana wa kuanzia umri wa miaka 18 hadi 30," alihoji.

Akijibu maswali hayo, Masauni alikiri kuwa baadhi ya magereza nchini hususan yenye mahabusu, suala la kuwatenganisha wahalifu kwa kuzingatia vigezo vya umri, kosa na kifungo limekuwa halizingatiwi.

Alisema hali hiyo inatokana na sababu ya msongamano wa mahabusu na uhaba wa mabweni na hivyo kusababisha kuchanganywa na wafungwa.

Hata hivyo, alisema katika kukabiliana na hali hiyo, serikali imeshachukua hatua mbalimbali ikiwamo kujenga magereza katika wilaya ambazo hazina.

Pia kufanya upanuzi na kujenga mabweni kwenye magereza na kutoa elimu kwa wahalifu juu ya madhara hasi ya vitendo vya uhalifu katika jamii na kutojihusisha na vitendo hivyo.

Alifafanua kuwa kitendo cha wahalifu wa aina mbalimbali kuwamo magerezani au kuchanganywa hakuhalalishi wao kuendelea na vitendo vyao vya uhalifu kwa kuwa zipo sheria, kanuni na taratibu za magereza zinakataza na zinatoa adhabu kwa mhalifu atakayebainika kufanya vitendo hivyo gerezani.

"Mathalani Kanuni ya Makosa Gerezani ya mwaka 1967, imeainisha makosa mbalimbali ambayo mhalifu hapaswi kuyafanya akiwa gerezani, na hatua za kuchukua na adhabu endapo itabainika amatenda kinyume," alisema.

Aliwataka wahalifu kutambua kuwa wanapaswa wajirekebishe kwa kuachana na tabia ya kufanya vitendo vya uhalifu na pia serikali inathamini na kulinda nguvu kazi yao.

# TPSF yaiomba serikali kuridhia azimio soko huru

**Na Romana Mallya**

TAASISI ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), imeiomba serikali kuridhia mkataba wa Azimio la Soko Huru la Bara la Afrika (CFTA), ambao wanaamini utajenga uchumi wa viwanda, kutoa ajira kwa vijana na kuongeza uzalishaji ambao utaleta ushindani duniani.

Mwenyekiti Mtendaji wa Kampuni ya Infotech Investment Group, Ali Mufuruki, akieleza umuhimu wa Tanzania kuazimia, alisema mwaka jana iliungana na nchi nyingine 44 kuusaini, lakini baada ya hapo haikuendelea na hatua zinazofuata.

"Hatua iliyofuata ni kuridhia ili Tanzania iweze kushiriki kikamilifu. Pamoja na kwamba hatujasaini, lakini kuanzia Julai Mosi kwa makubaliano waliyokuwa wameshayafanya wakuu wa nchi za Afrika kupitia Umoja wa Afrika, huo ndio mkataba rasmi wa biashara Afrika.

Hata hivyo, alisema sehemu kubwa iliyofanywa na viongozi wa siasa wakiwamo marais imeshafanyika kwa kipindi cha miaka mitano na CFTA ni eneo la biashara huru ya kwanza kuliko zote duniani kwa nchi ambazo zinashiriki.

"Kazi iliyobaki ni ya kimkakati ambayo inabidi isukumwe zaidi na sekta binafsi kwa sababu nchi hazifanyi biashara, wanaofanya ni watu na kampuni," alisema.

"TPSF wana kazi kubwa kuhakikisha wanalishikia bango suala hili na kuzungumza tena na viongozi wa kisiasa kuhusu umuhimu wa Tanzania kuwa mwanachama. "Nchi zinazotuzunguka zimesharidhia mfano Kenya, Uganda na Rwanda tumebaki Tanzania na Burundi, zipo nchi ndogo za Afrika zimeshajiunga na nchi kubwa Nigeria, Afrika Kusini na Misri nazo zimeshajiunga."

Akielezea fursa za CFTA, Mufuruki alisema Tanzania ina tatizo kubwa la ajira, zaidi ya asilimia 80 ni vijana, lakini hawana kazi, hivyo kwa soko hilo zitapatikana viwandani.

"Nchi zilizoendelea wamefanikiwa kwa sababu ya kujenga uchumi wa viwanda ambao Tanzania na nchi nyingine Afrika zimeamua kuelekea huko, kwa hiyo ni muhimu baada ya miaka michache tunataka mtu akienda dukani akutane na nguo iliyotengenezwa Tanzania au kutoka nchi za Afrika siyo China tena," alisema.

Kuhusu biashara ya anga, Mufuruki alisema wanaosafiri kwa kutumia usafiri huo Afrika wanalipa gharama mara nne ya ile inayolipwa maeneo mengine duniani.

"Moja ya sababu kulipa gharama kubwa, tunabeba gharama kubwa ya utengenezaji wa ndege, ununuzi wa mafuta ya ndege na uendeshaji wa mashirika. Wenzetu kwa kushirikiana wameweza kupunguza gharama hizi," alisema.

Mufuruki alisema kama Afrika wakiamua kushirikiana zipo huduma nyingi zinaweza kufanyika ndani ya bara hilo.

"Hakuna nchi moja ambayo itaweza kuzalisha marubani wa ndege au itatengeneza ndege zake zikiharibika au kuzifanyia bima peke yake. Tukishirikiana tutapunguza hizo gharama za sasa," alisema.

Pia alisema hakuna kipya kinachokuja kupitia CFTA kuhusu usalama wa taifa kwa sababu kama ni biashara zinafanyika.

"Mbona hatulalamiki makontena yanayokuja kutoka China kila siku kama yanatishia usalama wa taifa, yaani usalama wa taifa utatishiwa kama kontena litatoka Rwanda au Sudan," alihoji.

Naye, Mkurugenzi Mtendaji wa TPSF, Godfrey Simbeye alisema wamekutana kujadili Azimio la Afrika la kuanzisha soko huru na kuangalia kwanini Tanzania mpaka sasa hawajaridhia.

"Huu ni mwanzo wa majadiliano na yataendelea nchi nzima ili tuwe na uelewa wa kutosha kuhusiana na soko hili linalokuja ambalo litaanza mwezi Julai 2020. Tunajadili je, tusipojiunga tuna mbadala wa soko au tutafanya biashara na nani kisha tutatoa msimamo wa kuishauri serikali namna ya kuharakisha kuridhia," alisema.

Alisema kwa upande wa serikali imewaeleza kuwa bado inafanya tathmini ya faida na hasara zake kuingia kwenye soko hilo.

"Tunadhani zipo faida nyingi za sisi kujiunga kuliko kutofanya hivyo, Julai mwaka huu soko limeshapitishwa kwa hiyo kama umeridhia ama hujaridhia soko. Sekta binafsi lazima tushiriki hili soko, ni vizuri tujadili namna ya kujiandaa wakati serikali ikifanya tathmini yake," alisema.

Alisema Tanzania kwenye soko la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (Sadc) lenye watu karibu milioni 400, inauza bidhaa dola milioni 800 kwa mwaka.

"Ukubwa wa soko ndio ubora na uwezo wa kuwa na utajiri wa kutosha kwa sababu utaweza kuuza. Kuna faida kubwa kwa mfanyabiashara na mzalishaji kwamba bidhaa zake zitakwenda kwenye soko kubwa. Tanzania tusiogope, Afrika Kusini inauza kidogo sana kwetu sasa tunaogopa nini twende tukapambane," alisema.



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Ilala, Ubaya Chuma (kulia), akizungumza na wajumbe wa kamati za siasa za wilaya hiyo na matawi ya chama hicho, katika maandalizi ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa, katika Kata ya Liwiti, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MUHIDINI MSAMBA**

# Uvuvi haramu tishio idadi ya samaki

**Na Enock Charles**

LICHA ya jitihada za serikali kupambana na uvuvi haramu, samaki wanaendelea kupungua huku mahitaji ya walaji yakiongezeka.

Akizungumza jana na wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari jijini Dar es Salaam jana, Katibu Mkuu wa Sekta ya Uvuvi kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Rashid Tamatama, alisema ongezeko la walaji ni kubwa kuliko la samaki.

"Kiasi cha samaki wavuliwao kwa mwaka kimebakia kuwa kati ya tani 350,000 na 400,000 kwa mwaka toka miaka ya 90, lakini watu wameongezeka kutoka milioni 25 mpaka milioni 55 hali hii imeshusha kiasi cha samaki kiliwacho na mtu kwa mwaka kutoka kilo 14 miaka ya 90 hadi kilo nane mwaka 2019," alisema Dk. Tamatama.

Alisema katika kuimarisha rasilimali za uvuvi, serikali imeandaa na kutekeleza mkakati wa usimamizi na udhibiti wake ili kuongeza ufanisi katika usimamizi, ulinzi, uendelezaji na uhifadhi wa rasilimali za uvuvi pamoja na kudhibiti biashara haramu.

Kuhusu tani 2,803,000 za samaki waliopo katika maji nchini, alisema tani 2,210,000 zinapatikana katika Ziwa Victoria , 295,000 Ziwa Tanganyika, 168,000 Ziwa Nyasa, maziwa ya kati madogo, mito na mabwawa tani 30,000 na maji ya kitaifa ya Bahari ya Hindi tani 100,000.

Katika hatua nyingine, alisema serikali inafanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa bandari ya uvuvi nchini ikiwamo kufufua Shirika la Uvuvi Tanzania (Tafico) ili kuimarisha uwekezaji katika sekta hiyo.

Alisema serikali itaendelea kuwasiliana na wadau mbalimbali wa maendeleo ili kununua meli mbili za uvuvi, kukarabati miundombinu Tafico.

Vile vile, alisema serikali imefanikiwa kupata Yen za Japan mil. 200 (Sh. bilioni 4.2) kwa ajili ya ununuzi meli ya uvuvi ili kuvua samaki bahari kuu.

# TZ yasifiwa kuanzisha Mahakama ya Mafisadi

INATOKA UK.3

Alisema Tanzania ilisaini mkataba huo Julai mwaka 2003 na Takukuru kwa upande wa Tanzania Bara na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (Zaeca) wa Tanzania Visiwani na kutelezwa na baadhi ya taasisi.

Alitaja malengo wanayotekeleza ni kukuza na kuimarisha mifumo ya uzuiaji, uchunguzi, utoaji wa adhabu pamoja na kutokomeza rushwa katika nchi wananchama.

Alisema pia ni kukuza ushirikiano kati ya nchi wanachama ili kuhakikisha mifumo ya ushughulikiaji wa kero ya rushwa inatekelezeka.

Mbungo alisema pia wanaratibu sera na mifumo ya kisheria ya kuzuia na kupambana na rushwa kati ya nchi wananchama na kukuza maendeleo ya jamii na kiuchumi kwa kuondoa vikwazo katika shughuli za kiuchumi, kijamii, kiutamaduni zikiwamo za kisiasa.

Alisema pia ni kuweka miundombinu ya kukuza uwazi na uwajibikaji katika kusimamia shughuli za umma.

# Serikali yamuonya Musiba

INATOKA UK.2

Musiba

Katika ukurasa wake wa Tweeter, Musiba aliandika: "Namuomba Kangi Lugola aanze kumsaka (akiwataja watu wawili) kwanza kutokana na matusi na upotoshaji wake kwa serikali yetu, badala ya kuniziba mdomo mimi ambaye ni mtetezi wa nchi dhidi ya vibaraka. Nampenda rais wangu, naipenda nchi yangu."

"Lugola (pichani) aache kutumia serikali kutaka kunidhibiti kwa sababu ni waziri. Nimezaliwa siku moja, nitakufa siku moja na hizo jela wameumbiwa watu, kama anataka aje anikamate tu akaniweke. Anataka kuniziba mdomo kisa nimetoa msaada jimboni kwake sitakubali."



# Taasisi yasaidia Bakwata gari

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

KATIKA juhudi za kuchangia maendeleo pamoja na masuala ya maendeleo ya dini, taasisi ya Leopard Foundation ya jijini Arusha, imetoa msaada wa gari kwa Sheikh Mkuu wa Mkoa wa Arusha.

Gari hilo lenye thamani ya Sh.milioni 16 limetolewa kwa ajili ya kurahisisha shughuli za kidini katika ofisi ya Baraza Kuu la Waislamu (Bakwata) mkoani Arusha.

Lilikabidhiwa jana katika hafla iliyofanyika ofisini kwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo na kuhudhuriwa na Gambo, Shekhe Mkuu wa Tanzania Mufti Abubakari Zuberi na viongozi mbalimbali wa chama na serikali.

Mkurugenzi wa Leonard Foundation , Zuher Fazal, akikabidhi gari hilo, alisema kuwa taasisi yake imekuwa na utaratibu wa kusaidia jamii katika nyanja mbalimbali na awamu hii imetoa gari hilo kwa Sheikh Mkuu wa Mkoa baada ya kupata taarifa juu ya changamoto ya usafiri inayomkabili sheikh huyo.

Mufti Mkuu wa Tanzania, Sheikh Abubakari Zuberi, alishukuru kwa msaada huo wa gari litakalosaidia kufika eneo la tukio kwa wakati katika kutangaza dini na kutoa rai kwa watu wengine wenye uwezo kusaidia kutatua changamoto mbalimbali za dini.

"Tunashukuru kwa msaada huu kwani utarahisisha viongozi wa dini kufika kila mahali kwa wakati"alisema Mufti.

Sheikh wa Mkoa wa Arusha, Sheikh Shabani Juma, alishukuru kwa msaada wa gari hilo akisema litasaidia kutoa huduma mbalimbali za dini pamoja na shughuli nyingine za Bakwata.

Alisisitiza kuwa gari hilo litasaidia kutoa huduma katika maeneo mbalimbali na kutumiwa kwa kazi za viongozi wengine wa dini.

Awali Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, alishukuru kwa taasisi hiyo kutoa msaada huo kwa viongozi wa dini na kuongeza kuwa inasaidia jamii kutatua kero mbalimbali za wananchi.

"Taasisi hii kwa muda imekuwa ikitoa msaada kwa jamii ikiwamo ujenzi wa madarasa na msikiti na awamu ijayo tutaangalia waweze kusaidia na madhehebu ya Kikristo,"alisema Gambo.

# Waambiwa fursa ziko kwenye nafaka

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

VIJANA mkoani Arusha wametakiwa kuongezea mazao thamani hasa nafaka na kuyauza katika soko la Afrika Mashariki.

Aidha, wamehimizwa kuchangamkia fursa za masoko ya ndani na nje ya nchi za Afrika Mashariki ambako kuna uhitaji mkubwa wa bidhaa za chakula lengo likiwa ni kuongeza kipato na kupanua wigo wa ajira nchini.

Ofisa Vijana na Maendeleo Jiji la Arusha, Hanifa Ramadhani, alisema alipozungumza jana katika mkutano wa vijana kutoka asasi mbalimbali za kiraia.

Awaliwaambia vijana hao wanapaswa kusindika nafaka na kutengeneza bidhaa mbalimbali ambazo zinahitajika katika jamii, badala ya kuacha mazao ya wakulima yakiharibika kwa kukosa soko sababu ya kukosa kuongezwa thamani.

**Kazi hii mnapaswa nyie vijana mchangamkie fursa ya kuongeza thamani na kupeleka sokoni ili mpate ajira na uhakika wa kipato kitakachowainua kiuchumi.**

"Kazi hii mnapaswa nyie vijana mchangamkie fursa ya kuongeza thamani na kupeleka sokoni ili mpate ajira na uhakika wa kipato kitakachowainua kiuchumi,"alisema Hanifa.

Mratibu wa asasi ya kirai Infoy, Laurent Sabuni, alisema kuwa wamekuwa wakitoa mafunzo ya usindikaji wa bidhaa za chakula, hususan lishe pamoja na namna ya kuzifungasha bidhaa hizo kwa ubora.

Sabuni alisema kuwa vijana wanapaswa kuchangamkia fursa ya kuongeza thamani mazao na kuyafungasha katika viwango vya ubora wa hali ya juu ili yaweze kukubalika katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

"Vijana licha ya kujishughulisha na ujasiriamali pia wanapaswa kuongeza thamani ya mazao ya nafaka kama mahindi, ngano na hata mazao ya mifugo kuyachakata na kuyafungasha vizuri na kuyafikisha sokoni yakiwa katika hali nzuri ya kuvutia masoko ya ndani na nje," alisema Sabuni

Mmoja wa vijana waliopewa changamoto hiyo Fransisca Wilson, alisema, tayari wameanza kutengeneza unga wa lishe kwa kutumia nafaka, hivyo kuwasaidia kuinua kipato chao na kuchangia maendeleo katika jamii zao.

Leonard Paulo ni kijana mwingine aliyesema kuwa mwamko wa vijana katika kuongeza thamani umeongezeka huku changamoto kubwa ikiwa ni mtaji wa kuanzisha biashara zao na kununua mazao kwa mkulima pamoja na mashine za kuchakata mazao na kutengeneza bidhaa.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Nadoilchukin, Kata ya Komolo wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, wakishuhudia Shirika la ECLAT Foundation na Upendo Society yakikabidhi serikali baadhi ya miundombinu ya shule hiyo juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wadau Manyara waboresha elimu

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

ASASI za kiraia zimeiunga mkono serikali katika juhudi za kutoa elimu baada ya kujenga shule ya kisasa, madarasa na kukarabati nyumba za walimu.

Wanufaika wa mradi huo ni Kijiji cha Kimotorok kilichoko Kata ya Loiborsiret, wilayani Simanjiro, Mkoa wa Manyara.

Ujenzi huo ulifanywa na taasisi ya ECLAT Foundation ya Emboreet, umefanikisha ujenzi wa madarasa tisa na kukarabati nyumba mbili za walimu wa Shule ya Msingi Kimelok.

Aidha Shirika la ECLAT Foundation kwa kushirikiana na asasi ya Upendo Society ya nchini Ujerumani, wameikabidhi serikali jana, shule hiyo ya Kimelok pamoja na vyoo vyenye matundu 32 vyote vikigharimu zaidi ya Sh.milioni 267.

Mmoja kati ya wakazi hao, Meshak John akizungumza jana wakati wa hafla ya makabidhiano ya shule hiyo kwa serikali aliomba wadau kuunga mkono mashirika kama ECLAT Foundation kwani yamewanufaisha wananchi moja kwa moja kupitia miradi yao.

"Hakika sisi kama wananchi tunashukuru shirika kujenga na kukarabati miundombinu ya shule hii, kwani itakuwa chachu ya elimu eneo hili na wanafunzi kupenda shule sababu mazingira yanavutia,"alisema John.

Mwenyekiti wa ECLAT Foundation, Peter Toima, alisema shirika hilo limekuwa msaada kwa jamii katika sekta ya elimu, afya na kuwezesha kiuchumi vikundi vya maendeleo. Aliongeza kuwa baada ya kuikabidhi serikali shule hiyo ya msingi Kimelok, watakaibidhi shule ya Nadoilchukin ya Komolo wilayani Simanjiro na Lengijape ya Lorkisalie wilayani Monduli mkoani Arusha.

"Tunasaidiana na serikali katika kufanikisha miradi mbalimbali ya maendeleo, ili kuhakikisha jamii inanufaika kwa namna moja au nyingine," alisema Toima.

Ofisa Miradi wa ECLAT Foundation, Bakiri Angalia, alisema Sh.milioni 267 zimetumika kufanikisha miundombinu ya mradi huo wa shule ya Kimelok.

Angalia alisema madarasa tisa yamejengwa na kukarabatiwa, nyumba mbili za walimu zimejengwa na vyoo vyenye matundu 32 vimejengwa.

"Pia majiko mawili yamejengwa na mfumo na miundombinu ya kuvuna maji ya mvua umewekwa kwenye shule hiyo ya msingi Kimelok ambayo tayari imekabidhiwa kwa serikali," alisema Angalia.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Zephania Chaula, alisema Shirika la ECLAT Foundation ni mfano wa kuigwa kwa kufanikisha maendeleo kwa jamii ya eneo hilo.

"Nawasihi wenye mashirika mengine yasiyo ya kiserikali waige mfano wa ECLAT Foundation, kwani sisi hatuna ubaguzi tunashirikiana na wana maendeleo wote wanaotuunga mkono," alisema Chaula.

# Serikali kupambana wanyama hatari

Na Godfrey Mushi, MOSHI

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Profesa Adolf Mkenda, amesema wakati wowote kuanzia sasa, serikali itaanza operesheni maalum ya kupambana na wanyama hatari na waharibifu wanaovamia maeneo mbalimbali na kuleta hatari.

Akizungumza jana mjini hapa, Mkenda alisema tayari amemuagiza Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori nchini (TAWA), kuanza rasmi operesheni hiyo.

Matarajio ya sekta ya wanyamapori katika miaka 20 ijayo, yanakubaliana na Dira ya Maendeleo ya Tanzania ya Mwaka 2025 kuhusu uimarishaji endelevu wa mazingira na mageuzi ya kijamii na kiuchumi.

**Hivyo, kwa kukubali dhamana ya wanyamapori wetu tunatamka kwa dhati kwamba tutafanya kila tuwezalo kuhakikisha kwamba wajukuu wa watoto wetu watafurahia urithi huu mkubwa na wa thamani adimu.**

"Hatutaki wanyama waharibifu waendelee kuleta uharibifu huku na huko, tumesema itafanyika operesheni maalum ya kukabiliana nayo na nimeshamuagiza Dk. Msuha ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa TAWA kutekeleza haraka kazi hiyo," alisema Profesa Mkenda.

Matarajio ya sekta ya wanyamapori ni kukuza hifadhi ya uanuwai wa kibiolojia, kusimamia na kuendeleza rasilimali ya wanyamapori, kuwashirikisha wadau wote katika kuhifadhi wanyamapori na matumizi endelevu.

Yapo pia kugawana kwa usawa mafao yapatikanayo, kukuza matumizi endelevu ya rasilimali ya wanyamapori, kuinua mchango wa sekta ya wanyamapori katika Pato la Ndani la Taifa (GDP) toka kwenye asilimia mbili hadi kufikia tano na kuchangia kupunguza umaskini na kuinua hali za maisha ya watu wa Tanzania.

Pia, kuna masuala ya kukuza ubadilishanaji wa taarifa na utaalamu unaohusika, kitaifa, kikanda na kimataifa.

Alipotafutwa kuzungumzia operesheni hiyo, Dk. Msuha alisema: "Tuko mbioni kuanza operesheni hiyo nchi nzima na jambo la msingi la kufahamu ni kwamba uhai wa wanyamapori unatuhusu sote, lakini viumbe hawa wa porini wakiwa katika mapori wanamoishi, sio muhimu tu kwa ajili ya kuajabiwa na kuvutia, lakini pia ni sehemu ya maliasili yetu na pia ndio mustakabali wa maisha yetu ya baadaye.

"Hivyo, kwa kukubali dhamana ya wanyamapori wetu tunatamka kwa dhati kwamba tutafanya kila tuwezalo kuhakikisha kwamba wajukuu wa watoto wetu watafurahia urithi huu mkubwa na wa thamani adimu."



Magari yakikwepa shimo lililopo katika barabara ya Mtaa wa Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, kwa muda mrefu na kusababisha usumbufu kwa vyombo vya moto. **PICHA: JOHN BADI**

# Mgogoro mnada wanyama wamalizwa

Na Godfrey Mushi, MWANGA

HATIMAYE, serikali imefanikiwa kuzima mgogoro kati ya wafugaji wa jamii ya kimasai na wakulima, baada ya kusababisha mnada wa mifugo wa Mgagao uliopo Wilaya ya Mwanga, mkoani Kilimanjaro kutotumika kibiashara kwa wiki mbili mfululizo.

Jana, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga, Zefrin Lubuva, alithibitisha mgogoro huo kumalizwa kwa busara na pande mbili zilizokuwa zikihasimiana zimekubaliana kurejea upya katika mnada huo.

Wafugaji walisusa kupelekea mifugo yao katika mnada huo kutokana na kutoelewana na wakulima kuhusu eneo linalozagaa mifugo hiyo, na hivyo pande hizo kuingia katika mgogoro uliosababisha pia Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga kupoteza mapato yake kwa siku 14.

Mgogoro huo ambao umeiathiri zaidi serikali kwa kukosa mapato, uliilazimisha kwenda kutafuta suluhu ya kudumu ili kuwarejesha upya wachuuzi wa mifugo kutoka maeneo mbalimbali nchini.

Lubuva alisema: "Ni kweli mgogoro huo umemalizika tayari na pande zote zimekubali kuendelea na utaratibu wao, nilipokwenda pale niliwaahidi wafugaji na wafanyabiashara wa mifugo kwamba tutafanya maboresho makubwa ya mnada huo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, wakiwamo wafanyabiashara wa mifugo.

"Lakini kikubwa ni kwamba, nitaendelea kusimamia kikamilifu mapato yanayotokana na mnada huo na kurudisha asilimia ya mapato hayo kwenye jamii ya wafugaji na wakulima ili kuendeleza miradi ya kijamii inayozunguka jamii hizo."

Sababu ya mnada huo kukosa wafanyabiashara, inatajwa kuwa ni kuibuka kwa mgogoro kati ya wafugaji wa jamii ya Kimasai na wakulima kuhusu eneo linalowekwa mifugo hiyo kuzurura hadi katika mashamba yao, jambo lililosababisha wafugaji kususa kupeleka mifugo yao katika mnada huo.

Baada ya kuafikiana, Katibu wa Chama cha Wafugaji wa wilayani Mwanga, Peter Moleli, alisema kuanzia sasa watarejea rasmi kwenye mnada huo wa Mgagao na watapeleka mifugo ya kutosha.

Katibu huyo alisisitiza kuwa wataendelea kuheshimu wafugaji na sheria zilizowekwa na serikali kwa manufaa na maendeleo ya Wilaya ya Mwanga.

# DC awaonya wapinga maendeleo Siha

Na Mwandishi Wetu, SIHA

MKUU wa Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro, Onesmo Buswelu, amesisitiza kuchukua hatua kali kwa watu wanaopinga masuala ya maendeleo katika eneo hilo na kuonya watendaji wa umma kujiingiza katika mtego huo.

Pia, ameagiza Halmashauri ya Wilaya ya Siha kuhakikisha wanatoa vitabu kwa watendaji wa kata ili waandike majina ya wananchi wanaochangia michango ya maendeleo, ikiwamo masuala ya elimu.

Buswelu alieleza kuchukizwa na taarifa za baadhi ya wanasiasa na hasa wenyeviti wa vijiji kujihusisha na usaliti huo wa kupinga maendeleo kutokana na itikadi za kisiasa.

"Kuanzia sasa atakayepinga maendeleo ya wananchi, sisi kama serikali hatutamvumilia kwa sababu maendeleo hayana chama wala itikadi za kisiasa. Pale panapohitajika kuchangia masuala ya maendeleo, tuchangie, tujumuike na tuhamasishane wote.


"Napenda kutoa onyo kali kwa wote wenye tabia ya kupinga maendeleo ya wananchi, nawashauri muache tabia hiyo mara moja kwa kuwa dawa yenu ipo jikoni na imeshaiva."

Alisema amechukizwa na tabia ya baadhi ya wenyeviti wa vijiji, kutengeneza migogoro ya ardhi ili kuwapotosha wananchi wasichangie maendeleo, ikiwamo ujenzi wa shule, madarasa na matundu ya vyoo.

"Nitachukua hatua kwa wale wote wanaokwamisha maendeleo kwa wananchi hususan viongozi wa vijiji ambao badala ya kuhamasisha ujenzi wa madarasa, nyie mnaingiza migogoro, mambo ambayo hayafanani kabisa na naomba majina ya viongozi wanaokwamisha maendeleo ili hatua zichukuliwe," alisema.

Wilaya ya Siha ilianzishwa rasmi Julai mosi, 2007, kwa sheria namba saba ya mwaka 1982 na kuwa miongoni mwa wilaya sita za Mkoa wa Kilimanjaro.

Wilaya hiyo ina jimbo moja la uchaguzi, tarafa za Siha Magharibi, Siha Kati, Siha Mashariki, Siha Kusini na Siha Kaskazini. Wilaya pia ina kata 17, vijiji 60 na vitongoji 169.



HABARI DODOMA

## Dk. Tulia awaelekeza wanawake, wasichana

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

NAIBU Spika Dk. Tulia Ackson, amesema uthubutu, kujiamini na elimu ndiyo njia pekee itakayowashawishi wanawake na wasichana kufikia malengo ya usawa wa kijinsia.

Aidha, ndiko kutakakowapatia nafasi mbalimbali za uongozi na kufanya maamuzi kwa maendeleo ya taifa.

Kauli hiyo aliitoa juzi katika kongamano la kitaifa kuhusu usawa wa kijinsia lenye kauli mbiu ya 'Ongeza ushirikiano kati ya watunga sera na asasi za kiraia ili kukuza usawa'.

Naibu Spika alisema ni vigumu kwa wanawake kufikia malengo hayo hata kama serikali imeweka mazingira mazuri kiasi gani kwa kuwa wao ndio wanakuwa chanzo cha kurudishana nyuma.

"Wanawake tunapaswa kwanza kuanza na sisi wenyewe kuhamasishana kushiriki kwenye vinyang'anyiro mbalimbali vya uongozi wa kiasiasa badala ya kusubiria mazingira mazuri yawekwe na tuache tabia ya kusemana ovyo hasa tunapopanda kwenye majukwaa ya kisasa," alisema Dk. Tulia.

Alieleza kuwa wanawake wanapaswa kufanya siasa za kistaarabu pindi wanapopanda kwenye majukwaa ya kisiasa kwani yamejitokeza matukio yanayoonyesha wanawake kukatishana tamaa kwenye majukwaa kwa kutoleana kauli chafu ambazo zinakatisha tamaa na kupelekea kukosa nafasi wanazoziomba.

Kadhalika alisema serikali inafanya juhudi ili kuinua haki za wanawake na wasichana ili kuwapa fursa na haki yao ya kushiriki na kutetea na kutimiza mahitaji yao ya haki za msingi.

Mbunge wa Mtwara Vijijini, Hawa Ghasia, akizungumzia uzoefu alioupata wa kuchaguliwa mara tatu katika jimbo lake, alisema wanawake wanapaswa kuondoa woga ili kusaidia kujiinua katika nafasi za uongozi.

Alisema wanawake wakiondoa hofu na kujitokeza wana uwezo mkubwa wa kushinda nafasi hizo, kwani katika uchaguzi wa 2015 kati ya wagombea ubunge 21 wanawake walioteuliwa ni wawili tu ambao walikosa nafasi.

Kwa upande wake, Mbunge wa Kaliua Magdalena Sakaya, alisema yeye alitukanwa matusi ya nguoni wakati wa kampeni za kugombea lakini alipambana na kuonyesha kujiamini na matokeo yake alipata nafasi ya mwakilishi.

# Serikali yaonya maabara hazitoi vipimo sahihi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, amesema vituo vingi vya afya vinatibu wagonjwa wengi kienyeji bila kuwa na vipimo sahihi vya maabara.

Naibu Waziri huyo alisema inahitajika kuboresha huduma za maabara nchini kwa kuwa watu wanatibiwa kienyeji mno.

Alisema vituo hivyo vinatibu magonjwa yasiyosahihi kutokana na kukosekana kwa ufanisi katika huduma za uchunguzi wa maabara.

Dk.Ndugulile alitoa kauli hiyo juzi wakati akizindua Bodi ya nane ya Maabara Binafsi za Afya jijini Dodoma. Alisema watu wamekuwa wakitibiwa kienyeji katika vituo vya kutolewa huduma kutokana na huduma za maabara kutofanya kikamilifu na vile ipasavyo.

Alibainisha kuwa maabara ni chombo muhimu sana katika sekta ya tiba inayotoa dira ya tiba sahihi kwa wagonjwa wanaohitaji huduma husika.

"Si hivyo tu, tafiti nyingi duniani zinahitaji maabara kuweza kupata ushindi wa kisayansi, hivyo bodi hii inajukumu kubwa la kuhakikisha kuwa, maabara zinakuwa na ubora unaostahili kwa faida ya Watanzania na watu wengine kwa ujumla,"alisema.

**Huko vichochoroni nikifanya ukaguzi hata hapa Dodoma naamini nitakuta maabara za uchochoroni ambazo hazina usajili zipo zinatoa huduma kwa wananchi lakini zipo maabara ambazo zinakwenda zaidi ya huduma za uchunguzi wa magonjwa.**

Naibu Waziri huyo alisema inahitajika kuboresha huduma za maabara kwa kuwa watu wanatibiwa kienyeji sana.

"Nimekuwa nikiongeleza sana suala la kuwa na maambikizi ya mkojo -UTI, taifoid na homa, mgonjwa akienda hospitali anakaa dakika 15 anambiwa una UTI, anakaa dakika tano anaambiwa una typhoid, sijawahi kuona uchunguzi wa magonjwa haya wa dakika 15 nilivyofundishwa mimi uchunguzi unachukua kati ya saa 48 hadi 72 ,"alisema.

Alieleza kuwa hali ya sasa ya huduma za maabara zimekuwa ikitumika kufanya biashara na kuwa chanzo cha mapato kwa vituo vya kutolewa huduma huku akisema wagonjwa wengi wanatibiwa kwa magonjwa yasiyo sahihi.

"Zaidi ya asilimia 70 ya homa wanasema ni malaria wala sio malaria, watu wanakunywa dawa sana bila kuzingatia,"alionya Naibu Waziri.

Ndugulile alikemea tabia iliyoanza kuibuka kwenye maabara ya kuacha kutoa huduma za kimaabara na badala yake kutoa tiba na upasuaji.

"Maabara zimeanza kutumika kama sehemu za kutolewa matibabu, yule yule mtu wa maabara ndiyo daktari, wengine wameenda mbali zaidi maana maabara zimeanza kufanya upasuaji, hili halikubaliki,"alionya Naibu Waziri.

Sambamba na hilo, Naibu Waziri huyo aliitaka bodi hiyo kwenda kutafakari na kuona namna ya kuja na mchakato wa mabadiliko ya sheria ambayo ni ya muda mrefu ili iende na wakati na pia kuongeza majukumu ya Bodi.

Alitaka majukumu yaongezwe badala ya kusimamia maabara binafsi pekee bali hata maabara za vituo vya hospitali za umma ambazo pia baadhi yake zimekuwa hazifanyi vizuri.

Akizungumzia kuhusu uanzishaji holela wa maabara, Dk.Ndugulile aliitaka bodi hiyo kukabiliana na hali hiyo kwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara.

"Huko vichochoroni nikifanya ukaguzi hata hapa Dodoma naamini nitakuta maabara za uchochoroni ambazo hazina usajili zipo zinatoa huduma kwa wananchi lakini zipo maabara ambazo zinakwenda zaidi ya huduma za uchunguzi wa magonjwa,"alisema.

Aliitaka bodi hiyo kuja na kanzidata ya maabara na maduka yanayouza vifaa vya maabara na vitendanishi ili ifahamike yako magapi na yanafanya nini.



Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Deogratius Ndejembi, akiendesha trekta wakati wa maonyesho ya zana za kilimo yaliyofanyika Kibaigwa, Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wakulima watakiwa kukopa kwa malengo

**Na Ibrahim Joseph,** KONGWA

MKUU wa Wilaya ya Kongwa, Deogratius Ndejembi, amewataka wakulima kujiwekea malengo kabla ya kwenda kuchukua mikopo ya matrekta kwenye taasisi za kifedha ili wasijekukwama kwenye urejeshaji.

Ndejembi alitoa kauli hiyo jana wakati alipozungumza kwenye maonyesho ya zana za kilimo na uzinduzi wa trekta aina ya John Deere 3050B 4DW iliyofanyika wilayani Kongwa kwenye mji mdogo wa Kibaigwa.

Uzinduzi uliwashirikisha wakulima wakubwa na wadogo na uliandaliwa na Shirika la Lonagro.

Ndejembi aliwataka wakulima hao kujiwekea malengo yao ya kilimo kwanza kabla ya kutafuta mikopo ya kununua matrekta kwenye taasisi za kifedha.

"Leo hii hapa Kibaigwa kuna wakulima wengi na kampuni zinakuja na bidhaa mpya za trekta cha msingi ni ninyi wakulima kujiwekea malengo kwanza kabla huchukua mkopo wa trekta, sio kutegemea kuwalimia wenzako utakwama kurudisha mkopo huo,"alisema Mkuu wa Wilaya.

Alisema kutokana na uwingi wa wakulima katika wilaya hiyo kuna kampuni nyingi zimeendelea kuwapelekea wakulima hao matrekta kwa masharti ya mikopo hivyo wahakikishe wanaweka malengo kabla ya kuchukua mikopo hiyo.

Aidha, alizitaka kampuni hizo kupelekea pia vipuri katika maeneo hayo ili kuwapunguzia mzigo wa kuvifuata mbali.

"Unakuta kampuni inamuuzia mkulima kifaa lakini vipuri vyake vinakuwa havipatikani kwenye eneo lake na kama vinapatikana wanawauzia bei ya juu,hili serikali hatukubaliani nalo ,waleteeni kila kitu hapa ili kuwapunguzia mzigo wakulima wetu,"alisema Ndejembi.

Kwa upande wake, Meneja mauzo wa kampuni ya Lonagro Tanzania, Magreth Shilungushela, alisema kampuni hiyo ilikuwa ikiuza aina zingine za trekta lakini wameamua kuzindua aina hiyo mpya ili kuwasaidia wakulima wadogo.

Shilungushela alisema kampuni yao pamoja na kuwauzia wakulima trekta hizo wamekuwa wakiwasambazia vipuri na kutoa elimu ya jinsi ya kuyatunza matrekta hayo ili kupuka kudanganywa na mafundi wasiowaaminifu.

Alisema kampuni yao inatoa mikopo ya trekta hizo kwa wakulima na wafanyakazi kwa kulipa kwa awamu au wahusika kuchukua mkopo kupitia benki ya mbalimbali walizoingia nazo mkataba





# Balozi Iddi afurahishwa usimamizi, ufanisi Tasaf

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amesema ufuatiliaji pamoja na usimamizi makini wa watendaji wa ofisi yake katika kuratibu matumizi sahihi ya fedha zinazotekeleza miradi ya kijamii imefanikisha vyema miradi ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (Tasaf).

Alisema Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar ambayo inaratibu shughuli zote za Tasaf kwa upande wa Zanzibar, imelazimika kuchukua hatua hiyo ili kulinda heshima itakayotoa ushawishi kwa wafadhili wa mpango huo kuendelea kuunga mkono utoaji wa mikopo zaidi.

Balozi Iddi aliyasema hayo wakati wa mazungumzo yake ya Timu ya Waratibu Wakuu wa majimbo 36 yanayounda Taifa la Nigeria waliopo Zanzibar kwa ajili kujifunza kutokana na mafanikio makubwa yaliyopatikana katika mpango wa kuhudumia Alieleza kwa vile Tasaf inatoa huduma katika pande zote mbili za Tanzania, serikali zote mbili ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, zinalazimika kufuatilia mwenendo mzima wa fedha zinavyotumika katika miradi hiyo ili kufikia lengo.

**Serikali ililazimika kufanya uchambuzi yakinifu na kujiridhisha katika mwenendo wa matumizi ya miradi ya Tasaf ili kuepuka upotevu ambao ungegharimu machungu kwa wasimamizi wa miradi hiyo.**

"Serikali ililazimika kufanya uchambuzi yakinifu na kujiridhisha katika mwenendo wa matumizi ya miradi ya Tasaf ili kuepuka upotevu ambao ungegharimu machungu kwa wasimamizi wa miradi hiyo," alisema Iddi.

Alisema ipo miradi mingi ya kijamii katika maeneo mbali mbali ya visiwa vya Unguja na Pemba iliyoleta ukombozi kwa wananchi wengi baada ya kupata msukumo uliotokana na uanzishwaji wa Tasaf uliojikita kuhudumia moja kwa moja miradi hiyo.

Balozi Iddi alisema ipo haja kwa wafadhili wa miradi ya kijamii kama Benki ya Dunia pamoja na taasisi nyingine za kimataifa za misaada ya maendeleo kuendelea kuongeza ufadhili wao kwa vile lengo la uanzishwaji wa miradi ya kijamii limefanikiwa vyema.

Hata hivyo, alisema hatua hiyo ya wafadhili ni muhimu kwa vile inaweza kusaidia kuondoa mkwamo kwa baadhi ya changamoto zinazotokana na miradi inayoanzishwa hasa katika sekta za uzalishaji kupitia vikundi vya ujasiriamali.

Aliishauri timu hiyo ya waratibu wakuu wa majimbo ya Nigeria ili kuimarisha miradi na huduma za kijamii ipo haja ya mataifa ya Afrika kuzidi kushirikiana katika kubuni mbinu na njia za pamoja za kuendeleza miradi hiyo itakayoleta ustawi na maisha bora kwa Waafrika wengi.

Naye Mratibu wa washirika wa sekta za kijamii kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais wa nchini Nigeria, Gyangyang Limave, aliipongeza Tanzania kwa umakini wa kuhakikisha Bara la Afrika linaendelea kuimarika kiuchumi na ustawi.

Alisema msimamo wa Tanzania katika kustawisha maisha ya wananchi wake ni wa kuigwa na mataifa mengine duniani yaliyoanza mpango wa kuimarisha taasisi za kijamii.

Alisema Serikali ya Nigeria katika mwelekeo wake wa kustawisha maisha ya wananchi wake, imeshaanzisha taasisi inayoratibu na kusimamia masuala ya kijamii mwaka 2016.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi (kushoto), akiagana na Kiongozi wa Timu ya Waratibu Wakuu wa Majimbo 36 yanayounda Taifa la Nigeria, Naibu Mkurugenzi wa Taasisi inayosimamia masuala ya Ustawi wa Jamii, GyangyanLimave, baada ya mazungumzo yao, mjini Zanzibar juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Wadau washirikishwe mabadiliko ya sheria

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

TUME ya kurekebisha sheria Zanzibar imetakiwa kuwashirikisha wananchi kutoa maoni katika sheria mbali mbali zinazotarajiwa kufanyiwa marekebisho kikamilifu.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Katiba na Sheria, Khamis Juma Maalim, wakati akifungua mafunzo ya siku moja kwa waandishi wa habari kuhusu kazi za Tume ya kurekebisha sheria.

Alisema yapo malalamiko kwamba sheria nyingi zinazotungwa haziwashirikishi wananchi na kujitokeza tatizo la utekelezaji wake.

Alieleza kwamba sheria zote zinazotungwa, lengo lake ni kuwahudumia wananchi kama watekelezaji wakubwa na hivyo kitendo cha kushindwa kuwashirikisha ni kasoro kubwa.

"Tunatunga sheria nyingi, lakini moja ya tatizo letu hazitoi ushirikishwaji wa wananchi na hivyo wakati mwingine zinaleta upinzani katika utekelezaji wake," alisema.

Alisema katika kipindi cha Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, kazi kubwa imefanywa ya kuzipitia sheria zote ambazo zinaonekana zimepitwa na wakati.

"Bado tunaiomba Tume ya kurekebisha sheria kufanya kazi ya ziada ya kuzipitia sheria ambazo zinaonekana zimepitwa na wakati au zinahitaji marekebisho katika maeneo mbalimbali," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji Bakari Mshibe, alisema katika kipindi cha miaka tisa jumla ya sheria 37 zimepitiwa.

Alisema utaratibu wa sasa unaotumika katika kuzifanyia marekebisho sheria hizo ni kusikiliza na kutoa maoni ya wananchi.

Pia, alisema tatizo la kushindwa kuwashirikisha wananchi katika kutoa maoni athari zake zimeonekana.

"Tumefanya marekebisho makubwa na sasa sheria yoyote inayotaka kufanyiwa marekebisho kwanza lazima yapatikane maoni ya wananchi," alisema.

# Vijana waamshwa kuacha uvivu, malalamiko

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

VIJANA wametakiwa kuzitumia vyema fursa za kujiendeleza kimaisha katika nyanja mbalimbali badala ya kuendekeza uvivu na kulalamika.

Akitoa mafunzo kwa vijana kwenye Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar Vuga, mjini Unguja, Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa kampuni ya Sahara Ventures ya Dar es Salaam, Mussa Kamata, alisema vijana wanapaswa kuwa jasiri na wenye uthubutu.

Mafunzo hayo yaliyoratibiwa na Taasisi ya Zanzibar Sparks chini ya ufadhili wa Sahara Ventures na SUZA, yamelenga kuwajengea vijana uwezo wa kubuni mawazo ya biashara na ujasiriamali yatakayowavutia wawezeshaji ili hatimaye wapewe mitaji na fursa ya kuyatekeleza kivitendo.

Alisema uzoefu unaonyesha, watu wengi waliofanikiwa kimaisha na kupata utajiri mkubwa, walianza na mitaji midogo kwa kujishughulisha na biashara ndogondogo ambazo wengine wanazibeza na kuziona kuwa ni mzaha.

Kamata alieleza kuwa, Zanzibar na Tanzania zina fursa nyingi za kujiajiri ambazo kama vijana watazichangamkia ipasavyo na kitaalamu, umaskini utabaki kuwa historia badala ya kung'ang'ania ajira za serikali ambazo hazitoshi.

Aliwashauri kila wanapofikiwa na siku mpya na kuamka, akili zao ziwe na wazo lolote la ubunifu wa namna ya kujikwamua na maisha ya utegemezi.

"Sisi vijana tuone aibu kulalamika kwamba hatuna ajira au zinachukuliwa na wageni wakati nchi yetu imezungukwa na rasilimali na fursa nyingi ambazo tunapaswa kuzichangamkia," alieleza mkufunzi huyo.

Aliwasisitiza vijana kufuatilia matukio yanayotokeza katika nchi za nje ikiwamo Afrika Kusini na kujifunza ili akili zao zisihadaike na kujikuta wakiiga na hatimaye kuingia matatani.

Akifunga mafunzo hayo, Msimamizi wa Mfuko wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo na vya Kati (SNIDA) Shadida Ali, alisema kupitia mfuko huo, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imeamua kuwawezesha vijana katika miradi kwa mfumo wa teknolojia ili wafikie malengo ya kuajiriwa au kujiajiri.

Alisema SNIDA ina utaratibu wa kuwapa mikopo yenye masharti nafuu vijana wanaohitimu vyuo mbalimbali kwa lengo la kuwainua kiuchumi na kumudu kujiendesha kimaisha wao na familia zao.

Aliwaambia vijana walioshiriki mafunzo hayo kuwa, mafanikio ya mtu hutokana na fikra na maarifa mazuri yanayotoka kichwani mwake ambazo zikipangwa vizuri zitaweza kumuinua kiuchumi na kuyabadili maisha yake kuwa bora.

Yussuf Ali Suleiman, aliyehitimu Shahada ya Sayansi ya Kompyuta katika Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) mwaka 2019 ambaye alishiriki mafunzo hayo, alisema vijana wengi wanashindwa kufiki-



Soma UK. 14

**MBOSSO**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# BT
BURUDANI TELE

JUMAMOSI SEPTEMBA 14, 2019



# BOSS MARTHA
## NYOTA ILIYONG'AA IKAZIMIKA GHAFLA

UK.16

## BASI SAWA



## Wakoloni wanasababisha fujo Sauzi-Vanessa

MSANII wa muziki wa Bongo Fleva, Vanessa Mdee amesema kuwa chanzo cha vurugu za kibaguzi nchini Afrika Kusini, kiini chake ni Wakoloni.
Wakati wengi wanawalaumu raia weusi wa Afrika Kusini kwa kuwabagua Waafrika wenzao kuwapiga, kuwanyang'anya mali zao na kuwaua, Vanessa amesema kuwa chanzo cha yote hayo ni Wakoloni kuligawa Bara la Afrika, kwani mwanzo hakukuwa na mipaka.
Vanessa amedai ujio wa wakoloni ndio walioleta mikakati ya kuigawa bara la Afrika, Kwa kuweka mipaka, Jambo ambalo likasababisha watu kuanza kubaguana kwa utaifa wao.
"Walipokuja kututawala ndipo walipoligawa, hapa achukue nani, hapa atawale nani, na wao ndiyo waliweka mipaka. Mimi ninavyojua mwanzo hakukuwa na mipaka, hivyo Afrika ilikuwa ni moja wa Waafrika walikuwa wamoja, walipokuja wao ndiyo walitugawa na haya yote ni matokeo ya wakoloni. Alisema.



## Prezzo kama Sugu na Profesa Jay

MSANII wa muziki wa Hip Hop nchini Kenya, Jackson Makini maarufu kama Prezzo ametangaza rasmi kuingia kwenye siasa kwa kuchaguliwa nafasi ya kugombea ubunge katika jimbo la Kibra nchini humo.
Prezzo aliteuliwa na Chama cha Wiper Jumanne iliyopita mbele ya kiongozi wa Chama hicho, Kalonzo Musyoka ambaye alishawahi kuwa Makamu wa Rais wa Taifa hilo.
Taarifa hiyo imepokewa na kwa mikono miwili na Wakenya, Huku wengi wakimlinganisha na msanii mwenzie wa muziki, Jaguar ambaye yeye kwasasa ni Mbunge wa Jimbo la Starehe.
Kalonzo anaamini kuwa kutokana na umaarufu wa Prezzo, ana uwezo mkubwa wa kuchukua jimbo hilo kwenye uchaguzi utakaofanyika Novemba 7 mwaka huu.
Prezzo atapambana na mwakilishi mwingine wa Chama cha ODM, Imran Okoth kwenye kinyang'anyiro cha kusaka ubunge kwenye jimbo hilo la Kibra. Kama akichaguliwa atakuwa amefuata nyayo za Wana Hip Hop wenzake nchini Tanzania, Joseph Mbilinyi maarufu kama Sugu ambaye kwa sasa ni Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini, lakini pia Joseph Haule maarufu kama Profesa Jay ambaye yeye ni Mbunge wa Jimbo la Mikumi.



# MBOSSO AFUNGUKA KIFO CHA MZAZI MWENZAKE

MSANII Maromboso amefunguka kuwa mzazi mwenzake Boss Matha amefariki akiwa katika harakati za kutafuta nyumba, huku akikabiliana na changamoto za maneno maneno ya kifamilia.
Akizungumza kuhusu kifo hicho, Mbosso, huku akilengwa na machozi alisema siku chache kabla ya kifo hicho alizungumza na mzazi mwenzake mengi kwa njia ya simu.
"Mimi mwenyewe nilimwambia nahama Tegeta hahamia Mbweni, na yeye akaniambia kuwa anatafuta nyumba, akasema ataondoka Sinza atafute nyumba hata Mbezi Beach, pia akaniambia mtoto yupo Tabora, nikamshauri amrudishe Dar." Alisema na kuongeza.
"Kuna vitu vingi akaniambia kuhusu matatizo na familia yake, lakini mimi siwe muongo kwa sababu sikuwa na ukaribu naye kihivyo. Na pia marehemu hakutaka kabisa tuwe tunazungumzia suala la mtoto kwenye vyombo vya habari, yeye akihojiwa au mimi, hivi hapa nilivyoongea, najua namkosema marehemu." Alisema.

## INSTA-TWITTER





**Watu** hawasemi yote. Maneno usimalize, utakaukwa na mate, mengine shuti umeze.
Ubaya ni kotekote siri usizitangaze. Ulichague unalosema na usipayuke kwanza chunguza na ukumbukie na ule mwema-**Riyama Ally.**



**Unafika** nyumbani unakuta umeme umekatika. Unaamua kuwasha taa ya simu ili ukaoge. Unajimulikia unamaliza, baadae wakati unajikausha maji unacheki simu kumbe uko live Instagram. Kesho yake kwenye vikao hii ndio huwa mikao yake-**Peter Msechu.**



## Naibu Spika atamani ubora wa filamu

NAIBU Spika wa Bunge, Dk Tulia Ackson amewataka vijana kugeuza sanaa ya filamu kuwa sehemu ya ajira inayowaingizia kipato kama ilivyo kwa nchi zingine.

Akizungumza na vijana wanne waliofuzu mafunzo maalum ya uzalishaji filamu chini ya programu ya MultiChoice Talent Factory jijini Dodoma, Dk. Tulia amesema kama mafunzo hayo watayatumia vizuri wanaweza kubadilisha sekta hiyo na kuwa pendwa kama ilivyokuwa zamani.

Vijana waliopatiwa mafunzo hayo ni Jane Moshi, Sarah Kimario, Jamal Mohamed na Wilson Nkya.




@burudanitele

>>> **Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow**

UN...



# CHUCHU HANS MJAMZITO?

UJUMBE wa mwigizaji wa Bongo muvi, Ray Kigosi akimtaka mpenzi wake Chuchu Hansy, kuongeza mtoto mwingine umeibua mapya baada ya baadhi ya watu kudai kuna ujio wa mtoto huyo miezi michache ijayo.


Mashabiki wa waigizaji hao walidai kwamba Ray hakukurupuka kuandika ujumbe huo kwamba anajua kilicho nyuma ya pazia kuhusu mzazi mwenzake. Ray Kigosi na Chuchu wamekuwa kwenye mahusiano ya kimapenzi kwa muda na mpaka sasa wamejaaliwa kuwa na mtoto mmoja wa kiume waliyemuita Jaden.

## INSTA-TWITTER

Tuffolow/ Tu-tag
@burudanitele



**Muda** Ndio kila kitu, kama muda wako haujafika subili, haina haja ya kukimbizana na Muda-**Steve Nyerere.**



**Kuna** kipindi moyo unakuwa na furaha kama vile haujawahi kuwa na hudhuni,unaona kama dunia yote yako peke yako. Yote hii sababu siruhusu kukumbuka mabaya ya nyuma na wala sijutii, ingawa najifunza na sisahau-**Nisha Bebe.**



**Ahsanteni** sanaa wanafunzi wa shule ya msingi Tandika Mtwara kwa kunilavu. Nami nasema lavu yuu ninyi wote ahahaa ila huku mnanipenda na kusoma pia kuwepo, msitindinganye mambo-**Tausi Mgendela**

# Kuumbe!



# BOSS MARTHA

## NYOTA ILIYONG'AA IKAZIMIKA GHAFLA

TASNIA ya uchekeshaji nchini imepata pigo baada ya msanii wake maarufu aliyefahamika kama Boss Martha kufariki dunia wiki hii.

Martha (24) ambaye ni mzazi wa mwanamuziki wa WBC, Mbosso, aliaga dunia baada ya kuugua kwa muda mfupi

Kifo cha mrembo Martha aliyekuwa akijishughulisha na shuguli za uchekeshaji kupitia kipindi cha 'Cheka Tu' kimewashtua wengi na kusababisha mastaa mbalimbali kutoa machozi hadharani.

Mchekeshaji huyo wa kike ndio kwanza kipaji chake kilianza kung'aa kutokana na aina ya uchekeshaji wake kuwa tofauti kwa kuelezea maisha halisi ya uswahilini.

Ukiangalia baadhi ya vipande vya kazi zake zinazopatikana katika mtandao wa You Tube, utagundua Martha alikuwa nyota wa jukwaani na hakukosea kujiita jina la Boss Martha kutokana na kazi zake nzuri.

Maelezo yaliyopatikana awali inaeleza msanii huyo alikuwa akiugua uti wa mgongo kwa muda mrefu na kisha kuugua maleria kali iliyoondoa uhai wake.

Enzi za uhai wa Martha aliwahi kufanya kazi nyingi ikiwemo kupamba video za wanamuziki wa Bongfleva kama ya msanii Whozu kwenye wimbo wake 'Roboti'

### ATAKA SARE NYEUPE

Akisimulia kwa uchunga mama yake mzazi alisema kabla ya kufariki mwanawe alimwambia anajua anakufa na kumuomba akifa watu wavae sare ya rangi nyeupe .

"Siku ya mwisho mwanangu aliniambia mama najua nakufa, naomba watu wavae sare nyeupe, nilimwambia hapana hautakufa kumbe alikuwa ananiaga kweli," amesema huku akilia kwa uchungu

### MBOSSO ANA SIRI NZITO


Msanii anayetamba katika Bongofleva, Mbosso, ameonekana kuguswa zaidi na kifo hicho huku akifichua siri kwamba yeye na marehemu Martha wana mtoto mmoja.

Katika mahojiano yake na Bongo5, Mbosso alisema kifo chake kimemshtua kutokana na na marehemu kupanga mambo mengi.

"Siku moja kabla ya kifo chake niliongea na rafiki yake anayeitwa Malaika twende kesho yake tukamuangalie, lakini ilipofika jana nilipompigia alianza kulia akisema Martha ameaga dunia, nilishtuka sana," amesema Mbosso.

Mbosso alisema maisha yake na Martha yalitawaliwa na vikwazo vingi kiasi ambacho mambo mengi walifanya kuwa siri na hata kuhusu mtoto wao hawakutaka kuweka wazi ili kulinda uhusiano wao.

# KALI 5 ZINAZOENDELEA KUISHI



**Na Adam Fungamwango**

WADAU wengi wa muziki wamekuwa wakiwashauri sana wasanii wa bongo fleva kuacha sana kutunga nyimbo za mapenzi kwa zaidi ya asilimia 90, na badala yake wajikite pia kutunga nyimbo za matukio.

Hata hivyo wamekuwa wakikumbana na upinzani mkali kwa vijana wa kizazi kipya ambao wengi wamenufaika zaidi kiuchumi.

Lakini ukweli utabaki pale pale kuwa nyimbo nyingi za kisasa zinaegemea mapenzi, na huwa hazidumu na zinasahaulika kwa muda mfupi.

Kuna nyimbo zimepigwa zaidi ya miaka 50 iliyopita, lakini kwa sababu ni za matukio, hadi leo zimeendelea kupigwa linapokuja tukio au kumbukumbu ya tukio hilo.

Pamoja na pesa, lakini wanamuziki na wasanii wa sasa wanapashwa kujua kuwa, baadaye watazeeka, au kufa, hivyo wanatakiwa kuacha alama yao kwenye muziki.

Mwanamuziki au msanii yoyote hawezi kuacha alama ya muziki wake kupigwa redioni, au kwenye vituo vya televisheni kama pia hawawezi kutunga nyimbo za matukio, hasa yale yanayojirudia.

Wanamuziki waliofanya hivyo huko nyuma, pamoja na kwamba baadhi yao wamefariki, lakini wamekuwa wakikumbukwa na kujulikana hadi leo na watakumbukwa vizazi na vizazi vijavyo.

Msanii gani hataki hili?

**Mkono wa Idd-Salum Abdallah**

Ni miaka 59 sasa imepita tangu kufariki kwa mwanamuziki maarufu, aliyekuwa staa miaka ya '50 hadi '60, Salum Abdallah. Ni zaidi ya miaka 60 imepita tangu aliporekodi kibao cha 'Mkono wa Idd'.

Alifariki mwaka 1965 mjini Morogoro kwa ajali ya gari, lakini wimbo wake huo umebaki kumbukumbu hadi kwenye kizazi cha leo, ambacho hakijapata kunshuhudia.

Kila mwaka inapokuja sikukuu ya Idd El Fitri, kibao hicho ndicho kinachopamba zaidi sikukuu hiyo kiasi hata kizazi cha leo hii kumfahamu. Kwa maana hiyo Salum ataendelea kukumbukwa vizazi kwa vizazi kutokana na wimbo huo tu ambao maudhui yale ni endelevu.

**Christmas-King Kiki ft Maquiz Du Zaire**

Katikati ya miaka ya '70, mwanamuziki Kikumbi Mwanza Mpango, maarufu kama King Kiki, akiwa na bendi ya Maquiz Du Zaire alitunga kibao cha 'Christmas'. Ni wimbo ambao unazungumzia sikukuu ya Krismasi, ambapo Wakristo wote duniani wanakumbuka kuzaliwa kwa Yesu Kristu zaidi ya miaka 2000 iliyopita. Ni wimbo ambao kila ikikaribia Desemba 25 ni lazima usikike. Kutokana na hali hiyo Kiki, ataendelea kukumbukwa na wimbo wake kupigwa vizazi kwa vizazi.

**Siku ya Kufa- Dk. Remmy ft Orchestra Makassy**

Mwanamuziki Dk. Remmy Ongalla, ni mmoja wa wasanii ambao hawatosahaulika na vizazi hadi vizazi kutokana na kutunga nyimbo kadhaa za matukio, hasa za vifo. Mwishoni mwa miaka ya '70, alitunga wimbo wa 'Siku ya Kufa' akiwa na Orchestra Makassy. Pamoja na mambo mengine, ni wimbo unaozungumzia binadamu anapofariki, anaacha ndugu, jamaa, na pia haendi na mtu yoyote yule kaburini hata mke au mume.

Kutokana na kutokuwepo kwa nyimbo za vifo kwa kizazi cha sasa, ni wimbo unaotumika mno kwenye maombolezo, wanapofariki viongozi, mastaa, wanamuziki au watu muhimu kwenye jamii kila inapotokea.

**Noeli-King Kiki ft OSS**

Huyo huyo mzee Kiki, mwanzoni mwa miaka ya '80 alipotoka Maquiz na kujiunga na Orchestra Safari Sound (OSS) iliyokuwa na mtindo wa Masantula, alitunga wimbo mwingine wa Krismasi, uitwao 'Noeli'.

Maudhui ni yale yale, kuizungumzia sikukuu hiyo, kitu ambacho kinamuweka kwenye orodha ya wasanii ambao kila mwaka ikikaribia sikukuu hiyo, sauti yake itasikika, kwani ni wimbo ambao ni lazima upigwe kwenye redio.

**Kifo-Dk. Remmy Ongalla**

Miaka ya '80, Dk. Remmy alirudi tena. Safari hii akiwa na Super Matimila, alitunga wimbo wa 'Kifo'.

Staili ya wimbo huu ni kama vile anakilalamikia kifo kuwa kwa nini kinaua watu. Kwa nini kimekuwa katili? Kinaua watu wote na hakuchagui. Hata uwe bondia au mtemi vipi, siku ikifika utakwenda.

Ni wimbo ambao linapokuja suala la maombolezo ya kitaifa, au kifo cha kiongozi, staa yoyote nchini, ni lazima utapigwa. Na kama zikikosekana nyimbo za aina hiyo kwa wasanii wa kisasa utaendelea kupigwa kizazi kwa kizazi. Remmy alifariki mwaka 2010 jijini Dar es Salaam.

# Vijimambo

1. Hii ndio inaitwa 'nikinywa maji, nakuona kwenye glasi' - Agatha Mbale, Moro Town.
2. Ai weeewe, naoomba - Ebby Mbwambo, Tanga.
3. Hahahaaa, endelea kuomba tu mzee baba, atakupa tu - Maunda Alawi,
4. Duuh, kweli utoto kazi! Kidume kinategemea kabisa kimegewe mkate! - Beneali Moussa, Zenji.
5. Naomba, ukinipa na mie nikinunuliwa soda nakupa - Mauwa Minde, Kibada Kigamboni DSM.
6. Lazima huyo dogo atakua wa Bush Stars, anaiomba picha mkate! - Sultani Ubwa, Kibada DSM.
7. Endelea tu kuomba, huyo siyo mchoyo atakumegea tu - Moussa Beneali, Migombani Zenji.
8. Kama ulikuwa hujui tafsiri halisi ya neno 'zwazwa', basi ndio hiyo - Beneali Moussa, Migombani Zenji.
9. Naenda kukusemea kwa mama yako umeomba mkate kwa watu ->Julius Anthony, Usagara Tanga.
10. Acha uchoyo wewe, mwenzio anakuomba ndio unaingiza wote mdomo! - Mama Nah, Manzese DSM.
11. Mwache na uchoyo wake, na wewe ukinunua vitu vyako usimpe - Rehema Bwahoja, Buguruni DSM.
12. Dogo utachubuka 'makongoro' kwa kupiga magoti, hiyo picha tuu - Subira Bwahoja, DSM.
13. Jamani, si mngemuambia kama hiyo ni picha tu sio mtu kweli. Ona sasa anavyotia huruma - Dule DSM.
14. Yes, hiyo ndio dawa ya ombaomba. Kesho leteni roli lenye picha ya hela - Kijusi, Magomeni Mapipa DSM.
15. Daaah, mjukuu wa 'Matonya' anadhalilika hivi hivi kwa picha tu - Kijusi, Magomeni Mapipa DSM.
16. Huyo naye kubwa zima hajajua tu picha na mtu wa ukweli? Muacha achune magoti - Kole, Msata Pwani.
17. Hapo atalifuata gari mpaka wapi kwa kupiga magoti hivyo Magdalena Kachenja, Mabwepande DSM.
18. Tatizo dogo hajafunguka, anataka mkate au anataka uchumba - Alli Shaaban Mpanjira, Mbagala Kuu DSM.
19. Kweli walimu wanakazi. Huyo mpaka aje kujua hiyo ni picha tu si atakua Chuo Kikuu! - Pili Mpanjira DSM.
20. Mmmh, mie mgeni hapa, acha nipite tu! - Abass Ngulunga, Msasani Macho, DSM.
21. We mtoto utagongwa na magari buree. Huyo sio mtu kweli ni picha tu - Bernad Isuja, Makore Dodoma.


**SMS Bomba ya Leo:**

**Tatizo dogo hajafunguka, anataka mkate au anataka uchumba -Alli Shaaban Mpanjira, Mbagala Kuu DSM.**

## PICHA MPYA




**TUMA MESEJI - 0773 477311**




# Catherine: Mchawi anapokuwa ndugu

**Na Adam Fungamwango**

UMDHANIAYE ndiye kumbe siye. Na umdhaniaye siye kumbe ndiye.

Unaweza kupata matatizo au mkasa ambao hujui chanzo chake ni nini.

Wakati mwingine anaweza kuwa ni ndugu wa damu ndiyo anakuumiza.

Filamu ya 'Catherine' inaweza kuwa mfano tosha wa haya ninayobainisha hapa.

Filamu hii imechezwa na magwiji wa tasnia hiyo nchini kama Hemed Suleiman, Jackline Wolper na msanii anayekuja kwa kasi Najma Dattan, pamoja na msanii wa bongo fleva Hamad Ally 'Madee'.

Hemed anatokea kumpenda Najma ambaye ni dada wa Madee, huku wao wenyewe wakiwa ni marafiki wa damu.

Hata hivyo, Madee anapinga rafiki yake Hemed kumpenda dada 'ake kwa madai kuwa hajatulia.

Hemed anamhakikisha Madee kuwa ni kweli amekuwa kicheche, lakini kwa Najma atatulia na hatimaye kumuoa kabisa.

Akamhakikisha shemeji mtarajiwa kuwa hana nia ya kumchezea, kitu ambacho kinapingwa vikali na Madee.

Mapenzi ya Hemed na Najma yanakuwa motomoto kiasi cha kwamba hakuna tena mtu wa kuyazuia na kufikia posa kutolewa.

Kabla ya ndoa anawasili kutoka nchini Marekani alikokwenda kwa masomo dada wa Najma ambaye ni Wolper aliyecheza kama Sharon.

Aina yake ya maisha akawa anaijua mwenyewe, kwani ni tofauti na Najma ambaye amelelewa katika mazingira ya kumcha Mungu.

Sharon, binti aliyeishi kwenye nchi za watu, mwenye mbwembwe nyingi na kuyajua ya usiku na ya mchana anaanza kuona wivu mdogo wake kuwa na mvulana 'handsome'.

Anatumia kila aina ya hila ili kumgombanisha Najma na Hemed na anafanikiwa.

Anamtumia kijana mmoja 'kumpaka' Najma mbele ya mchumba wake kuwa amekuwa akitembea na mume wa dada yake kiasi kwamba amesababisha dada yake kukosa amani kwenye ndoa.

Pia kijana huyo anatuma meseji za mapenzi kwenye simu ya Najma kwa kutumiwa na Sharon.

Hemed anachukia na kuachana na mchumba wake, lakini pia akiingia kwenye penzi la siri na dada wa mchumba wake Sharon.

Za mwizi arobaini, Najma anawafuma 'live' kitandani dada yake na mchumba 'ake kitu ambacho kinasababisha achanganyikiwe na kukimbia mbio kiasi cha kugongwa na gari.

Sharon naye baada ya kuona hila zake zimegundulika anaamua kunywa vidonge kwa ajili ya kujiua, lakini anapona.

Kikao kikubwa kinafanyika na kila kitu kinagundulika.

Filamu inaisha kwa Hemed kufunga ndoa na Najma.

Ni filamu nzuri sana, lakini sijaridhishwa na jinsi ilivyomaliziwa.

Kwanza kabisa Sharon kwa sababu ndiye mkosaji mkuu kwenye filamu hii, adhabu yake ingekuwa ni kufariki alipokunywa vidonge ili kuiambia jamii kitu alichokifanya si kizuri.

Pia kwa maadili ya Kiafrika, sidhani kama kuna mzazi yoyote angeweza kukubali kumpa binti yake aolewe na mwanaume ambaye tayari ameshatembea hata na ndugu wa ukoo wake tu, achilia mbali Sharon ambaye ni ndugu wa damu moja na Najma.

Kilichotakiwa kumaliziwa hapo kwamba, kwa kosa alilolifanya Hemed kutembea na dada wa mchumba wake, angekosa mke. Sharon angekufa kwa kosa la uchonganishi na kuhatarisha ndoa ya mdogo wake.



# MTATA

## AKISIMAMA JAGUAR LAZIMA UTOKE JASHO

MIEZI michache iliyopita, Mbunge wa Jimbo la Starehe nchini Kenya, Jaguar, aliibua utata baada ya kutoa kauli ya kibaguzi kwa wageni wanaoishi nchini humo.

Mbunge huyo ambaye pia ni mwanamuziki, alisababisha serikali ya Kenya na Tanzania kuwa katika uangalizi wa hali ya juu baada ya kuwataka raia wa Tanzania na nchi zingine wanaofanya biashara nchini humo kuondoka mara moja.

Kauli yake ilisababisha viongozi wa nchi hizo mbili kukutana haraka na kisha kumkemea kiongozi huyo ambaye naye alikiri kuteleza na kuomba radhi.

Sasa Jaguar, amekuja na jambo jipya ambalo kama likipitishwa wafanyakazi wa Kenya ambao wana umri mkubwa wanaweza kupoteza kazi zao ndani ya serikali.

Mbunge huyo amewasilisha mapendekezo serikalini akitaka umri wa kustaafu upungue kutoka miaka 60 hadi 50 ili kuongeza ajira kwa vijana.

Akitoa mapendekezo hayo juzi, Jaguar amesema kuwa Kenya inakabiliwa na uhaba wa ajira kwa asilimia 55, wahanga wakubwa ni vijana.

Kwa mujibu wa takwimu alizozitoa, amesema vijana zaidi ya 800,000 wanaingia kwenye soko la ajira nchini Kenya lakini wanaopata nafasi ni vijana 70,000.

Endapo mabadiliko hayo yatafanikiwa, nafasi 25,000 zinazotumikiwa na watumishi wa umma wenye umri kati ya 50-60, zitakuwa wazi.

Tamko hilo, limeungwa mkono na vijana wengi kwenye mitandao ya kijamii nchini humo wakidai kuwa litapunguza tatizo la ajira.

Hata hivyo, Tamko hilo huenda lisipite kwa urahisi kwani watu wenye umri mkubwa nchini humo, wameanza kuleta pingamizi

# AY anapokataa kama Dangote



MCHEKESHAJI kutoka Nigeria, AY ameyatoa ya moyoni baada ya kuwataka watu wafahamu kwamba si kila anapoombwa msaada anaweza kufurahia.

Amewataka watu hao kuona jambo hilo ni la kawaida kwani muda wote hawezi kusaidia na kuacha mambo mengine katika maisha yake.

Akitumia ukurasa wake wa Instagram aliandika ujumbe huo ambao ulisababisha mashabiki wake waupokee katika hali tofauti.



## Kumbe hamjui Burna Boy hatakagi kuremba!

MWANAMUZIKI Burna Boy amemkabili shabiki wake na kumwambia hana sura inayoweza kumvutia.

Burna Boy amekumbana na hali hiyo wakati akiwa nchini Marekani akifanya ziara yake ya kimuziki.


Katika tamasha lake lililofanyika Atalanta shabiki alijitokeza na kuanza kumghasi kwa maneno makali ambayo yalimsababishia kupandwa na hasira.

## Washiriki BBNaija wajadili ngono

WASHIRIKI wa shindano Big Brother Nigeria (BBNaija) wameingia katika hatua muhimu baada ya wiki hii kuitumia wakiwa wanajadili matukio ya ngono yanayotokea ndani ya nyumba.

Waliokuwa wakijadili suala hilo ni Seyi, Ike na Frodd ambao walizungumzia uhusiano wa kimapenzi ulivyotawala tangu waingie ndani ya nyumba hiyo siku 73 zilizopita.

Washiriki hao walianzia kujadili mapenzi ya Ike na Mercy, Seyi na Tacha na sasa Frodd na Esther.






## Hee! Tonto kwani kusema ukweli unaonaje?

MWIGIZAJI wa Nollywood,Tonto Dikeh, ameonekana kuchoshwa na maswali ya mashabiki wake ambao wanataka kujua maisha yake na mpenzi wake wa zamani.

Mrembo huyo akitumia ukurasa wake wa Instagram amesema amechoshwa na kauli za watu hao wanaodai kuwa mtoto wake amezaa na mwanamume huyo jambo ambalo halina ukweli.

Dikeh amesema anamheshimu mpenzi wake huyo kwa kumpatia furaha, lakini hakuwahi kupata naye mtoto kama watu wanavyodai.

## Peter umeyataka pambana mwenyewe

MWANAMUZIKI nyota kutoka Nigeria, Peter Okoye, amejitokeza kumtetea mmoja wa washiriki wa shindano la Big Brother Nigeria (BBNaija), akiwataka watu kutomhukumu kwani hakuna kiumbe kilichokamilika hapa duniani.

Okoye, alitumia mtandao wa kijamii kutuma maoni yake hayo akisema kama kuna watu wanambagua Tacha, basi ni vyema wajiangalie kama wamekamilika.

Hata hivyo wafuasi wake wengi wamemjia juu wakisema kauli yake hiyo ni wazi anamtetea mrembo huyo ambaye ameonekana kuwa na tabia za kushangaza ndani ya nyumba hilo.





## MIONZI YA SHERIA

Na John Juma
0716217615

# Wateja wanaweza kushtaki kampuni za huduma za simu

MARA nyingi nimekuwa nikiulizwa na wasomaji wengi swali hili , hivi ni mazingira gani kampuni za simu zinaweza kudaiwa fidia?

Leo ninaona nizungumze nawe msomaji wangu kwa kukufungulia mambo machache kuhusu huduma ya simu na iwapo unaweza kudai fidia kutoka kwa kampuni husika.

Kwa mujibu wa sheria hata kampuni za simu zinafanya makosa fulani hivyo hupaswa kuwajibika kisheria kwa kuwatendea kinyume na mkataba au mikataba ya huduma kwa wateja wao.

Siyo ajabu tena, siku hizi, kusikika mteja au wateja wa simu wakilalamikia baadhi ya kampuni zinazowapa huduma bila ya kujua nini wafanye, kuchukua hatua zaidi.

Ni watu wachache au pekee mno wenye uthubutu wa kuchukua hatua dhidi yao kwa kufungua mashauri ya madai ya fidia mahakamani kwa kampuni hizo kufuatia hasara au uonevu mkubwa au mdogo ambao mteja amesababishiwa.

Bila shaka hii ni kutokana na aidha walio wengi kutokana na kutokujua wanayo haki ya kudai fidia; au hata kama ni kweli, kwa kiasi fulani wanatambua juu ya hilo? Wanaamua kuacha tu, Mungu atawalipia.

Kwa nchi zilizokwishaendelea kama vile Ujerumani, Ufaransa, Marekani, Uingereza na baadhi ya mataifa ya Afrika mfano Nigeria na Afrika Kusini kampuni za simu zinalazimika kulipa fidia pale ambapo itathibitika mteja au wateja wao wametendewa kinyume na mkataba au mikataba ya huduma kwa wateja.

Bado isitoshe, raia mmoja wa nchini Nigeria, Edo Emeka, aliripotiwa kulipwa fidia ya Dola za Kimarekani 90,000, mara baada ya kufungua shauri la madai dhidi ya kampuni ya simu inayotoa huduma nchini humo.

Kufuatia kufungiwa namba au kadi (chip) yake ya simu bila ya sababu za msingi.

Katika shauri hilo, mlalamikaji Edo Emeka, aliieleza Mahakama Kuu ya nchi hiyo, mjini Lagos juu ya kufungiwa kadi na kueleza usumbufu alioupata kwa kitendo hicho cha kufungiwa namba yake na kupelekea kupata usumbufu mwingi.

Mara baada ya mahakama ya kujiridhisha, iliamuru tuzo (decree) mlalamikaji alipwe fidia ya Dola 90,000 ambayo ni takribani Sh. milioni 207.

### KUSHITAKI KAMPUNI

Kama wateja tunaweza kujiuliza ni makosa gani kampuni ya simu inaweza kushtakiwa nayo?

Tanzania, kama ilivyo kwa nchi nyingine zote duniani. Mara nyingi makosa yanayofanywa na kampuni ya simu, kwa wateja wao, yanafanana kwa kiasi kikubwa.

Mfano kukata salio la mtu bila sababu za msingi, kumwekea mtu mwito wa simu ambao mhusika mwenyewe hajaafiki, kutumia mziki au nyimbo ya msanii katika program yoyote kwa faida bila ya kufanya makubaliano kwanza, wakati mwingine kukata mawasiliano bila taarifa maalum kwa wateja, majenereta ya minara kusababisha usumbufu wa kelele kwenye makazi ya watu lakini pia fedha kuhamishwa kwa njia za muamala na zikapotea. Kupata ujumbe wa kidanganyifu kila wakati bila watuhumiwa kuchukuliwa hatua.

### TARATIBU ZA KUFUATA

Namna ya kufungua Mashtaka dhidi ya kampuni za simu huenda watu wengi hata nchi za nje walizishitaki kampuni ya simu wameshitaki katika kesi za madai. Kesi za madai ni zile ambazo hukumu yake kama mlalamikaji atashinda basi hutakiwa kulipwa kiasi fulani cha fedha. Malipo hayo yaweza kuwa ya fidia, usumbufu, gharama, kutegemea na mtu mwenyewe alichoomba kulipwa.

Kwa mfano kosa la kufungiwa namba. Imekuwapo tabia ya kampuni hizi kufunga namba ya mtu kwa kisingizio cha kuwa eti amekuwa haitumii laini hiyo kwa muda mrefu.

Wapo watu ambao huacha kutumia laini zao kwasababu za kuwa nje ya nchi na wengine huacha kutumia kwa ugonjwa wa muda mrefu hivyo hutumia kwa nadra. Hili linapaswa kuwa kosa iwapo sharti hilo lipo katika ile karatasi unayopewa wakati wa usajili wa laini.

Ni vema kujua kuwa karatasi unayopewa wakati wa usajili ndiyo mkataba wa makubaliano kati yako na kampuni ya simu. Ukiangalia karatasi za kampuni zote zilizoko nchini hakuna hata moja yenye maelezo ya kufungiwa kadi iwapo itakuwa haitumiki kwa muda fulani.


Hivyo ni kusema kuwa kitendo chochote cha kufunga kadi ni kufanya kosa na kusababisha usumbufu ambao unahitaji kufidiwa.

Pia kumwekea mteja mlio ambao mpigaji akimpigia anausikia wakati mteja hakuuomba ni kosa ambalo wakati mwingine humvunjia heshima mteja. Kwa kampuni za simu za Tanzania ni rahisi kumpigia simu kiongozi mwenye heshima zake ukasikia mwito wa nyimbo zenye maudhui ya kidini.

Halikadhalika, nyimbo za wasanii kutumika kibishara bila wao kutoa ridhaa ni kosa linalohitaji fidia. Kutokana na haya fungua kesi mahakama kuu, kesi hizi hufunguliwa mahakama za wilaya na mahakama kuu kulingana na kiwango cha hela unachodai.

Wakili mmoja jijini Dar es Salaam ameishtaki kampuni ya simu akidai kulipwa milioni 400 kwa kumfungia kadi alipokuwa nje ya nchi kimasomo. Na wewe pia waweza kufanya hivyo ili kupunguza usumbufu unaotokana na ama fedha kuhamishwa kijanja, kutumiwa ujumbe wa kuelekezwa kufanya jambo linalokukera ili kupunguza usumbufu unaosababishwa na watoa huduma za simu.

---



## KALAMU YA MWALIMU

Na Reubeni Lumbagala

# Ndiyo fimbo ya kuchapa ujinga, ufukara, magonjwa

BABA wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, katika jitihada za kuijenga upya Tanzania baada ya kuitoa mikononi mwa wakoloni, aliwataja maadui watatu wa maendeleo kuwa ni ujinga, umasikini na maradhi.

Aliendelea kusisitiza kuwa ni lazima maadui hawa watatu watokomezwe ili kuchochea kazi ya ukuaji wa maendeleo katika nchi yetu.

Kumekuwa na juhudi kubwa zinazofanywa na serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, asasi za kiraia na watu binafsi katika mapambano ya kutokomeza maadui hawa wa maendeleo.

Moja ya juhudi za kitaasisi zilizofanywa katika mapambano ya adui umaskini ni pamoja na kuanzishwa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf).

Tasaf ambacho ni kifupisho cha maneno Tanzania Social Action Fund yaani Mfuko wa Maendeleo ya Jamii, una madhumuni makuu ya kujengea uwezo jamii na wadau katika kuainisha matatizo, kuyachambua, kupanga mikakati na kutekeleza miradi ya maendeleo endelevu. Mchakato huu unawawezesha wananchi kuboresha huduma zao za kijamii na kiuchumi na hivyo kuchangia kupunguza umaskini.

Sambamba na hili, TASAF huwapatia fedha kaya maskini ili kuanzisha shughuli ndogo ndogo za kiuchumi na hatimaye kujinasua katika lindi la umaskini ambalo ni kikwazo katika ukuaji wa uchumi. Mfuko wa Tasaf umekuwa msaada mkubwa katika mapambano ya kuondoa adui umaskini na hatimaye kusongesha mbele gurudumu la maendeleo.

Ubunifu huu wa serikali wa kuanzisha mfuko wa Tasaf ni katika jitihada za kuhakikisha kuwa wananchi kutoka kaya maskini na wanyonge wanashirikishwa na kuwezeshwa kikamilifu katika kujikomboa na umaskini.

Jambo la kwanza linalofanywa na maofisa wa Tasaf ni kuzitambua na kuzisajili kaya masikini. Kazi hii hufanywa kwa umakini ili kuhakikisha wale wanaosajiliwa ni wananchi ambao wanaostahili kupata msaada kutoka serikalini ili kuwezeshwa kumudu maisha yao .

Viongozi wa serikali za mitaa hushirikishwa na kusaidia usajili wa kaya maskini.

Aidha, ukamilishaji wa zoezi la utambuzi na usajili wa kaya maskini, hufuatiwa na kujengewa uwezo kwa kaya maskini ili waweze kuzitumia vyema fedha watakazopewa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii katika uanzishaji na uendelezaji wa miradi midogo midogo ili kuweza kukuza kipato cha kaya na kwa maendeleo ya nchi.

Semina za kuwajengea uwezo kaya maskini huenda sambamba na kuwaonyesha fursa za kiuchumi ambazo wanafamilia wa kaya maskini wanaweza kuzianzisha katika ukuzaji kipato.

Mathalani uanzishaji wa miradi ya ufugaji wa kuku, mbuzi, ng'ombe, kilimo cha mbogamboga, upandaji miti ya matunda pamoja na mbao na biashara ndogondogo.

Maofisa wa Tasaf baada ya kuhakikisha elimu hiyo imeeleweka ipasavyo kwa wanufaika kazi ya kugawanya fedha au ruzuku za kunusuru kaya maskini huanza.

Kaya maskini hupata ruzuku kila baada ya miezi mitatu ili ziwasaide katika maisha yao na kwa uendelezaji wa shughuli zao walizozianzisha.

Tangu serikali ilipoanzisha mfuko wa Tasaf ambao ulianzisha program ya kugawa fedha ili kuzinusuru kaya maskini, kumekuwa na matokeo chanya kwa wanufaika wa fedha hizo.

Hii ni kutokana na matumizi mazuri ya fedha hizo katika mapambano ya adui umaskini pamoja na uibuaji wa vikundi na miradi mbalimbali ya kukuza uchumi katika maeneo wanayoishi wanufaika hao. Wanufaika hao pia wameweza kuboresha makazi yao kwa kujenga nyumba bora na imara.

Kupitia mfuko huo jamii imeweza kupambana na umaskini kwa kuhakikisha watoto wanaotoka kaya maskini wanawezeshwa kupata mahitaji muhimu ili kupata elimu bora.

Kuelimika ni njia mojawapo ya kupambana na adui umaskini. Wanufaika wa Tasaf kupitia ruzuku wanazopokea wameweza kusomesha watoto wao na hatimaye kusonga mbele kielimu, jambo linalochochea ongezeko la wasomi katika jamii na hatimaye kuondoa ujinga na umaskini katika jamii.

Ni muda muafaka kwa wanufaika wa mfuko huo kuendelea kuzitumia vyema fedha hizo katika mapambano ya umaskini.

Kila mnufaika wa mfuko wa maendeleo ya jamii ahakikishe kuwa hazitumii fedha hizo katika mambo yasiyo ya kimaendeleo kwani fedha hizo ni maalum kwa ukuzaji wa kipato na uchumi wa kaya na taifa.

Serikali iendelee kuujengea uwezo mfuko huo kwa kuupa fedha ili kuongeza wigo wa wanufaika.

Vilevile, serikali iwatumie vyema wataalam wa kuandaa miradi ya kimaendeleo katika kuzisaidia kaya maskini kukuza vipato vyao.

Ni dhahiri kuwa Tasaf ni ukombozi mkubwa kwa nchi yetu katika mapambano ya umaskini na ukuaji wa uchumi na ni ni nyenzo muhimu ya kuhakikisha kuwa nchi yetu inafikia dira yake ya maendeleo ya viwanda na uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025. Kupitia shughuli na miradi inayoanzishwa na kaya maskini, wanaweza kusaidia upatikanaji wa malighafi za kilimo na ufugaji katika kulishaji wa viwanda vyetu. Tafakari.

***Maoni (+255) 764 666349.***

# Haya yanakoleza unyanyasaji



Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Maendeleo ya Wazee, Wanawake na Watoto, Moudline Castico, akiangalia bidhaa za kazi ya mkono zilizotengenezwa na watoto katika maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika yaliyofanyika hivi karibuni katika Kijiji cha SOS Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

LICHA ya Zanzibar kuwa na sheria ya ushahidi namba 9 ya mwaka 2016, kesi nyingi za udhalilishaji wa kijinsia zimeendelea kufutwa mahakamani kwa kukosa ushahidi.

Mwanamke mmoja (jina linahifadhiwa) ambaye mtoto wake mwenye miaka 15 amebakwa na kupewa ujauzito , amekataa ushahidi mahakamani na kutaka kesi ifutwe.

Anachukua uamuzi huo baada ya kukubaliana na familia ya kijana aliyempa mjauzito binti yake kuwa wameafikiana kufunga ndoa.

"Tayari nimepokea mahari na mwezi ujao unaolewa hivyo sioni haja tena ya kuendelea na kesi maana mkwe wangu akifungwa mtoto wangu atakosa kuolewa,"alisema mama huyo wakati akizungumza na Nipashe.

Anaongeza :"Mtoto kakataa kusoma bora aolewe asije akaniletea tena mimba nyingine." Anasema mama ambaye mwanae ana miaka 15 na ambaye hajafikia umri wa kuzaa.

Anaeleza kuwa mwanzo alipogundua kuwa binti ana ujauzito, alikwenda kituo cha polisi kuripoti kesi hiyo na mtuhumiwa aliyempatia ujauzito binti yake alikamatwa baada ya msichana kumtaja.

Alisema wakati kesi hiyo ilipokua ikiendelea baada ya mtuhumiwa kupatikana, familia ya walalamikiwa pamoja na mtuhumiwa mwenyewe walimfuata na kutaka wasuluhishe na amepanga kumuoa.

"Kwa kuwa binti yangu mwenye yupo tayari kuolewa na kijana huyo tumeamua tumuozeshe na hivi tunajiandaa kwenda kufuta kesi", anasema mzazi huyu ambaye katika mahojiano anaelekea hajui hasara za ndoa za utotoni.

> **"Pamoja na changamoto za vitendea kazi lakini nayo jamii haitupi ushirikiano, utasikia DPP wanafuta kesi kumbe jamii yenyewe ndio inafanya hivyo, lazima jamii iamke kwani kufanya hivyo kunarejesha nyuma juhudi hizo.**

**MAONI YA BINTI**

Binti huyo anasema ameamua bora aolewe, maana analaumiwa mno kwa kupata ujauzito.

"Familia yangu inasema kuwa nimeyataka mwenyewe hivyo kwa kuwa aliyenipa ujauzito ameukubali na anataka kunioa nimeamua bora nielewe," anasema mtoto huyo. Msichana huyo ambae ametoroka shule akiwa kidato cha kwanza, ameamua kuungana na familia yake kuolewa ili kuwa mama japo ana umri mdogo.

**WADAU WALALAMA**

Kilio cha wanaharakati, Jeshi la Polisi, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Mahakama kuhusu kesi za udhalilishaji wa kijinsia ni wananchi wanaokataa kutoa ushahidi mahakamani.

Hali hiyo imekua ikiwapa mwanya wadhalilishaji kuendelea kudunda mitaani na wengine kudhalilisha watoto zaidi kwa sababu kesi nyingi zinakosa ushahidi wa kuwatia washtakiwa hatiani.

Kesi 910 za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia zimeripotiwa katika vyombo vya sheria Unguja na Pemba kwa mwaka 2018 na kati ya hizo 226 zimefutwa kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kukosekana kwa ushahidi.

Kesi hizo zimekua zikikosa ushahidi baada ya familia ya waathirika na familia ya mtuhumiwa wa udhalilishaji kukubaliana kwa kulipana fidia na kuzimaliza kesi hizo nyumbani licha ya kwamba zipo mahakamani.

Jaji wa Mahakama Kuu Zanzibar, Omar Othman Makungu, anasema muhali (kuoneana aibu) umetawala katika jamii hali ambayo ni changamoto katika kutokomeza vitendo vya udhalilishaji Zanzibar.

Anasema wananchi wanapopatwa na kadhia ya udhalilishaji, huwa na muamko wa kuripoti kesi hizo katika vituo vya polisi lakini mashtaka yakifika mahakamani huwa wagumu kutoa ushahidi.

Anasema kuwa sababu kuu ya kukataa kutoa ushahidi ni muhali ambapo wahanga wa matukio hayo wanahofia kutengwa au kusimangwa na familia zao.

Aidha, anasema kuwa baadhi ya watoto wanaodhalilishwa kwa kubakwa na kupewa ujauzito hufika mahakamani wakiwa wameshafungishwa ndoa na watuhumiwa na kukataa kutoa ushahidi na hatimae kesi kufutwa.

**KUKOSEKANA AMANI**

Mwanajuma Majid, ni Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, anasema kuwa kushamiri kwa vitendo hivyo vya udhalilishaji kunapoteza muelekeo wa taifa na kukosesha amani na usalama kwa watoto na jamii kwa ujumla.

"Sote ni mashuhuda kuwa hakuna hata siku moja ambayo itapita bila ya kusikia matukio ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia mjini na vijijini,"anasema Mwanajuma.

Hivyo, kuendelea kwa vitendo vya ukatili na udhalilishaji ni udhaifu katika malezi na mmong'onyoko wa maadili kwa mujibu wa maelezo yake.

Changamoto za upatikanaji wa takwimu kwa baadhi ya taasisi zinazoshughulikia kesi hizo ni tatizo na kuwataka wasimamizi wa taasisi zinazoshughulikia vitendo hivyo kushirikiana kwa karibu na ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali katika upatikanaji sahihi wa takwimu hizo.

Anasema takwimu sahihi zitatoa taswira halisi na kuweza kupanga mikakati madhubuti ya kudhibiti janga hilo.

Hakimu wa Mahakama ya Watoto Vuga, Naila Abdul Basit, anasema kuwa kesi nyingi za udhalilishaji zinakosa ushahidi jambo ambalo linapelekea kuzifuta.

"Mashahidi wanakuwa hawaji tena kesi iko katika hatua za mwisho, sasa sisi tutafanyaje kama watu hawataki kutoa ushahidi tutalazimika kufuta kesi", anasema Basit.

Sambamba na hilo anasema kesi nyingi za kutoroshwa au ujauzito, jamii imekuwa ikipatanisha na kusimamia kuoana hivyo kunakua hakuna kesi tena kwa sababu wanandoa wanakataa kushtakiana.

Khamis Juma kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, anasema sheria ya ushahidi namba 9 ya mwaka 2016 na sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai namba 7 ya mwaka 2018 zinasisitiza umuhimu wa kuwamo kwa ushahidi katika kesi za udhalilishaji ili ziweze kumtia mtu hatiani kwa mujibu wa sheria.

Anaeleza kuwa kesi bila ya kuwa na ushahidi inakuwa vigumu mshitakiwa kutiwa hatiani na kupewa adhabu inayostahiki.

"Shahidi ni mtu yoyote aliyoona tukio au kusikia ambapo makosa ya jinai yanatakiwa yapatikane ushahidi usiokua na shaka ili kuweza kuwatua hatiani washtakiwa,"anasema Juma.

**KUFUTA KESI**

Nassor Zahran, wakili kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, anasema kuwa baadhi ya watu wanaofungua kesi hufika ofisini kwao na kufuta kesi jambo ambalo linarejesha nyuma mapambano dhidi ya udhalilishaji.

"Pamoja na changamoto za vitendea kazi lakini nayo jamii haitupi ushirikiano, utasikia DPP wanafuta kesi kumbe jamii yenyewe ndio inafanya hivyo, lazima jamii iamke kwani kufanya hivyo kunarejesha nyuma juhudi hizo", anasema.

"Wakati mwingine hata ukimtafuta huyo mshtakiwa humpati kwa njia yoyote ya mawasiliano. Tunalazimika kuliondoa shauri, kotini lakini mtu kama hajui hilo anatupa lawama kwa ofisi ya DPP", anaongeza wakili huyo.

Jamal Himid , kutoka dawati la jinsia la kituo cha polisi Mwera, anasema ipo haja ya serikali kuwashtaki wale ambao wanakataa kutoa ushahidi wa kesi za udhalilishaji.

"Hili janga litaendelea kutuandama ikiwa kila muhusika wa kesi atakataa kutoa ushahidi, hili bado ni tatizo kubwa, kesi haziendi mbele", anasema.

Ofisa Miradi wa Chama cha Wanahabari Wanawake (Tamwa) Zanzibar, Asha Abdi Makame, anasema kuwa licha ya juhudi kubwa zinazochukuliwa katika kukabiliana na matendo ya udhalilishaji, bado vitendo hivyo vimekuwa vikiibuka kila siku.

MAKALA

# Mbongo anavyosheheni tamaduni za kigeni jikoni

Na Mwandishi Wetu

ZAMA hizi ukiingia jikoni kwa mama au binti Mtanzania au Mbongo unaweza ushindwe kutofautisha kati ya jiko lake na la raia wa kigeni.

Kwanini? Vifaa vya asili na mpangilio, vimetoweka, hakuna kata ya maji, vyungu, vikaango, pawa, vijiko vya asilia hata ungo. Vifaa hivyo vina nafasi kubwa katika majiko na mapishi pia kuutambulisha utamaduni wa Mtanzania.

Kiwe kijiko au upawa wa mbao au wa kifuu ni bidhaa adimu mijini na kwa kifupi vimetoweka kwenye macho ya wengi hasa wakazi wa mijini na sasa kinachosikika ni 'ladow ' au 'serving spoon' zilizotengenezwa kwa bati au plastiki. Tena zikitoka ughaibuni na zikiagizwa kwa fedha za kigeni.

Tukibaki na mjadala wa upawa , zama hizi plastiki ndizo zinazotumika iwe nyumbani kwenye familia , kwa mamalishe, migahawani na kwenye hoteli kubwa za kitalii.

Mtanzania usiukimbize upawa au kijiko cha asili, bado vina nafasi ya kipekee jikoni kwako. Haipendezi kukoroga juisi na vijiko vya bati au platisiki tumia miti, upawa na mwiko ndiyo marafiki zako hapa.

Si jambo la kufurahia upawa ukitoweka kwa vile ni kupoteza ajira kwa wale mabingwa wa saa za kuchonga wanakosa kazi , wanabakia kuchonga miko na pengine vibao vya kukunia nazi kwa kuwa kibao cha chapati nacho kinatoka ng'ambo.

Licha ya sanaa na mambo ya kale kama uchongaji wa vijiko, miko na pawa kuwa utambulisho wa taifa, pia ni sehemu ya kujenga na kukuza vipaji kwa vijana na kuongeza ajira.

Upawa ni kama mwiko, kila jiko utaukuta, matumizi yake yanaanzia kwenye kupakua, kukoroga, kuchota uwe unga au mafuta, chumvi na sukari jikoni lakini si hapo pekee hata kwenye biashara upawa ni kipimo.



Kuna usemi kuwa jasiri haachi asili, hivi kusahau upawa, kata na vyungu vya jadi si kudharau na kuacha asili ya Mta zania. Vifaa kama hivi jikoni au sebuleni kwako pamoja na kutumika kupikia pia ni urembo. **PICHA MTANDAO**





### KAZI ZA UPAWA

Upawa ni mahususi kukorogea na kuchotea mchuzi, uji, dawa na vyakula mbalimbali vya maji maji na hupendeza zaidi ukitumiwa. Si kama 'ladow' au upawa wa plastiki ambao huchubuka, kupauka na hata wakati mwingine kutoa kemikali za sumu kwenye vyakula.

Tena zama hizi wataalamu wanashauri kuachana na vyombo vya plastiki ambavyo huenda vinapopata moto husababisha sumu inayoweza kusababisha saratani.

Upawa hutengenezwa kwa kifuu hasa ukanda wa pwani, kuna mianzi na mbao kadhalika huwekewa kijiti ambacho ndicho mpini au kikamatio.

Huko Zanzibar na Pemba uchongaji pawa ni maarufu na sehemu nyingine za mwambao wa pwani husussan Tanga, Bagamoyo na hata Lindi ambako kila kwenye wazee utakuta upawa unachongwa ama unatumiwa.

Ukweli uliopo sasa ni kwamba upawa wa asili unaotengenezwa kwa kifuu umeanza kupoteza umaarufu na hautumiki na watu wengi .

Lakini pia hata nazi zimetoweka kutokana na kuadimika kwa kiungo hicho cha mafuta hasa ukanda wa pwani ikiwamo Zanzibar kulikosababishwa na uharibifu wa mazingira na kukata minazi ovyo ama kuitumia zaidi kwenye madafu na kwingineko ukigemwa kuzalishapombe ya mnazi.

Upawa wa kifuu au mti muhimu kiafya kwani hauna kemikali wala madhara kutokana na malighafi yake kuwa asilia.

Jamii hii ya kijiko kikubwa hutengenezwa zaidi vjijini kwa upande wa Zanzibar ni visiwani Unguja na Pemba na wahusika wakubwa ni wazee wa rika za kati, ambao wanaifanya kazi hii kama sehemu ya kujipatia riziki.

Kwa Tanzania Bara ni ukanda wote wa pwani kuanzia Tanga hadi Mtwara. Tena kwa kusini kuna upawa na miiko bomba myeusi inayotengenezwa na Wamakonde ambayo pengine asili yake ni mpingo.

Kuchonga na kuremba upawa utengenezaji wake ni wa kiasili kuna kuchonga kwa kutumia zana za asili kama panga ambalo hukata miti , kuchimba na kipande cha chupa kuulainisha na pia msasa hutumiwa kuweka shoo au umaridadi zaidi ili uwe mwororo.

Kwa upande wa upawa wa kifuu kazi si ngumu kinachojiri ni kuulanisha zaidi kwa kuwa kifuu kipo tayari kutumika.

Kijiko hiki ni muhimu hivyo ili kuweza kuuenzi utamaduni wa kutumia upawa na kuhakikisha unabakia, kuna haja kwa watengenezaji ambao wengi ni wenye kipato cha chini kuongeza ujasiriamali, kurembesha na kuboresha upawa ikiwa ni pamoja na kutengeneza vijiko vya miti vinavyoweza kutumiwa na watalii.

> **Ubunifu nao ni muhimu kama ilivyo kwa wakazi wa Iringa na Bukoba mianzi inaweza kutumiwa kuzalisha pawa hizo.**

Lakini pia kuna haja kwa serikali kusaidia wananchi kuimarisha kilimo cha miti kama mipingo, mikurunge na hata minazi kwa sababu inaweza kutumiwa kwenye uzalishaji wa vijiko hivyo.

Ubunifu nao ni muhimu kama ilivyo kwa wakazi wa Iringa na Bukoba mianzi inaweza kutumiwa kuzalisha pawa hizo.

Pamoja na upawa kuna haja ya kutumia pia vijiko vya asili si lazima kulia misosi lakini hata pia kupamba nyuma na makazi mijini na vijijini.

Msemo kuwa jasiri hasau asili , uwakumbushe Wabongo kupenda 'vitu vyao'. Pengine haipendezi kwa zama hizi watu wakitaka kuona kijiko cha asili inawalazimu kwenda Nyumba ya Makumbusho ya Taifa, kuvitizama.

Chonde ujasiriamali unapotumiwa ni chanzo cha kufufua na kuendeleza utamaduni pamoja na uchumi wa vijana na wazee.

# TMA inavyojizatiti kulifikisha kwenye uchumi wa viwanda




Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Issack Kamwelwe (wa pili kulia), akinyanyua cheti kuashiria uzinduzi wa Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) kwenye hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni, kushoto kwake ni Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Dk Agnes Kijazi. **NA MPIGAPICHA WETU**



Mvua, ukame na taarifa za mafuriko ni baadhi ya mambo muhimu kwa wananchi ili wachukue tahadhari. **PICHA MTANDAO**

**Na Faustine Feliciane**

MIAKA ya karibuni mabadiliko ya tabianchi yamekuwa kitisho kipya cha mazingira kinachokabili dunia. Taathira yake inaonekana kwenye mabadiliko ya hali ya hewa yanayoleta, ukame, mafuriko, vimbunga na hata ongezeko la viuatilifu.

Kwa Tanzania suala la hali ya hewa ni kipaumbele na kipo chombo cha kuratibu na kutolea maelezo ya masuala ya hali ya hewa kabla ya kumfikia mwananchi.

Kikiwa kimeundwa mwaka 1999 kilijulikana kama Wakala wa Hali ya Hewa Tanzania sasa mabadiliko yameendelea kufanyika na kinaitwa Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA).

> “Tulipokuwa wakala, tulipata mafanikio makubwa ambayo yanahitaji kuendelezwa...

TMA imeboreshwa ili kuendelea kuwapa Watanzania taarifa za hali ya hewa yenye usahihi mpaka kufikia kati ya asilimia 87 hadi 96 kama ambavyo Mkurugenzi wa TMA, Dk Agnes Kijazi anavyobainisha.

“Tumepitia vipindi vingi mpaka kufikia sasa kuwa mamlaka kamili, usahihi wa utabiri wetu unazidi kuimarika na sasa kwa kufikia hapa tupo kati ya asilimia 87-96. Ni mafanikio makubwa ukilinganisha na kiwango cha usahihi wetu hapo awali kuwa asilimia 75,” anasema Dk Kijazi.

“Tulipokuwa wakala, tulipata mafanikio makubwa ambayo yanahitaji kuendelezwa tunapofikia hatua ya kuwa mamlaka, tunaendelea kujivunia mambo makubwa ikiwa ni pamoja na kutambulika kimataifa,” anaongeza Kijazi.

## KUTAMBULIKA KIMATAIFA

Mkurugenzi wa TMA imepata vyeti vya ubora vya utoaji wa huduma za hali ya hewa kwa viwango vya kimataifa katika sekta ya usafiri wa anga na wanatambulika kwa cheti ISO 9001:2008 ambacho kilipatikana mwaka 2011.

Anasema Tanzania ilikuwa nchi ya kwanza kwa taasisi za hali ya hewa Kusini mwa Jangwa la Sahara kupata cheti hicho na ISO 9001:2015 ambacho kilipatikana mwaka 2017 na Tanzania ilikuwa nchi ya tatu Afrika kupata cheti hicho.

Anaongezea kusimikwa kwa mitambo miwili ya radar mbili za hali ya hewa na rada nyingine tatu zikiwa katika hatua ya ununuzi. Aidha, wakala unaendelea kuwa taasisi ya kiungo ya kuratibu taarifa za matukio ya tsunami nchini (National Tsunami warning Centre).

Anaiambia Nipashe kuwa wataalamu wa wakala wametoa mchango mkubwa wa kitaalamu katika Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) na kuzisaidia baadhi ya nchi wanachama wa WMO ndani na nje ya Afrika kuboresha huduma za hali ya hewa katika mataifa yao.

Dokta Kijazi anasema: “Mafanikio mengine ni pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa TMA, kuchaguliwa kuwa Makamu wa Tatu wa Rais wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO).”

## WANANCHI WAAMKA

Umuhimu wa wananchi kufuatilia taarifa za hali ya hewa za TMA ni jambo la kufurahia pia kwa mamlaka hiyo, anasema Dk. Kijazi.

Kama ambavyo Waziri wa Ujenzi,Uchukuzi na Mawasiliano, Isaack Kamwelwe, alivyosema wakati wa kuizindua rasmi mamlaka hiyo, taarifa za hali ya hewa ni muhimu kwenye sekta ya uchumi wa mtu na taifa , anaongeza.

“Taarifa za hali ya hewa zinaweza kusaidia kuifikisha nchi kwenye uchumi wa viwanda na hivyo nchi kuwa kwenye uchumi wa kati kama ilivyo sera ya serikali, kila mmoja anazihitaji taarifa hizi kuweza kufanya shughuli zake kwa ufanisi,” anasema Waziri Kwamwelwe.

Dokta Kijazi, anasema kama wananchi watafuatilia kwa karibu na kufuata ushauri unaotolewa watajiweka mbali na majanga na kadhia inayoweza kuwapata kutokana na athari za hali ya hewa.

“TMA tunatoa taarifa za hali ya hewa kwa vipindi tofauti tofauti, ni muhimu sana kwa wanachi kufuatilia kupitia vyombo vya habari. Hii itamsaidia kupanga shughuli zake kutokana na kile watakachoambiwa na mamlaka,” anasema Dk. Kijazi.

## KUFIKIA VIWANGO

Mkurugenzi wa TMA anasema taarifa za mamlaka zina usahihi na kila wanachokitabiri kinatokea kwa asilimia kubwa na hivyo wamekuwa watu muhimu kwa maendeleo ya taifa.

Dokta Kijazi anaeleza kuwa malengo yao ni kufikia kiwango cha utabiri kwa usahihi kwa asilimia 100 na jambo hilo linawezekana kutokana na ushirikiano wanaoupata kutoka serikalini na watumishi wa chombo hicho wanavyojituma.

## HABARI KIMATAIFA

# Familia kumzika Mugabe katika uwanja wa mashujaa

**HARARE, ZIMBABWE**

MWILI wa aliyekuwa rais wa Zimbabwe Robert Mugabe, utazikwa kifamilia katika viwanja vya mashujaa, karibu na mji wa Harare, mmoja wa wanafamilia ameiambia BBC.

Leo Mugabe, msemaji wa familia, alieleza kuwa mazishi hayatafanyika siku ya Jumapili kama ilivyokuwa ikitarajiwa, badala yake mwili wake utapelekwa katika kijiji alichozaliwa cha Kutama.

Huko Kutama machifu na wazazi watapata nafasi kufanya shughuli za kimila na siku ambayo haijatajwa mwili wa Mugabe aliyefariki juma lililopita akiwa na miaka 95 utazikwa katika uwanja wa mashujaa jijini Harare. Eneo hilo ndilo serikali ililokuwa inalitarajia kumuhifadhi kiongozi huyo wa zamani na mpigania uhuru maarufu wa taifa hilo.

Ilionekana kuwa walifikia muafaka baada ya siku kadhaa za mjadala mkali na inadaiwa kuwa kumekuwa na mvutano kati ya familia ya Mugabe na wale waliomshinikiza aondoke madarakani kwa mapinduzi ya Novemba mwaka 2017.

Awali, Familia ya Robert Mugabe ilisema imeshtushwa kwa kutoshauriwa na serikali kuhusu mipango ya mazishi ya aliyekuwa rais huyo.

Mugabe, alifariki wakati alipokuwa nchini Singapore akipata matibabu na mwili wake unatayarishwa kulazwa ili kupewa heshima za mwisho kitaifa katika uwanja wa soka katika mji mkuu wa Zimbabawe wa Harare.

Familia yake na serikali zilitofautiana kuhusu sehemu atakapozikwa, familia inasemekana kuwa na uchungu kwa namna Mugabe alivyotimuliwa na aliyekuwa mshirika wake Mnangagwa miaka miwili iliyopita.

Mugabe alimfuta kazi wakati huo makamu wake ambaye sasa ni rais wa taifa hilo, Emmerson Mnangagwa.

Mnangagwa mwaka 2017, katika kile ambacho wengi waliamini ni njia ya kumtayarisha mkewe Mugabe Grace kumrithi, alitimuliwa kazi. Mugabe alikuwa kiongozi wa kwanza wa Zimbabwe baada ya taifa hilo kupata uhuru mwaka 1980. Alishikilia madaraka kwa takriban miongo minne kabla ya kutimuliwa katika mapinduzi baridi ya mwaka 2017.

Baadhi ya maneno ambayo Mugabe aliyowahi kuyasema dhidi ya bara la Ulaya kuhusu nchi yake.

"Zimbabwe ni huru kwa sababu watu wake wako huru na watu wake wanapaswa kuwa huru daima"

"Sisi si watu wa Ulaya, hatujawahi kuomba hata sehemu ndogo ya Ulaya, Blair kaa na Uingereza yako na mimi niache nibaki na Zimbabwe yangu"

Awali Mugabe alisifiwa kwa kupanua sekta ya afya na elimu kwa weusi walio wengi, baadaye alitumia ghasia dhidi ya wapinzani wake na kuongoza uchumi wa taifa hilo ulioanguka vibaya.

"Hawawezi kuanzisha demokrasia hapa, sisi tumeanzisha demokrasia"

"Hii ni ardhi ya mtu mweusi hivyo ni mtu mweusi ndiye mwenye haki ya kuamua nani akae na nani asikae"

"Tuna ardhi yetu na katika ardhi yetu ndiko tutapata fedha"

Mugabe alikuwa maarufu miongoni mwa wapiga kura wengi hata katika kipindi chake cha hivi karibuni alipong'atuliwa madarakani.

***BBC***



Waombolezaji wakiangalia picha za Mugabe katika mitaa mbalimbali ya Harare ikiwa ni namna mojawapo ya kumuomboleza. **PICHA:MTANDAO.**

# Mdahalo Wanademocrat wajikita bima ya afya

**TEXAS, MAREKANI**

KWA mara ya kwanza, washindani wakuu wa chama cha Democratic nchini Marekani wanaotaka kuwania urais wameshiriki mdahalo wa pamoja. Joe Biden, Elizabeth Warren na Bernie Sanders ni miongoni mwa wawaniaji 10 walioshiriki.

Wanawasiasa wanaowania kupeperusha bendera ya chama cha Democrat katika uchaguzi wa rais nchini Marekani mwaka ujao, walishiriki mdahalo wa tatu usiku wa kuamkia jana. Kwa mara ya kwanza mdahalo huo uliwaleta pamoja washindani wakuu wa chama hicho, waliochuana juu ya masuala muhimu ya kisera ikiwemo kuhusu bima ya afya na mabadiliko ya tabianchi.

Miongoni mwa wagombea 10 walioshiriki mdahalo huo ulioandaliwa Houston jimbo la Texas, ni pamoja na makamu wa zamani wa rais chini ya utawala wa Barrack Obama Joe Biden, ambaye uchunguzi wa maoni umemweka mbele ya wagombea wengine wote wa chama hicho, pamoja na washindani wake wa karibu Bernie Sanders na Elizabeth Warren.

Tofauti kati ya wazi yadhihirika miongoni mwa wawaniaji

Japo wagombea hao wa chama cha Democratic wameonyesha nia moja ya kumuondoa Rais Trump madarakani, pamoja na haja ya dharura ya kukabili mabadiliko ya tabianchi, tofauti zao zilidhihirika wazi kuhusu suala la mageuzi katika bima ya afya nchini humo.

Mara kwa mara Joe Biden alikabiliana vikali na washindani wake wakuu kuhusu bima ya afya. Aliwashutumu maseneta Bernie Sanders na Elizabeth Warren kwa kufuatilia ndoto hiyo bila ya mipango ya kuifadhili.

Warren ambaye amekuwa akishangiliwa sana katika kampeni zake kwenye kumbi mbalimbali kando na sera zake za kuwavutia wafuasi wengi, alisema anafahamu kile ambacho kimeharibika na anajua namna ya kukishughulikia na ataongoza kuhakikisha hilo limetekelezwa. Ameongeza kuwa matajiri ndio watagharamia zaidi bima ya afya.

Naye Sanders anayependekeza kuachana na bima binafsi ya afya ameapa kuhakikisha, hatimaye kila raia wa Marekani atapata huduma ya afya kama haki ya msingi ya binadamu.

Masuala mengine kama uhamiaji, udhibiti wa umiliki wa bunduki, uchumi na hata biashara pia yalijadiliwa huku kila mmoja akijaribu kunadi sera zake na kujitetea dhidi ya ukosoaji.

Kuhusu mvutano wa kibiashara kati ya Marekani na China, wawaniaji hao waliahidi kuiwajibisha China kutokana na mbinu zake za ufisadi.

Lakini kando na kukosoa vita hivyo vya Trump na China hakuna hata mmoja aliyedokeza kwamba atashughulika kupata suluhisho la haraka akichaguliwa.

***DW***

# Spika Uingereza amuonya Johnson

LONDON, Uingereza

SPIKA wa Bunge la Uingereza John Bercow, amemuonya Waziri Mkuu Boris Johnson kuhusu kutoheshimu sheria kwa kukataa kuomba kusogezwa mbele muda wa nchi hiyo kujitoa Umoja wa Ulaya ama Brexit.

Spika huyo ameapa kupinga jaribio lolote linalonuia kulikwepa Bunge. Kulingana na shirika la habari la Press Association la Uingereza, spika huyo wa bunge alisema kutoheshimu sheria kunaweza kuwa mfano mbaya kabisa utakaoonyeshwa mbele ya umma.

Bercow alionya kwenye hotuba yake jijini London kwamba iwapo serikali itakaribia kufanya hivyo bunge litatumia nguvu zake zote kuondoa uwezekano huo. Matamshi yake yanakuja baada ya Waziri Mkuu Johnson kukanusha shutuma kuwa alimdanganya Malkia Elizabeth kuhusu kuomba kuvunjwa bunge mwezi huu.

Bunge, mapema mwezi huu lilipitisha sheria iliyolenga kuzuia Brexit bila ya makubaliano ingawa Johnson anasisitiza kuondoka kama ilivyopangwa awali Oktoba 31, kwa makubaliano ama bila ya makubaliano.

**DW**



Spika wa Uingereza John Bercow, akitoa maelekezo bungeni wiki hii. **PICHA: DAILY TELEGRAPH.**

# HADITHI

WASWAHILI wana msemo wao unaosema kuwa ufukara ni jereha la ulimwengu. Wakiwa na maana, mtu fukara mara nyingi hukutana na mitihani mikubwa duniani, ambayo mingi husababishwa na baadhi ya binadamu, wengine wenye vipato kwa kuwaona hawana thamani na hawahitajiki kuwa na kitu chochote cha thamani. Kijana anayetoka kwenye familia duni Kadili, anatokea kupendwa na msichana mrembo anayetoka kwenye familia ya kitajiri, Edina.

# Jumba Jekundi-18

**Na Adam Fungamwango**

(0716 350534)




Lakini kitendo hicho kinamsababishia kijana huyo matatizo makubwa ambayo hajawahi kuyapata katika maisha yake, kiasi cha maisha yake kuwa hatarini. Fuatilia mkasa huu wa aina yake.

"Binti yangu bado mdogo, halafu kifaa cha nguvu. Si unamuona? Huyu si msichana wa kuolewa na mtu kapuku kama wewe. Kula yako na vaa yako shida huyu unamuweza wewe? Hapa unaponiona, kichwa kinaniuma, maana wanaume kibao wenye wadhifa na pesa zao wametuma washenga kutaka kumuoa binti yangu, yaani sijui nimkubali nani nimuache nani. Halafu kanatoke kajitu kama wewe nako, eti nako kanajitia kutaka kupimana ubavu na watu hao," Alisema na kuonekana kama kuutua mzigo mzito uliokuwa kwenye kifua chake.

Kuna mawaziri, mapofesa, madaktari na wafanyabiashara wakubwa nchini mpaka watoto wa vigogo wanataka kumuoa Edina, hadi marubani wa ndege. Lakini kwa sababu ni lazima aolewe na mtu mmoja, nimetuliza kichwa ili nione kati ya hao nani anaweza kuwa mtu sahihi kwa binti yangu ili asiende kupata tabu kwa sababu mimi mwenyewe mama yake nimemzaa na kumlea kwa mapenzi makubwa. Amelelewa kitajiri na hajawahi kupata shida yoyote."

Kwa mara ya kwanza ndipo Kadili alipojua kuwa kumbe Edina hajaolewa kama walivyokuwa wakidhani na rafiki yake Meze na kwamba hata kule kulindwa na mabaunsa si kwa sababu ya wivu wa mwenye mali, bali ni mama yake ndiye aliyekuwa akimlinda binti yake na watu watakaoonekana kutaka kumrubuni binti yake.

"Hawa mabaunsa ndiyo waliokuja kumwambia huyu mama mambo yote yale, ndiyo maana nimeletwa huku." Kadili alijisemea mwenyewe moyoni.

"Sasa sikiliza we mbwa mtoto. Nisikilize kwa makini. Leo nakusamehe kwa sababu binti yangu Edina amelia sana kwa sababu yako ili usiuawe. Saa hizi tayari ungekuwa umeshawasili kuzimu. Yoyote anayeingia kwenye jumba hili kwa sababu kama zako, au zingine za utovu wa nidhamu huwa hatoki salama. Nadhani ulitembezwa kwenye yale makaburi ya wajinga wenzako. Kuanzia leo sitaki umfuatilie tena mwanangu. Umuogope kama ukoma. Sitaki kusikia habari zako tena hapa. Nikisikia chochote kile juu yako na binti yangu, au kutoa siri ya hiki kilichomo kwenye nyumba hii, basi tusilaumiane. Kwa sababu ni lazima uuawe. Haya toeni hii taka taka mkaitupe huko." Aliamrisha.

> **"Leo nakusamehe kwa sababu binti yangu Edina amelia sana kwa sababu yako ili usiuawe. Saa hizi tayari ungekuwa umeshawasili kuzimu. Yoyote anayeingia kwenye jumba hili kwa sababu kama zako, au zingine za utovu wa nidhamu huwa hatoki salama."**

*************************************

Hakuamini kama yuko tena huru. Hakuamini kama yuko hai. Tayari moyo wake ulishakufa ganzi na kujiona ni kama mfu, lakini tu anayesubiri kuuawa rasmi.

Ni baada ya kuteremshwa Kijitonyama maeneo ya Sayansi, karibu wa Wizara ya Sayansi na Telnolojia. Watekaji alimteremsha kwenye kona ya barabara inayokwenda Kijitonyama, Tandale na Magomeni na ile inayokwenda Mwenge.

Ilikuwa ni saa moja usiku. Hakuhitaji chochote kile zaidi ya kuifuata barabara inayokwenda Tandale na Magomeni, taratibu alianza kutembea kwa miguu kurudi kwao.

Hakuwa na wasiwasi wa kitu chochote kwani asingeweza kutekwa tena. Hakudhani kuwa kibaka, mwizi yoyote atakayemvaa hapo anaweza kuwa hatari zaidi kama wale waliomuachia. Alijihisi mwenye bahati ya mtende.

"Leo nakusamehe kwa sababu binti yangu Edina amelia sana kwa sababu yako ili usiuawe. Saa hizi tayari ungekuwa umeshawasili kuzimu. Yoyote anayeingia kwenye jumba hili kwa sababu kama zako, au zingine za utovu wa nidhamu huwa hatoki salama."

Sauti hiyo ilikuwa ikimjia na kutoka kichwani. "Ina maana nimekuwa hai kwa sababu ya Edina?" Aliwaza na kujiuliza kwa pamoja.

"Vinginevyo ningezikwa hai ndani ya lile jumba jekundu. Lakini mbona huyo Edina ndiyo aliyeniuza kwa kusema kuwa mimi ni mpenzi wake? Kama asingesema hivyo, haya yote yangetokea?" Alizidi kujiuliza maswali ambayo hayakuwa na majibu.

Mawazo tele kichwani ya yale yote yaliyotokea, kutekwa, kuteswa vikali, kudhalilishwa na kubaguliwa utu wake, vilimfanya ajione mzito kama vile dunia yote amaibeba kichwani.

*********************************

Kwa siku mbili nzima Mama Kadili hakupata usingizi. Bauansa walimwambia anamchukua na wangemrudisha. Haikuwa hivyo. Hakukuwa na dalili za mwanaye kwa kiume pekee kurejea.

Hakuwa kwenye hali nzuri. Hata hivyo siri hiyo alibaki nayo yeye peke yake. Hakutaka kuisema kwa mtu yoyote. Hakutaka watu waitangaze na kumtia presha zaidi. Lolote likitokea, basi iwe ni yeye na mzigo wake. Hata mabinti zake Halima na Ashura hawakujua kaka yao yuko wapi. Lakini kwa sababu ni mtoto wa kiume hakutaka kuuliza sana.

Kwa mara ya kwanza, mama Gombea ambaye mtaani hapo anasifika kwa umbea, hakujua chochote kuhusu tukio la Kadili kuchukuliwa nyumbani na watu wasiojulikana na kwa muda wa siku mbili hajaonekana nyumbani.

"Hata kama mwanangu Kadili wamemuua ni bora wakanirudishia maiti yangu nimzike mimi mwenyewe." Alilia peke yake usiku kwa maumivu.

Akiwa nje amepumzika kwenye mkeka wake. Kwa mbali, pamoja na macho wake ya uzee aliona kama kuna mtu ana utembeaji kama wa mwanaye Kadili.

Alipokuwa akizidi kuwa karibu ndipo alipokuwa akimuangalia kwa makini zaidi. Taa za umeme zilizokuwa nyumba jirani zilimfanya mama huyo kuona kama mzimu wa mtoto wake ukimjia.

Hakuamini kwa muda huyo, ikienda saa mbili na kitu hivi kumuona mtoto wake akirejea, tena mwenyewe, badala ya jina la marehemu.

Moyo ulimpiga alipoona mtu yule akiwa anatembea taratibu kuelekea kwenye nyumba ile ile yake.

"Ni kweli Kadili huyu." Alijiuliza. Alinyanyuka kwenye mkeka na kubaki amesimama akiwa amepigwa na bumbuwazi.

"Mama." Sauti ya Kadili ilipenya kwenye masikio ya mama yake.

Alikuwa ametanua mikono yake ili amkumbatie mama yake. Mama naye kama vile aliyekuwa ametoka kwenye usingizi mzito baada ya kuisikia sauti ile ambayo aliamini ni ya mwanaye, japo ilionyesha uchovu.

"Mwanangu Kadili ndiyo wewe."

"Ndiyo mimi mama."

"Uko hai mwanangu."

"Niko hai mama, ndiyo maana nimerudi."

"Najua umepitia kipindi kigumu sana siku hizi mbili, lakini karibu nyumbani baba."

"Ahsante mama."

Wakati huo Kadili na mama yake walikuwa wamekumbatiana mithili ya mtoto aliyerejea kwa mzazi wake baada ya kuondoka hapo zaidi ya miaka 10 iliyopita bila mawasiliano yoyote.

***ITAENDELEA JUMAMOSI***

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA / MASHAMBA

**SHAMBA LENYE NYUMBA NDANI LINAUZWA,** Liko eneo la Lumumba Pangani mkoa wa pwani. Lina ukubwa wa heka mbili. Kwa Mawasiliano 0767332830, 0686137871, 0686807366


NIPASHE NI JIBU LAKO


NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,

au piga simu: 0767 223311


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAMBO YA NDANI
IDARA YA UHAMIAJI

**MAOMBI YA URAIA**



**MELODY MUFARO KUTCHWA** mwenye picha hapo juu anaomba uraia wa Tanzania kwa Mh. Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Utaifa wake wa sasa ni MZIMBABWE. Nchi atokayo ni ZIMBABWE. Anwani ya Mwajiri S.L.P 72776. Yupo hapa nchini tangu 2011. Kwa yeyote mwenye taarifa/sababu za kwanini mwombaji asipewe Uraia wa Tanzania, atume taarifa ya maandishi kwa Kamishna Jenerali wa Uhamiaji S.L.P 512, Dar es salaam. Kumb. Na. DN. 704090.

Kny: KAMISHNA JENERALI WA UHAMIAJI

115419002

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA
USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI YA 2
Katika mahakama ya mwanzo
MJINI MOROGORO

**Usimamizi wa mirathi No; 185/2019**

Ombi la **HAMISI ISSA NGEDERE** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **MTORO RAMADHANI ATHUMANI**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 24/09/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 12/09/2019.

115418702

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA
USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI YA 2
Katika mahakama ya mwanzo
MJINI MOROGORO

**Usimamizi wa mirathi No;182/2019**

Ombi la ANWAR ALI KHAN Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **ABDALLAH MAHMOOD KHAN**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 08/10/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 12/09/2019.

115418902

## HATI YA KIAPO

Mimi **MICHAEL MBOGO** wa S.L.P 992, Tanga, Mkristo, mtu mzima na mwenye akili zangu timamu, Nathibitisha katika kiapo changu hichi na kuyatamka haya yafuatayo na kama ifuatavyo:-

Kwamba **OFFER YANGU, NINATHIBITISHA KUWA IMEPOTEA MIKONONI MWANGU MIMI.**

Kwamba nimejaribu kuitafuta kwa juhudi zangu zote sikufanikiwa, Nimetoa taarifa Polisi na kupatiwa TAN/RB/290374/2019 ya tarehe 10/09/2019.

Kwamba Naiomba Ofisi ya Mipango Miji Pamoja na Polisi Mkoa wa Tanga itambue upotevu huu na ninathibitisha imepotea mikononi mwangu mimi muapaji, na niko tayari kulipia gharama na kodi zote husika za serikali.

Nakiri na kuapa kiapo hichi na kuyatamka haya yote nikiwa na akili zangu timamu na bila ya kushawishiwa na mtu yoyote yule na kukiri kwa kuweka saini yangu hapa chini kama ifuatavyo:-

115419202

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

MAJID ALI NASSOR anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 742 DEF TOYOTA SIENTA.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: DAR/OST/R-B/288319/2019.

115418102

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
JUDICIARY
NOTICE TO RESPONDENT/APPELLANT OF DAY FIXED FOR HEARING OF THE APPEAL
IN THE KILOLO COURT OF KILOLO
AT KILOLO
Misc. MATRIMONIAL APPLICATION NO: 1 OF 2019
EMILIO MARCUS LALIKA..................APPLICANT
Versus
MARRY JOHN MATEMBO........................RESPONDENT

To:
MARRY JOHN MATEMBO

Take Notice that an appeal/application from decree/order of judgment in the case has been presented by **EMILIO MARCUS LALIKA.**

And registered in this court, and the 23rd day of September 2019 at 9am been filed court for Mention of the appeal.

**GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT THIS 10 day of September 2019**

215418302

BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA SINGIDA
LILILOPO KATIKA OFISI YA MKUU WA MKOA WA SINGIDA
MAOMBI MADOGO NO. 55 OF 2018

JULIUS MAKALA........................MSHINDA TUZO
(Msimamizi wa mirathi ya Marehemu Gerson Mkumbo Makala)
Dhidi ya
1. ZANTEL TANZANIA
2. ARON ABDI BAKARI

KWA: ZANTEL TANZANIA
POPOTE ULIPO TANZANIA

**KUITWA SHAURINI**


Kwa kuwa Mshinda tuzo ameleta maombi yake ya kukaza hukumu ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala ya maombi, ambayo yanaweza kupatikana katika Baraza hili. Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria hapa Barazani tarehe **16/09/2019 saa 2:00** asubuhi siku ya kusikilizwa kwa shauri hilo.

**ANGALIA:** Kushindwa ua kupuuza kufika tarehe na saa iliyotajwa hapo juu kesi itapangwa kusikilizwa upande mmoja na uamuzi kutolewa.

Hati hii imetolewa kwa AMRI yangu na **CHAPA ya BARAZA** hili leo tarehe **03 Mwezi wa 09 mwaka 2019.**

115418502

## CHETI KIMEPOTEA




**Omary J. Sanyagi** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0445/0157** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa Mwaka 2006 katika shule ya Sekondari Mwembetogwa.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kwenye kituo cha polisi kilicho karibu.

**Taarifa ya polisi: IRI/IRI/RB/297233/2019**

115418202

## KUPOTEA KWA CHETI



**Thomas Buhunile** anatangaza kupotea kwa vyeti vifuatavyo: cheti cha kidato cha nne chenye index **namba S0101/0397** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2006 katika shule ya Sekondari Azania, Cheti cha kidato cha nne chenye **index namba P0465/0642** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2007 katika Shule ya Sekondari Jamhuri .

Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
**Polisi Taarifa: KGD/RB/6843/2012**

115418002

## SUNDI (T) LIMITED

### TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **Akiba Commercial Bank** tutauza kwa mnada wa hadhara magari ya mdaiwa ndugu **Gilbert Thomasy Mmassy**.

Mnada utafanyika kuanzia saa 4.00 asubuhi mpaka saa 10.00 jioni, tarehe 21/9/2019.

| NA | DHAMANA | MAHALI | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1 | GARI AINA YA MITSUBISHI CANTER. YENYE NAMBA ZA USAJILI T650 ASG | SUNDI AUCTION MART | 21/9/2019 |
| 2. | GARI AINA YA TOYOTA NOAH. YENYE NAMBA ZA USAJILI T720 CXV | SUNDI AUCTION MART | 21/9/2019 |

**MASHARTI YA MNADA:**
A) Mnunuzi atalipa 25% (au zaidi) ya bei aliyoshinda na salio litalipwa ndani ya siku saba (7) kuanzia tarehe ya mnada

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kwa simu Na
0715 549 782 : 0713 893 706


Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi

Kwa Bei Poa Tupigie 0767 223311

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku

Tupigie
0767 223 311

Nipashe
MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI MICHEZO



# MESSI KUIKOSA VALENCIA LEO

**BARCELONA, Hispania**

LIONEL Messi hatakuwa sehemu ya kikosi cha Barcelona kitakachochuana na Valencia wikiendi hii, huku pia kukiwa na wasiwasi kama atakuwa fiti kukipiga kwenye mechi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Nyota huyo wa Argentina mwenye umri wa miaka 32, bado hajaichezea mechi yoyote Barcelona msimu huu na ataendelea kuwa benchi kutokana na maumivu ya misuli ya kigimbi aliyopata kwenye kipindi cha mapumziko ya majira ya joto.

Bila Messi, Barcelona wameshinda mara moja tu katika mechi nane alizokosa pamoja na zile za Novemba mwaka jana.

Kwa msimu huu, Barca wamekusanya pointi nne tu katika mechi zao tatu walizocheza kwenye La Liga.

Kocha wa miamba hiyo ya Nou Camp, Ernesto Valverde, amesema kwamba mshindi huyo mara tano wa Balon d'Or alipaswa kuwa fiti baada ya mapumziko ya mechi za kirafiki.

Lakini, kwa mazoezi ya Jumanne na Jumatano, Messi alionenkana akifanya kivyake kwa sababu bado hajapona vizuri.

Hivyo Messi hatarajiwi kuonekana uwanjani leo Jumamosi kwenye mchezo dhidi ya Valencia.

Pia Messi anaweza kukosa mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Borussia Dortmund.

## WENGER: SOLSKJAER HAWEZI KUIPA UBINGWA UNITED

**LONDON, England**

ARSENE Wenger amesema kuwa, kocha wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer hawezi kutwaa ubingwa Ligi Kuu England akiwa na wachezaji chipukizi.

Manchester United imeanza ovyo msimu huu ikishinda mechi moja, kutoka sare mbili na kufungwa moja, na tayari Wenger anaamini United haina wachezaji waliopevuka vya kutosha kuweza kupata mafanikio msimu huu.

Wenger ameweka wazi kuwa kikosi hiki ni tofauti na kile kizazi cha United cha mwaka 1992, ambacho kilipandishwa kutoka kikosi cha vijana na kocha maarufu wa zamani, Sir Alex Ferguson na kupata mafanikio makubwa kwa kipindi kirefu.

Wenger anaamini kwamba wachezaji vijana wa United kama Scott McTominay, Mason Greenwood na Daniel James hawajajiandaa kuwa wachezaji wa kuanza katika klabu kubwa kama ya United na itakuwa ngumu kwao kupata mafanikio.

"Unapoona unajua kuwa ni mmoja kati ya mfano wa sehemu ambapo kuna vipaji lakini bado hawajajua kucheza kwa pamoja. Labda hawa wachezaji hawajapevuka vya kutosha kuweza kuibeba timu kama Manchester United," alisema Wenger.



## LIGI KUU ENGLAND KUWASHA MOTO WIKIENDI HII

**LONDON, England**

LIGI Kuu England inarudi tena leo Jumamosi kwa viwanja mbalimbali kuwaka moto baada ya mapumziko ya kupisha mechi za kimataifa.

Liverpool ambao tangu ligi imeanza hawajapoteza mchezo wowote watakuwa uwanja wa nyumbani pale Anfield kuwakaribisha Newcastle United ambao katika mechi zao nne zilizopita wameshinda moja, kutoa sare moja na kufungwa mbili.


Manchester United wao watakua nyumbani 'Old Traford' kuwakaribisha Leicester City, mechi hii itakua kali kutokana na mwenendo wa Manchester United kutotabirika huku wenzao Leicester wakiwa kwenye kiwango bora maana mechi nne zilizopita wameshinda mbili na kutoa sare mbili, huku wenyeji Manchester United wameshinda mechi moja, sare mbili na kufungwa moja na Crystal Palace.

Chelsea chini ya kocha wao Frank Lampard watakua wakikipiga ugenini dhidi ya Wolverhampton Wanderers ambapo mechi nne za Ligi Kuu zilizopita wameshinda mchezo mmoja, sare mbili na kupoteza mmoja huku wapinzani wao Wolves wakitoa sare mechi tatu na kufungwa moja dhidi ya Everton.

Manchester City pia watakua ugenini kucheza na Norwich City ambao wamepoteza michezo mitatu na kushinda mchezo mmoja kati ya minne ya ligi iliyopita.

Tottenham Hotspur watakuwa nyumbani kuwakaribisha Crystal Palace ambao mechi za ligi nne zilizopita wameshinda mechi mbili, sare moja na kupoteza moja wakati wenyeji Tottenham wakishinda moja sare mbili na kupoteza moja.

Mechi nyingine ni Brighton and Hove Albion dhidi ya Burnley huku Sheffield United watakua nyumbani kuwakaribisha Southampton.





# KUMBE

## POGBA ALISHAMALIZANA NA PSG

**MANCHESTER, England**

IMETHIBITIKA kuwa, kiungo wa Manchester United, Paul Pogba, alishafikia makubaliano ya maslahi binafsi na uongozi wa Paris Saint-Germain, lakini mambo yalivurugika siku chache kabla ya dirisha la usajili wa majira ya joto kufungwa.

Jarida la michezo la Calciomercato la nchini Italia, limefichua siri hiyo iliyokua ikiendelea nyuma ya pazia, na limeeleza Pogba alikubali mshahara wa pauni 429,000 kwa wiki.

Sababu kubwa iliyotajwa hadi kuvurugika kwa dili hilo, ni hatua ya mshambuliaji kutoka nchini Brazil Neymar, kushindwa kufanikisha azma yake ya kurejea Barcelona.

Hata hivyo, Jarida hilo limeeleza kuwa, mbali na PSG kupewa nafasi kubwa ya kumsajili Pogba, pia klabu nyingine kama Barcelona na Real Madrid zilikua tayari kupambana kwenye kinyang'anyiro cha usajili kiungo huyo.

"Kocha wa PSG Thomas Tuchel, alihitaji huduma ya kiungo huyo, na mara kadhaa aliutaka uongozi wake kufanya jitihada za kufanikisha dili hilo, lakini mambo yalikwenda kombo." imeelezwa katika taarifa iliyochapishwa kwenye jarida la Calciomercato.

Kwa mantiki hiyo Pogba amekosa dili nono la mshahara wa pauni milioni 22 kwa mwaka, na huenda ingemweka katika ramani tofauti, endapo angefanikiwa kurejea nyumbani kwao Ufaransa.

# Madrid yamfungia kazi Kante

**MADRID, Hispania**

REAL Madrid na Chelsea zimefikia makubaliano maalumu kuhusu uhamisho wa kiungo, N'Golo Kante, kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail.

Makubaliano hayo yanaipa nafasi Real Madrid kuwa ya kwanza kufahamishwa na Chelsea kama inamuuza nyota huyo wa kimataifa wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 28 au kama kuna klabu nyingine zinamtaka nyota huyo.

Inadaiwa Kocha wa Real Madrid, Zinedine Zidane kwa muda mrefu amekuwa akimtaka kiungo huyo, huku Chelsea ikiwa imegoma kumuuza lakini sasa Madrid imepewa nafasi ya kumnunua kama klabu nyingine zikimtaka.

Madrid inaweza kumnasa Kante baada ya mwaka mmoja katika dirisha kubwa la majira ya joto.

Kwa kufanya hivyo, Kante ataungana tena na Eden Hazard ambaye alikuwa naye Chelsea.

Kante amekuwa mmoja kati ya viungo bora barani Ulaya tangu alipoibuka katika kikosi cha Leicester City kilichotwaa ubingwa wa Ligi Kuu England Mei 2016 lakini achilia mbali kutakiwa na Real Madrid pia amekuwa akitakiwa na mabingwa wa Ufaransa PSG.



# LUKAKU KUONGOZA KAMPENI KUPINGA UBAGUZI

**MILAN, Italia**

MSHAMBULIAJI wa Inter Milan, Romelu Lukaku ameombwa kuongoza kampeni ya kupinga ubaguzi wa rangi nchini Italia.

Lukaku mchezaji wa zamani wa Manchester United alikumbwa na kelele za kibaguzi wiki chache zilizopita wakati alipokuwa akiitumikia Inter Milan, ambapo mashabiki walidai wao walipiga tu kelele za nyani, lakini haikuwa ubaguzi.

Lakini, maofisa wa Ligi Kuu Italia, Serie A, wamesema wametambua kwamba kuna tatizo kubwa na kumtaka Lukaku na beki wa Napoli, Kalidou Koulibaly kuwa sehemu ya vinara kwenye vita ya kupambana na ubaguzi kwenye soka la Italia.

Serie A wanataka kuanzisha kampeni inayofanana na 'Kick It Out' inayofanyika huko England ili kukomesha vitendo hivyo vya kibaguzi.

Jambo hilo linawafanya kuwataka Lukaku na Koulibaly kuwa wasimamizi wakubwa wa jambo hilo.

Mastaa hao wote wawili waliwahi kukumbwa na tatizo la kelele za kufanyiwa ubaguzi huko Italia, licha ya kwamba mara kadhaa mashabiki wamekuwa wakikanusha kufanya ubaguzi, ila tu wamekuwa wakifanya ili kuwavuruga wapinzani.

Kundi la mashabiki wa Inter linalofahamika kwa jina la 'L'Urlo Della Nord' lilidai kwamba Lukaku anapaswa kutambua kwamba kelele zile za nyani zilifanywa kwa malengo tu ya kumvuruga mchezaji wa timu pinzani ili kusaidia timu.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# VAN DER SAR KUREJEA UNITED

Mkongwe huyo afungua milango kwa klabu yake hiyo ya zamani kurejea...

**AJAX, Uholanzi**

MLINDA mlango wa zamani wa Manchester United, Edwin van der Sar, amefungua milango kwa klabu yake hiyo kwamba anaweza kurejea katika timu hiyo mara baada ya muda wake wa kuitumikia Ajax utakapomalizika.

Mkongwe huyo mwenye umri wa miaka 48 ambaye ni Mtendaji Mkuu wa mabingwa hao wa Ligi Kuu Uholanzi maarufu Eredivisie, amesema hayo baada ya kuwapo na mazungumzo endapo United itahitaji kumwajiri kama Mkurugenzi wa Ufundi wa klabu hiyo.

Van Der Sar ambaye kwa sasa anaitumikia na kuisaidia Ajax, lakini amekuwa tayari kufungua milango kwa kupata klabu nyingine ya kuifanyia kazi na kuongeza kwamba anaweza pia kufanya majukumu mengine tofauti ndani ya klabu.

"Huwezi kujua, kwa sasa akili na nguvu zangu nimezielekeza katika klabu hii ya Ajax, na kitakachotokea hapo baadaye tutakijua hapo hapo," golikipa huyo wa zamani wa United alisema.

"Nafikiri kwamba, nafasi ya kuendelea kukua na kujifunza inapotokea ni vema kuipokea. Hicho ndicho unachotakiwa kukifanya kama mchezaji wa mpira wa miguu.

"Hii iliwahi kutokea pale nilipokwenda nchini Italia na kwa wakati nilipoelekea England kwa kuichezea Fulham na baadaye United, ni mwendelezo wa kawaida.

"Hapa Ajax tunapambana kuhakikisha tunaifanya klabu inakuwa moja ya timu bora kwenye ukanda wa Ulaya na si tu kutoka kwenye moja ya nchi tano kubwa."

Van Der Sar pia aliisaidia United kumaliza mgogoro wa mkataba uliomhusisha golikipa wake, David de Gea, lakini alisisitiza kwamba timu hiyo inayo wachezaji wenye uwezo mzuri ambao wanaweza kuziba pengo la Mhispania huyo ambaye anatajwa kutaka kuondoka klabuni hapo.

"Magolikipa wengine waliopo wanaweza kuziba nafasi yake itakayoachwa," aliongeza. Kuna magolikipa wachache kwenye Ligi Kuu England ambao wanacheza katika timu zao ambaye wanaweza kupandishwa.

"Uamuzi huwa unakuja kulingana na wakati husika. Huchukua muda mrefu sasa, ni suala la kusema ndio au hapana. Viwango vyao hutofautiana. Ameendelea kuwa kwenye ubora wa juu kwa muda mrefu, inafika wakati anajitambua.

"Huenda ikawa ni mara yake ya pili, lakini watu wanaweza kuandika kuhusu yeye, na ikaonekana ni jambo sahihi. Ni golikipa mwenye kiwango cha juu kwa sasa."

## KWA UFUPI

**MADDISON ANUKIA UNITED**

MANCHESTER United imeanza mchakato wa kumwania kiungo wa Leicester City, James Maddison ambaye ana umri wa miaka 22 kwa ajili ya kujiunga kwenye kikosi chake katika kipindi cha majira ya joto mwakani. ***(Manchester Evening News)***

**CITY YATOA NENO EPL**

MANCHESTER City imependekeza kuwapo kwa mabadiliko ya uhamisho katika usajili wa wachezaji wa ndani kabla ya kuanza kwa msimu wa Ligi Kuu England lakini klabu kubwa zikiwa na ruhusa ya kuendelea kusajili kutoka katika timu za Ulaya hadi mwishoni mwa Agosti. ***(Mail)***

**RUIZ AGOMBEWA ULAYA**

LIVERPOOL, Real Madrid, Barcelona na Bayern Munich zote zimeonyesha nia ya kumwania kiungo wa Napoli na Timu ya Taifa ya Hispania, Fabian Ruiz ambaye kwa sasa ana umri wa miaka 23. ***(Calciomercato, via Mail)***

**ZIDANE AMTAJA KANTE**

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane, ameweka wazi kwamba anataka kumsajili kiungo wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Ufaransa, N'Golo Kante (28). ***(The Athletic - subscription required)***

**POGBA SAFARI YANUKIA**

MABOSI wa United wamesema watakuwa tayari kumuuza kiungo wake Mfaransa Paul Pogba (26), kwa Real Madrid katika kipindi cha dirisha dogo la Januari kama vigogo hao wa Hispania watakubali kumjumlisha kiungo Mjerumani Toni Kroos (29), katika mchakato wa usajili huo. ***(Diario Madridista - in Spanish)***

**TERRY ATAJWA CHELSEA**

NAHODHA wa zamani wa Chelsea, John Terry, ametajwa kuwa siku moja anaweza kuwa kocha mkuu wa timu hiyo, kauli hiyo imesemwa na kocha wa zamani wa klabu hiyo, Roberto di Matteo. ***(The Athletic, via Birmingham Mail)***

**WILLIAN: CHELSEA ITASUMBUA**

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Brazil, Willian (31), amesema kuwa anaamini Chelsea ina uwezo wa kutwaa mataji mbalimbali msimu huu licha ya kocha mpya wa timu hiyo, Frank Lampard kufanya kazi katika mazingira magumu na yenye changamoto mbalimbali. ***(Standard)***

**LINDELOF MAMBO SAFI**

MANCHESTER United inajiandaa kumpa ofa mpya ya kumlipa mshahara mara mbili ya anachopokea sasa, beki wa Timu ya Taifa ya Sweden, Victor Lindelof (25) ambao utamfanya awe analipwa pauni 150,000 kwa wiki. ***(Sun)***

**SOUTHGATE: VARDY ANAHITAJIKA**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa ya England, Gareth Southgate, amesema kuwa straika wa Leicester City, Jamie Vardy, anaweza kurejea katika kikosi chake, licha ya nyota huyo mwenye umri wa miaka 32 kutangaza kustaafu soka la kimataifa hapo mwaka jana. ***(Times - subscription required)***

**AURIER KUONDOKA SPURS**

BEKI wa kulia wa Tottenham ambaye pia anakichezea kikosi cha Ivory Coast, Serge Aurier (26), amekiri kwamba anataka kuondoka katika klabu hiyo katika majira ya joto. ***(Football.London)***

**BOLASIE AJITABIRIA MAZURI**

WINGA wa Everton na Timu ya Taifa ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Yannick Bolasie (30), amesema kuwa anaamini mchakato wake wa kujiunga na Sporting Lisbon kwa mkopo utakamilika katika kipindi cha majira ya joto mwakani na atapewa mkataba wa kudumu. ***(Record, via Sport Witness)***

**UNITED KUNASA KINDA**

MANCHESTER United imeanza mchakato wa kumsajili golikipa chipukizi wa Reading, Coniah Boyce-Clarke ambaye ana umri wa miaka 16. ***(Mirror)***

## HABARI MICHEZO

# MAJALIWA AZIPA NENO SIMBA, YANGA AFRIKA

**Na Sanula Athanas, DODOMA**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amezipongeza Yanga, Azam FC na Malindi kwa kufanikiwa kuingia katika hatua ya pili ya michuano ya Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Vilevile, kiongozi huyo wa serikali amezitaka klabu za Simba na KMC kujitathimini kutokana na kuondoshwa mapema katika mashindano ya shirikisho hilo msimu huu.

Katika hotuba yake ya kuahirisha mkutano wa 16 wa Bunge la 11 jijini Dodoma jana, Majaliwa alisema anawapongeza Azam FC, Malindi na Yanga, aliyoiita 'Timu ya Wananchi' kwa kufanikiwa kusonga mbele na kuingia hatua ya pili katika michuano ya CAF, akieleza kuwa wameiwakilisha vyema nchi kimataifa.

"Kwa vilabu vya KMC, KMKM na Simba, ambavyo vimeondolewa katika hatua ya mwanzo kabisa, vichukulie hali hiyo kama changamoto ya kujitathimini na kujiandaa kwa ajili ya michezo ya ndani na mashindano yajayo ya kimataifa badala ya kutumia muda mrefu kujadili kuhusu kutolewa mapema," alisema.

Waziri Mkuu pia alisema anaipongeza kwa dhati Timu ya Taifa ya Wanawake chini ya Umri wa Miaka 20 'Tanzanite' kwa kutwaa kombe la michuano ya soka kwa Nchi za COSAFA huko Port Elizabeth, Afrika ya Kusini.

Majaliwa pia aliipongeza Timu ya Taifa 'Taifa Stars' kwa kufanikiwa kuiondoa Harambee Stars (Kenya), katika mashindano ya CHAN 2020.

Pia, aliimwagia pongezi timu hiyo kwa kuiondoa Burundi na kufanikiwa kuingia hatua ya makundi ya kufuzu Kombe la Dunia huko Doha, Qatar mwaka 2022.

Alisema hatua hiyo ni nzuri na muhimu kwa kuwa inaiweka timu hiyo katika nafasi nzuri kushiriki fainali za mashindano hayo makubwa zaidi duniani.

"Timu ya Taifa itarudi dimbani kupambana na Sudan Septemba 22, mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa. Kama kawaida yetu, twendeni tukaujaze uwanja wetu na kuishangilia kwa nguvu timu yetu ya taifa," Waziri Mkuu alitoa rai.

Kwa upande wa masumbwi, Majaliwa alisema bendera ya Tanzania imeendelea kupeperushwa vyema kufuatia wana masumbwi wengine wawili wa Kitanzania kuendelea kufanya vizuri katika medani za kimataifa.

"Nitumie nafasi hii kuwapongeza mwanamasumbwi Abdallah Shaaban Pazi maarufu Dulla Mbabe kwa kufanikiwa kutwaa ubingwa wa Dunia wa WBO baada ya kumpiga kwa KO kwenye raundi ya tatu mpinzani wake Mchina anayejulikana kwa jina la Zulipikaer Maimaitiali.

Waziri Mkuu aliitaka wizara kuendelea kuratibu vizuri shughuli za michezo, utamaduni na sanaa ili zilete ufanisi wa hali ya juu na pia kuweka msisitizo sambamba na kuwa na mikakati ya kuendeleza michezo ikiwamo shuleni, vituo maalumu vya michezo sambamba na kuwa na mifumo mizuri ya upatikanaji wa fedha.




Mabalozi wa Taasisi ya Tulia kutoka kushoto, Mwasiti Almassy, Dotto Bernard "Ditto" na Yvonne Cherrie " Monalisa", wakitambulisha nembo ya Tamasha la Ngoma za Jadi linaloandaliwa na taasisi hiyo litakalofanyika baadaye mwezi huu mjini Tukuyu, Mbeya.
**PICHA: SOMOE NG'ITU**

# Kelvin amfuata Samatta Ubelgiji

**Na Faustine Feliciane**

NYOTA ya wachezaji wa Tanzania kucheza soka la kulipwa Ulaya inaendelea kung'ara baada mshambuliaji chipukizi, Kelvin John, kupata mwaliko wa kwenda katika klabu ya KRC Genk ya Ubelgiji, ambayo anaichezea nahodha wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Mbwana Samatta, imefahamika.

Kwa muda mrefu Kelvin licha ya kujumuishwa mara kwa mara kwenye timu za taifa, hakuwa na timu ya kuichezea hali iliyopelekea wadau wengi wa soka kupiga kelele wakitaka mchezaji huyo apate klabu ili kutunza kipaji chake huku mipango ya kusaka klabu Ulaya ikiendelea.

Taarifa zilizopatikana jijini Dar es Salaam jana, zinaeleza kuwa KRC Genk imetuma barua kwa ubalozi wa nchi hiyo nchini Tanzania ikielezea kumuita kinda huyo kwenda nchini humu kwa ajili ya majadiliano ya kusaini mkataba.

Nipashe imeiona nakala ya barua hiyo ambayo pia ilikuwa inampatia viza ya kuingia nchini humo kwa ajili ya kukamilisha mchakato wa kuanza kucheza soka la kulipwa.

Barua hiyo pia imeelezea mahali ambapo mshambuliaji huyo atafikia na klabu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu Ubelgiji ikiweka wazi, ndiyo italipa gharama zote za usafiri na malazi kwa muda wote atakaokuwa nchini humo.

Mshambuliaji huyo alianza kung'ara akiwa na kikosi cha Timu ya Taifa ya Vijana ya umri chini ya miaka 17 (Serengeti Boys), ambacho kilishiriki Fainali za Kombe la Mataifa Afrika (AFCON U-17 2019), ambazo zilifanyika Aprili mwaka huu hapa jijini.

# Zawadi zaboreshwa Tamasha la Tulia

**Na Mwandishi Wetu**

VIKUNDI vya sanaa zaidi ya 100 kutoka mikoa ya Tanzania Bara na Visiwani vinatarajia kushiriki katika Tamasha la Ngoma za Jadi maarufu "Tulia Traditional Dance Festival" linalotarajiwa kufanyika kuanzia Septemba 26 hadi 28 mwaka huu Tukuyu jijini Mbeya, imeelezwa.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Balozi wa Taasisi ya Tulia, Yvonne Cherrie "Monalisa", alisema kuwa lengo kuu la tamasha hilo ambalo linafanyika kwa mwaka wa tatu mfululizo ni kusaidia jamii na ikilenga zaidi wanawake, vijana na watoto.

Monalisa alisema kuwa wanatarajia kupitia tamasha hilo, jamii itaendelea kuenzi tamaduni zake mbalimbali za Kitanzania.

"Tutapata nafasi ya kujifunza ngoma na tamaduni za makabila mengine, pia mwaka huu kila kikundi kitaruhusiwa kuja na wanawake wawili ambao watapika vyakula vya asili, tutapata nafasi ya kula vyakula vya kimanyema kutoka Kigoma, madikodiko ya Tanga na vingine vingi," alisema Monalisa.

Aliongeza kuwa katika kufanikisha tamasha hilo linafanyika kwa mafanikio, taasisi ya Tulia inaushukuru Ubalozi wa China kwa kusaidia maandalizi mbalimbali.

Naye Dotto Bernard "Ditto" alisema kuwa kikundi kitakachofanya vizuri katika tamasha hilo na kushika nafasi ya kwanza, kitapata zawadi ya pikipiki 22, ikimaanisha kila msanii ataondoka na pikipiki yake.

Alitaja zawadi ya mshindi wa pili itakuwa ni Sh. milioni moja kwa kila mwanakikundi huku wale watakaoshika nafasi ya tatu watajinyakulia zawadi ya Sh. 700,000 huku kila kikundi kikipewa Sh. 400,000 za ushiriki.

"Tamasha la mwaka huu ni tofauti na miaka iliyopita kwani zawadi zimeongezeka pamoja na washiriki, pia nafasi ya wasanii watakaokwenda kusoma katika Chuo cha Sanaa Bagamoyo zimeongezeka na kufikia 40," alisema Monalisa.

Naye msanii wa bongo fleva na balozi wa taasisi, Mwasiti Almasy, ambaye pia ni balozi wa Tulia Trust alisema kuwa katika tamasha hilo linatarajiwa kuwa na watazamaji zaidi ya 15,000.

# Shime ajivunia Twiga Stars

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), Bakari Shime, amesema kuwa kikosi chake kinaendelea kuimarika na anaamini kitafanya vema katika mashindano ya Afrika Mashariki na Kati yatakayofanyika hapa nchini mapema mwezi ujao.

Twiga Stars ndio mabingwa watetezi wa mashindano hayo yatakayofanyika kwa mara ya tatu kwenye ukanda huu chini ya usimamizi wa Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa).

Akizungumza na gazeti hili jana, Shime, alisema kuwa kila mchezaji anaonyesha kujituma kwenye mazoezi hayo ili aweze kubakia katika kikosi cha mwisho kitakachoshiriki michuano hiyo.

Shime alisema kuwa kwa sasa ana wachezaji 40 katika kikosi hicho na anamshukuru Mungu, hana mchezaji ambaye ana majeruhi makubwa.

Aliongeza kuwa anafurahi kuona Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), linaipa kipaumbele timu hiyo kwa kukubali kutekeleza programu zake mbalimbali za maendeleo.

Michezo
Jumamosi Septemba 14, 2019
Nipashe



## Van Der Sar kurejea United

HABARI UK 30



Wachezaji wa Timu ya Real Madrid wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya La Liga dhidi ya Levante itakayochezwa leo mchana: **PICHA: MTANDAO**

# ZAHERA ATAMBA ZESCO HAWATOKI

●●●Kocha huyo Mkongomani aeleza mikakati ya kumaliza kazi Taifa...

**Na Somoe Ng'itu**

HATUMWI mtoto! Ndio maneno yanayozungumzwa na wenyeji kuelekea mchezo wa mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika kati ya Yanga dhidi ya Zesco FC kutoka Zambia unaotarajiwa kuchezwa leo kuanzia saa 10:00 jioni kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Yanga ilisonga mbele katika mashindano hayo baada ya kuwaondoa Township Rollers ya Botswana kwa jumla ya mabao 2-1.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera, alisema kuwa kikosi chake kimejiandaa vema kuwakabili Zesco na kila mchezaji yuko imara kwa ajili ya kutimiza majukumu atakaowakabidhi katika mchezo huo.

Zahera alisema kuwa hawana hofu na wapinzani wao na anaamini wachezaji wake watatumia vizuri nafasi ambazo watazitengeneza katika mchezo huo na hatimaye kupata matokeo mazuri.

"Tumefanya mazoezi mazuri, programu zote za kuhakikisha tunapata ushindi tumezikamilisha, tusubiri muda wa kutekeleza tuliyojiandaa nayo, ila ni mechi ngumu kwetu na kwa Zesco pia," alisema kocha huyo raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Naye Kocha Mkuu wa Zesco, Mzambia George Lwandamina, aliliambia gazeti hili kuwa kikosi chake kiko tayari kwa mchezo huo wa leo na anaamini wachezaji wake wataonyesha soka la kuvutia kwenye mchezo huo wa kwanza wa raundi ya kwanza.

Lwandamina alisema kuwa kikosi chake kimecheza mchezo mmoja wa Ligi Kuu Zambia na mechi mbili za kimataifa, lakini wamejipanga kuendelea kupata matokeo chanya kwenye mchezo huo.

"Kama mnavyofahamu, tumekuja tukitokea katika maandalizi ya msimu mpya, tumecheza mechi mbili za kimataifa, na moja ya ligi ya ndani, lakini timu iko tayari kukabiliana na changamoto ya aina yoyote kuelekea mchezo huo, Zesco imekuwa katika mabadiliko katika kikosi chake, kuna wachezaji kama watatu niliowaacha, wameondoka, timu iliyopo ni timu mpya ambayo ndiyo imeanza kuimarika na tutarajie mechi yenye ushindani," alisema Lwandamina. Kocha huyo wa zamani wa Yanga aliongeza kuwa wamejipanga kukabiliana na ushindani kutoka kwa Yanga ambayo pia imefanya mabadiliko katika kikosi chake, benchi la ufundi pamoja na uongozi mzima wa klabu hiyo.

"Mechi ya Jumamosi inatarajiwa kuwa na kuvutia, hasa ukizingatia, timu zote mbili zinaundwa na sura mpya, natumaini tutalinda heshima yetu, kabla ya kurudi nyumbani kwa ajili ya mchezo wa marudiano," Lwandamina aliongeza.

Wawakilishi wengine wa Tanzania waliobakia katika mashindano ya kimataifa ni Azam FC ambao wataikaribisha Triangle United kutoka Zimbabwe kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika huku Malindi ya Zanzibar itawavaa Al Masry ya Misri kwenye Uwanja wa Amaan katika michuano hiyo.

## Kagere, Miraji waipaisha Simba

**Na Faustine Feliciane**

NYOTA ya mshambuliaji wa mabingwa watetezi, Simba, Meddie Kagere, imeendelea kung'ara baada ya kufunga bao moja katika ushindi wa magoli 2-1 katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Mtibwa Sugar uliochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Kwa matokeo hayo, Simba imefikisha pointi sita na kukaa kileleni katika msimamo wa ligi hiyo ambayo inatarajia kuendelea tena kesho.

Bao hilo la Kagere ambalo ni la tatu msimu huu lilipatikana dakika ya 17 baada ya kuunganisha pasi ya kisigino iliyopigwa na kiungo Sharaf Shiboub aliyepokea krosi ya Hassan Dilunga.

Hata hivyo bao hilo lilidumu kwa dakika tatu tu kabla ya Mtibwa Sugar kusawazisha kupitia kwa Riffat Hamisi aliyeunganisha kwa kichwa mpira wa kona uliopigwa na Haruna Chanongo na kushinda mlinda mlango wa Simba, Aishi Manula ambaye jana alikuwa akisherehekea siku yake ya kuzaliwa.

Ilimchukua dakika tano tu, kwa Miraji tangu alipoingia uwanjani kuipatia Simba bao la pili la ushindi akiitumia vema pasi ya Shiboub na kuachia shuti kali lililomshinda mlinda mlango Shaaban Hassan "Kado" ambaye jana alifanya kazi kubwa kuwazuia Simba kuibuka na ushindi mnono.

Licha ya Simba kufanya mashambulizi ya mara kwa mara, bado Mtibwa Sugar ilikaa imara na kumaliza kipindi cha kwanza wakiwa sare bao 1-1.

Kocha wa Simba jana alilazimika kuanza na mshambuliaji mmoja wa asili huku kiungo Shiboub akicheza kama namba 10 kufuatia kuwa nahodha wa timu hiyo, John Bocco kutokuwa fiti.

Kipindi cha pili kilianza kwa kasi huku timu zote zikifanya mabadiliko ambapo Simba walimtoa Dilunga na nafasi yake kuchukuliwa na Miraji dakika ya 63, huku pia akimtoa Clatous Chama dakika ya 79 na nafasi yake kuchukuliwa na Francis Kahata wakati Mtibwa Sugar kwa upande wao walimtoa Chanongo dakika ya 67 na nafasi yake kuchukuliwa na Omari Hassan huku Issa Rashid, akiumia na nafasi yake kuchukuliwa na mkongwe, Henry Joseph.

Katika mechi nyingine ya ligi hiyo, Coastal Union ilipata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya KMC katika mchezo uliochezwa kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini Tanga.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002